Kiswahili

Kuishi Kusio kwa Kawaida

Kupitia Vipawa vya Roho Mtakatifu

Na A.L. na Joyce Gill

Kuishi Kusio kwa Kawaida

Kupitia
Vipawa vya Roho Mtakatifu

na
A.L. na Joyce Gill

www.gillministries.com

Vitabu katika Mwongozo Huu

Mamlaka ya Mwamini
Jinsi ya kukoma kushindwa na Kuanza Kushinda

Ushindi wa Kanisa
Kupitia Kitabu Cha Matendo

Karama za Huduma
Mtume, Nabii, Mwinjilisti,
Mchungaji, Mwalimu

Uinjilisti wa Mwujiza
Mpango wa Mungu Kufikia Ulimwengu

Sura ya Kuumbwa Upya
Kutambua Wewe ni Nani Katika Kristo

Mbinu za Kuishi
Kutoka Agano la Kale

Sifa na Kuabudu
Kufanyika Waabudu wa Mungu

Maombi
Kuileta Mbingu Duniani

Kuhusu Waandishi

A.L. na Joyce Gill ni wanenaji wanaojulikana kimataifa, waanzilishi na walimu wa Biblia. Huduma ya utume ya usafiri wa A.L. umempeleka katika nchi zaidi ya sitini, akihubiri kwa umati unaozidi elfu mia moja ya watu na pia kupitia redio na runinga kwa mamilioni.

Vitabu vyao na nakala inayouza sana imeuzwa zaidi ya milioni saba. Maandishi yao, ambayo yametafsiriwa katika lugha nyingi, inatumika katika shule za Biblia na katika semina duniani.

Kweli zenye nguvu zibadilishayo maisha za Neno la Mungu zinalipuka katika maisha ya wengine kupitia huduma za mahubiri, mafundisho, uandishi, video na kanda za kusikiza.

Utukufu wa ajabu wa uwepo wa Mungu unaonekana katika semina za sifa na kuabudu wakati waamini wanagundua jinsi ya kufanyika ibada ya uhusiano wa karibu na Mungu. Wengi wamegundua mbinu mpya ya ushindi na ujasiri kupitia mafundisho yao juu ya mamlaka ya mwamini.

Wamefundisha waamini wengi kuchukua hatua katika huduma zao walizopewa na Mungu kwa nguvu za uponyaji wa Mungu kupitia mikono yao. Wengi wamejifunza kuwa kawaida katika nguvu za juu wakihudumu katika vipawa vyote tisa vya Roho Mtakatifu katika maisha huduma zao kila siku.

Wote A.L. na Joyce wana shahada katika mafunzo ya Thiolojia. A.L. pia na shahada ya udaktari katika philosophia kutoka Chuo Kikuu cha Kikristo cha Vision. Huduma yao imeegemea kwa uthabiti juu ya Neno la Mungu, katikati mwa Yesu, yenye nguvu katika imani na kufundishwa katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Huduma yao huonyesha upendo wake Baba. Mahubiri yao na mafundisho huambatana na upako wa nguvu za juu,, ishara, miujiza, na uponyaji katika miujiza huku wengi wakipigwa katika nguvu za Mungu.

Ishara za uvuvio unaojumlisha mawimbi ya kicheko kitakatifu, kilio mbele za Bwana na kuonekana utukufu wa ajabu wa Mungu unaonekana na wengi wanaohudhuria mikutano zao.

Neno kwa Walimu na Wanafunzi

Mafundisho haya yenye nguvu juu ya uponyaji yanaweka msingi dhabiti wa Neno ambalo huachilia imani kwa wanafunzi ili kupokea uponyaji wao, kuenda katika afya, na kwa ujasiri kuhudumu uponyaji kwa wengine. Wengi wataponywa wakati ufunuo huu utafanyika hai rohoni mwao.

Katika kitabu cha Mariko, maneno ya maagizo ya mwisho ya Yesu kabla hajaondoka duniani yalikuwa, "wataweka mikono yao juu ya wangonjwa nao watapona." Kitabu hiki kinatoa maagizo ya wazi jinsi ya kuhudumia uponyaji kwa wagonjwa.

Kabla ya kufundisha somo hili, tazama au sikiliza video na kanda katika mwongozo huu, na pia soma vitabu vilivyoorodheshwa kama pendekezo. Kadri unavyokolea katika ukweli wa Neno la Mungu kuhusu uponyaji, ndivyo kweli hizi zitaingia moyoni mwako. Nakala hii basi itatoa muhtasari wa kutumia unapotoa kweli hizi kwa wengine.

Mifano ya binafsi ni bora na lazima kwa mafundisho bora. Waandishi hawajatumia katima nakala hii ili mwalimu aweze kutoa mifano yake binafsi yenye ustadi, au kwa wengine ambayo wanfunzi watakubaliana nayo.

Na ikumbukwe kila mara kuwa ni Roho Mtakatifu ndiye mwalimu wetu, na kuwa tunapojifunza, au kufundisha, kila mara tutiwe nguvu na kuongozwa na Roho Mtakatifu.

Mafundisho haya ni bora kwa binafsi au kikundi, shule za Biblia, Shule ya Jumapili na makundi ya nyumbani. Ni muhimu kuwa mwalimu na mwanafunzi wawe na nakala ya kitabu hiki wakati wa masomo.

Andika ndani, tia mistari, tafakari na kutoa maoni katika kitabu hiki. Tumeacha nafasi kwa ajili yako. Mtindo uliotumika ni kwa ajili ya marejeo ya haraka ili kurudia na kusaidia katika kupata mada. Kimeandikwa bora ili kila mtu, baada ya kusoma kitabu hiki, waweze kuwafundisha wengine.

Paulo aliandika kwa Timotheo,
Na mambo uliyosikia kutoka kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo mwakabidhi watu waaminifu watakaowafundisha wengine pia. 2 Timotheo 2:2b

Masomo haya yameundwa kama ili kuhusika katika mafunzo ya Biblia katika Mpango wa Kuendeleza Huduma ambayo imetayarishwa kwa ajili ya mipango ya kujifunza. Wazo hili limetayarishwa kwa ajili ya kujumlisha maishani, huduma, na mafundisho ya baadaye kwa wanafunzi. Wanafunzi wa awali, kwa kutumia nakala hii, wanaweza kufundisha kosi hii wengine.

Orodha ya Yaliyomo

Somo la Kwanza	**Roho Mtakatifu**	**7**
Somo la Pili	**Kupokea Nguvu za Roho Mtakatifu**	**11**
Somo la Tatu	**Kunena Katika Ndimi**	**17**
Somo la Nne	**Sanaa Muhimu za Huduma**	**23**
Somo la Tano	**Vipawa Kutengwa na Kufafanua**	**28**
Somo la Sita	**Vipawa vya Souti - Ndimi na Kukalimani**	**34**
Somo la Saba	**Vipawa vya Souti Ya Utumainifu - Kipawa cha Unabii**	**42**
Somo la Nane	**Kipawa cha Ufunuo Kutofautisha Vipawa**	**51**
Somo la Tisa	**Kipawa cha Ufunuo - Neno la Kimaarifa**	**61**
Somo la Kumi	**Kipawa cha Ufunuo - Neno la Hekima**	**70**
Somo la Kumi na Moja	**Kipawa cha Nguvu cha Imani**	**80**
Somo la Kumi na Mbili	**Kipawa cha Nguvu cha Kutenda Miujiza**	**89**
Somo la Kumi na Tatu	**Vipawa vya Nguvu vya Uponyaji**	**96**

Scriptures in **Supernatural Living**
are taken from the **New King James Version**.
Copyright 1979, 1980, 1982 Thomas Nelson Inc., Publishers
Scriptures identified as Amplified are from **The Amplified Bible**,
Copyright 1954-1965 by Lockman Foundation and Zondervan Publishing House.

Somo la Kwanza

Roho Mtakatifu

Je, Roho Mtakatifu ni Nani?

Ikiwa ni sharti tumfahamu Mungu, si lazima tumfahamu Baba na Mwana tu, lakini pia ni lazima tumfahamu Roho Mtakatifu kwa njia ya kweli na ya kibinafsi.

Mungu ni mmoja, lakini anatambulika katika Watu watatu tofauti. Kila mmoja katika Mungu ni sawa na hushiriki katika sifa za Mungu. Kila Mtu ---------wa Mungu, kama anavyodhihirishwa, anayo kazi maalum na binafsi. Roho Mtakatifu, kama vile Baba na Mwana, hupendekeza kwetu tuje katika uhusiano wa kibinafsi Naye. Anatutaka tuishi na kutembea kwa karibu pamoja Naye, tukitambua umuhimu Wake katika maisha yetu kila siku.

KAZI YA ROHO MTAKATIFU KUDHIHIRISHWA KATIKA AGANO LA KALE

Wakati wa Kuumba

Roho Mtakatifu alikuwa sehemu ya Utatu wakati wa kuumba.

Mwanzo 1:1-3 Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi. Nchi haikuwa na muundo, na tupu; na giza lilitanda juu kote. Na Roho wa Mungu alikuwa juu ya maji.

"Roho wa Mungu" alikuwa wimbi, pumzi, mlipuko, dhoruba, mawimbi.

Zaburi 104:30 Ulituma Roho Wako, vikaumbwa; na Unafanya upya uso wa nchi.

Kujumuika na Wanadamu

➢ *Alikuja Juu ya*

Wakati wa vipindi vya Agano la Kale, Roho Mtakatifu hakukaa juu ya wanadamu. Alikuja juu yao kuwapaka kwa ajili ya kazi maalum au kitendo.

1 Samueli 10:6 Kisha Roho wa BWANA atakuja juu yako, na utatoa unabii kwao na kubadilishwa kuwa mtu mwingine.

➢ *Kupewa Hekima*

Kutoka 28:3a Basi utanena na wote walio na vipawa vya usanii, ambao nimewajaza na roho wa hekima.

➢ *Kupingana na*

Mwanzo 6:3a Na BWANA akasema, "Roho wangu hatapingana na mwanadamu milele ... "

➢ *Alinena Na*

Zekieli 2:2 Kisha Roho akaniingia aliponinenea, na kuniweka nikisimama; na nikamsikia Yeye aliyeninenea.

KAZI YA ROHO MTAKATIFU KUDHIHIRISHWA KATIKA INJILI

Wakati wa maisha ya Kristo, Roho Mtakatifu alikuja juu ya waume na wake kwa kazi maalumu, lakini kufuatia kurudi kwa Yesu mbinguni na siku ya Pentekote, Alikuja kukaa ndani ya waume kwa wake.

Yohana Mbatizaji

Luka 1:15 Kwa kuwa atakuwa mkuu mbele za Bwana, na kamwe hatakunywa mvinyo wala kinywaji kikali. Na pia atajazwa na Roho Mtakatifu, hata tangu tumboni mwa mamaye.

Elizabeti

Luka 1:41 Na ikafanyika, wakati alisikia salamu za Maria, ikawa mtoto akaruka tumboni mwake; na Elizabeti akajazwa na Roho Mtakatifu.

Zakaria

Luka 1:67 Naye baba yake Zakaria alijazwa na Roho Mtakatifu, na akatoa unabii ...

KAZI YA ROHO MTAKATIFU KATIKA MAISHA NA HUDUMA YA YESU

Yesu alikuja kwa Roho

Matayo 1:20,24 Lakini alipowaza juu ya mambo haya, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, "Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukuwa Maria kama mkeo, kwa kuwa kilicho tumboni mwake ni kwa Roho Mtakatifu."

Yesu kwa kuzaliwa kwake kwa bikira, alikuwa mwanadamu kamili na pia alikuwa Mungu kamili. Yeye kuwa mwanadamu haikumzusha katika sifa kama Mungu.

Yesu aliacha Haki Zake

Yesu kwa kupenda aliweka kando haki Zake na faida kama Mungu alipokuwa hai hapa duniani. Alikuja kama "Adamu wa Mwisho" ili kutimiza yote ambayo alimwumba mwanadamu kutenda hapa duniani alipomwumba Adamu wa kwanza.

Wafilipi 2:5-8 Acheni na akili hii iwe ndani yenu ambayo pia ilikuwa juu ya Kristo Yesu, Ambaye, katika umbo la Mungu, hakuona kuwa unyang'anyi kuwa sawa na Mungu, lakini akajifanya asiye na heshima, kuchukua mfano wa mtumwa, na kuja katika mfano wa wanadamu. Na kuonekana kama mwanadamu, alinyenyekea na kuwa mtiifu hadi kufa, hata mauti msalabani.

Yesu alipakwa na Roho

Huduma ya Yesu haikuanza hadi alipobatizwa katika maji na Roho Mtakatifu akaja kumtia nguvu na kukaa ndani Yake. Yote ambayo Yesu alifanya katika maisha Yake na huduma kutoka wakati huo na kuendelea, alifanya kama mwanadamu aliyetiwa nguvu na Roho Mtakatifu. Huu ulikuwa mpango na mbinu kwa wanadamu alipowaumba.

Matayo 3:16,17 Kisha Yesu, alipobatizwa, akatoka majini mara moja; na lo, mbingu zikafunguka kwake, Naye akaona Roho wa Mungu akishuka kama njiwa na kukaa juu Yake. Na punde sauti ikatoka mbinguni, ikisema, "Huyu ndiye Mwanangu mpendwa, nimependezwa Naye."

Mariko 1:10 Kwa haraka, akitoka katika maji, aliona mbingu zikifunguka na Roho akishuka juu Yake kama njiwa.

➢ *Kuongozwa na Roho*

Kwa kujifunza juu ya kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha na huduma ya Yesu, tunaweza kuelewa kazi ya Roho Mtakatifu maishani mwetu na huduma leo. Yesu ni mfano wetu kweli.

Matayo 4:1 Kisha Yesu akaongozwa na Roho hadi jangwani ili kujaribiwa na ibilisi.

Mariko 1:12 Na mara Roho akamwongoza hadi jangwani.

Luka 4:1 Kisha Yesu, akiwa amejazwa na Roho Mtakatifu, alirejea kutoka Yordani na kuongozwa na Roho hadi jangwani ...

➢ *Kufundishwa na Roho*

Matendo 1:2 Hadi siku ile alipochukuliwa juu, baada ya Yeye kupitia Roho Mtakatifu alitoa amri kwa mitume aliowachagua ...

Yohana 14:10 Je, hamukuamini kuwa niko ndani ya Baba, naye Baba yu ndani yangu? Maneno ninayonena nanyi sineni kwa mamlaka yangu mwenyewe; bali Baba aliye ndani yangu hutenda kazi.

➢ *Kupakwa na Roho*

Luka 4:18 Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa kuwa amenipaka ili kuhubiri injili kwa maskini. Amenituma kuwaponya waliovunjika mioyo, kuhubiri ukombozi kwa watumwa na kuwafanya vipofu kuweza kuona, kuwapa uhuru wanaoteseka.

➢ *Kukemea Mapepo kwa Roho*

Matayo 12:28 Lakini nikiwakemea pepo kwa Roho wa Mungu, kwa kweli ufalme wa Mungu umekuja juu yenu.

➢ *Kutolewa kwa Roho*

Waebrania 9:14 Je, ni mangapi zaidi damu ya Kristo, ambaye kupitia Roho wa milele alijitolea Yeye bila dosari kwa Mungu,

akaunganisha fikira zako kutoka kazi ya mauti hadi kumtumikia Mungu?

➢ *Kufufuka katika Roho*

Warumi 1:4 Na kutangazwa kuwa Mwana wa Mungu katika nguvu, kulingana na Roho wa utakatifu, katika ufufuo kutoka kwa wafu ...

Warumi 8:11 Lakini ikiwa Roho wa Yule aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu yu juu yenu, Yeye aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu pia atawapa uhai mili yenu ikufayo kupitia Roho Wake aliye ndani yenu.

ROHO MTAKATIFU NI NGUVU ZA MUNGU

Kama vile Yesu aliitaji nguvu za Roho Mtakatifu maishani Mwake, nasi pia ni sharti tupokee nguvu hiyo ya Roho Mtakatifu kikamilifu maishani mwetu!

Nguvu ya Ufufuo

Waefeso 1:19,20 Je, nguvu Yake ya juu kwetu tunaoamini, kulingana na utenda kazi wa nguvu yake ya juu ambayo alifanya katika Kristo alipomfufua kutoka kwa wafu na akaketi mkono Wake wa kuume mbinguni ...

Nguvu katika Paulo

1 Wakorintho 2:4,5 Na hotuba yangu na mahubiri yangu haikuwa na maneno ya kuvutia ya hekima ya mwanadamu, bali ni katika utenda kazi wa Roho na nguvu, kuwa imani yako isiwe katika hekima ya wanadamu bali ni katika nguvu za Mungu.

Warumi 15:17-19 Kwa hivyo ninayo sababu ya kutukuza katika Kristo Yesu katika mambo ya Mungu. Kwa kuwa sitanena juu ya kitu chochote ambacho Kristo hajakamilisha akinitumia, kwa maneno na matendo, kuwafanya mataifa kutii-katika ishara kuu na miujiza, kwa nguvu za Roho wa Mungu, ili kutoka Yerusalemu na karibu na Iluriko, nimeihubiri injili ya Yesu kikamilifu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Andika, kwa maneno yako mwenyewe, Roho Mtakatifu ni nani.

2. Je, Yesu alitumika vipi alipokuwa hapa duniani kufuatia ubatizo Wake wa maji na Roho Mtakatifu kuja kuishi ndani Yake?

3. Je, tunatakiwa kutumika vipi?

Somo la Pili

Kupokea Nguvu za Roho Mtakatifu

Ahadi ya Kwanza

Yoeli 2:28,29 Na itatimika baadaye kuwa nitamwaya Roho Wangu juu ya viumbe wote; wazee wenu wataota ndoto, vijana wenu wataona maono; na pia juu ya watumwa wangu nitamwaga Roho Wangu siku zile.

Isaya 28:11,12 Kwa kuwa katika kigugumizi na ndimi nyingine Atawanenea watu, ambao atawaambia "Hii ndiyo utatumia kuwawezesha waliochoka kupata pumziko," na, "Hii inafurahisha;" lakini hawatasikia.

KUAHIDIA KATIKA AGANO JIPYA

Na Yesu

➢ *Nguvu kutoka Juu*

Luka 24:49 Tazama, natuma Ahadi ya Baba Yangu juu yenu; lakini subirini mjini Yerusalemu hadi mpate nguvu kutoka juu.

➢ *Na Roho Mtakatifu na Moto*

Matayo 3:11 Kwa kweli nawabatiza kwa maji katika toba, lakini Yeye ajaye nyuma yangu ni mkuu kwangu, ambaye kiatu chake sifai kukibeba. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na moto.

➢ *Zawadi Nzuri*

Luka 11:9-13 Na nawaambia, uliza, na mtapewa; tafuta, nanyi mtapata; bisha, na mtafunguliwa. Kwa kuwa yeyote aulizaye hupokea, naye atafutaye hupata, na kwa yule abishaye hufunguliwa.

Je, mwana akiuliza mkate kutoka kwa baba yeyote hapa, atampa jiwe? Au ikiwa atauliza samaki, atampa nyoka badala ya samaki? Au ikiwa atauliza yai atapewa nzige?

Ikiwa basi, mkiwa waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, basi ni kiasi gani zaidi Baba wenu wa mbinguni kutoa Roho Mtakatifu kwa wale wanaomwuliza!

➢ *Mito ya Maji ya Uzima*

Yohana 7:37-39 Siku ya mwisho, siku hiyo kuu ya pasaka, Yesu akasima na kupasa sauti, akisema, "Ikiwa yeyote ana kiu, hebu na aje Kwangu na anywe. Yeye aniaminiye, Maandiko yanasema, ndani ya moyo wake mito ya maji ya uzima itatoka." Lakini haya alinena kuhusu Roho, ambaye wale wamwaminiye watapokea; kwa kuwa Roho Mtakatifu hakuwa ametolewa, kwa kuwa Yesu hakuwa amepewa utukufu.

Na Petro

Matendo 2:38,39 Kisha Petro akawaambia, "Tubu, na kila mmoja wenu abatizwe katika jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi; nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi ni yenu na watoto wenu, na wote walio mbali, wengi ambao Bwana Mungu wetu ataita."

JE, ANAYEBATIZA NI NANI?

Kumekuwa na kutokuelewa tofauti kati ya kazi ya Roho Mtakatifu katika kubatiza kila mwamini katika mwili wa Yesu Kristo wakati wa wokovu na kazi ya Yesu katika kuwabatiza waamini "katika" au "na" Roho Mtakatifu.

Kufafanua Ubatizo

Neno "batiza" badala ya kutafsiri katika lugha yetu limetungwa kutokana na neno lisikikalo kama Kigiriki ya asili lililotumika na waandishi. Hakika, ina maana, "kukubaliana na kuzamishwa kabisa." Wakati vazi linapakwa rangi, huwa tofauti kabisa na hutambulika na rangi hiyo. Linabatizwa ndani ya rangi hiyo.

Roho Mtakatifu alitutambulisha kikamilifu na Yesu Kristo wakati wa wokovu. Ubatizo wa maji, ambao umeamuriwa na Mungu kwa kila mwamini ni picha au ushuhuda mbele ya wanadamu kuwa tumetambulishwa na Yesu katika mauti Yake, maziko na ufufuo. Lakini, Yesu anapotubatiza katika Roho Mtakatifu, pia tunatambulishwa kabisa na Roho Mtakatifu. Tunapokea nguvu za Roho Mtakatifu maishani mwetu.

Roho Mtakatifu kama Mbatizaji

Wakati wa wokovu, Roho Mtakatifu humbatiza kila mwamini katika Yesu Kristo. Tunafanyika wa karibu na kuunganika na Yesu. Tunakuwa washirika wa Mwili wake.

Warumi 6:3 Wala haukujua kuwa wengi wetu tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti Yake?

Wagalatia 3:27 Kwa kuwa wengi kama walivyobatizwa katika Kristo wamevishwa Kristo.

1 Wakorintho 12:13 Kwa kuwa kwa roho mmoja sote tulibatizwa katika mwili mmoja – iwe Myahudi au Mgiriki, awe mtumwa au huru-na wote wamefanywa wanywe katika Roho mmoja.

Waefeso 5:30 Kwa kuwa sote tu washirika wa mwili mmoja, wa mwili Wake na mifupa Yake.

Yesu kama Mbatizaji

Kama kazi tofauti na ustadi, Maandiko huweka wazi kuwa Yesu anataka tubatize katika Roho Mtakatifu.

Kutabiriwa na Yohana

Luka 3:16 Yohana akajibu, akiwaambia wote, "Kwa kweli nawabatiza kwa maji; lakini Yeye ajaye nyuma yangu ni mkuu kwangu, ambaye kiatu chake sifai kukibeba. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na moto."

Iliamuriwa na Yesu

Matendo 1:4,5 Na kwa kukusanyika pamoja nao, Aliwaamuru wasiondoke Yerusalemu, bali wasubiri Ahadi ya Baba, "ambaye," Alisema, "mmesikia kutoka kwangu; kwa kuwa Yohana kweli alibatiza kwa maji, lakini mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu siku chache kutoka sasa."

Matendo 1:8 "Lakini mtapokea nguvu Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu; na mtakuwa mashahidi wangu Yerusalemu, na kote Yudea na Samaria, na hadi mwisho wa dunia."

Iliahidiwa na Petro

Matendo 2:38 Kisha Petro akawambia, "Tubuni, na kila mmoja wenu abatizwe katika jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi; na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

AHADI KUPOKELEWA

Na Wayahudi Siku ya Pentekote

Matendo 2:1-4 Sasa siku ya Pentekote ilipowadia kabisa, wote walikuwa katika chumba kwa nia sawa. Na ghafla pakatokea sauti kutoka mbinguni, kama wimbi kali, na ikajaza chumba chote walikoketi. Kisha pakatokea miale, kama ya moto, na kila moja ikikaa juu ya kila mmoja wao. Na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu na kuanza kunena katika ndimi tofauti, wakiongozwa na Roho.

Matendo 2:15,16 Wala hawa hawajalewa, kama mnavyodhania, kwa kuwa ni mapema ya saa tatu tu. Lakini hii ilinenwa na nabii Yoeli ...

Kumekuwa na mafundisho kuwa hii ilikuwa ni tukio la mora moja tu. Lakini, baada ya Roho Mtakatifu kuja juu ya waamini katika chumba cha juu, baada ya kilema kuponywa katika langoNzuri, baada ya Anania na Safira kufa, baada ya wazee kuchaguliwa, baada ya Stefano kupigwa kwa mawe na usaliti kuwa wazi, ni nakili kuwa waamini wanabatizwa katika Roho Mtakatifu.

Na Mataifa Katika Samaria

Filipo alienda kwa Wasamaria na mwamsho ukatokea. Samaria ilipokea neno la Mungu na kisha Petro na Yohana wakaja.

Matendo 8:14-17 Na sasa mitume waliokuwa Yerusalemu waliposikia kuwa Samaria ilipokea neno la Mungu, waliwatuma Petro na Yohana kwao, amabo walipofika, waliwaombea ili kupokea Roho Mtakatifu. Kwa kuwa hakuwa amejazwa juu ya yeyote. Walikuwa tu wamebatizwa katika jina la Bwana Yesu. Kisha wakawawekelea mikono, na wakapokea Roho Mtakatifu.

Na Mataifa Kaisaria

Ili tusifikiri kuwa Roho Mtakatifu alikuja juu ya Wayahudi kama tukio la mara moja tu, tunapewa maelezo kuhusu waamini katika Kaisaria.

Matendo 10:44-46a Petro alipokuwa angali akinena maneno haya, Roho Mtakatifu akaja juu ya wote waliolisikia neno. Na wale wa tohara walioamini walishangazwa, hata kwa wote waliokuja na Petro, kwa kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu alimwagwa juu ya mataifa pia. Kwa kuwa waliwasikia wakinena katika ndimi wakimtukuza Mungu.

Matendo 11:15 Na nilipoanza kunena, Roho Mtakatifu akaja juu yao, kama juu yetu hapo mwanzo.

Kwa Mataifa Efeso

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulifanyika kama miaka 33 AD (Ussher's date). Kuelekea mwisho wa kitabu cha Matendo, kama miaka 54 AD, Paulo alikuja Efeso.

Matendo 19:2-6 Akawaambia, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?"

Nao wakamwambia, "Wala hatujasikia kuwa kuna Roho Mtakatifu."

Na kisha akawaambia, "basi mlibatizwa ndani ya nini?"

Kisha wakasema, "katika ubatizo wa Yohana."

Kisha Paulo akasema, "Yohana kwa kweli alibatiza katika ubatizo wa toba, akiwaambia watu kuwa wanatakiwa kumwamini Yeye atakayekuja baada yake, ambaye, ni Kristo Yesu."

Waliposikia haya, walibatizwa katika jina la Bwana Yesu. Naye Paulo alipowawekelea mikono, Roho Mtakatifu alikuja juu yao, nao wakanena katika ndimi huku wakitoa unabii.

MAFUNDISHO YA PAULO JUU YA ROHO MTAKATIFU

Je, Mlipokea?

Matendo 19:2a Akawaambia, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?"

Hili lilikuwa swali la kwanza Paulo aliwauliza waamini walipofika Efeso. Alijua kuwa kila mwamini aliitaji nguvu ya Roho Mtakatifu ili kufanyika shahidi bora.

Jibu lao lilikuwa kawaida kama Wakristo wengi leo.

Matendo 19:2b,6 Nao wakamwambia, "Wala hatujasikia kuwa kuna Roho Mtakatifu."

Naye Paulo alipowawekelea mikono, Roho Mtakatifu alikuja juu yao, nao wakanena katika ndimi huku wakitoa unabii.

Huu ulikuwa mwanzo wa kipindi cha injili iliyo kuu kihistoria katika mkoa wa Asia! Matokeo ya waamini kuwa na nguvu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu katika maisha yao ulikuwa mwanzo wa uvuvio wa miujiza ya kiinjili.

Matendo 19:10 Na haya yakaendelea kwa miaka miwili, ili wote walioko Asia walisikia neno la Bwana Yesu, Wayahudi na Wagiriki.

KUPOKEA ROHO MTAKATIFU LEO

Kwa Kila Mtu

Yesu alisema tutapokea nguvu Roho Mtakatifu akija.

Matendo 1:8 "Lakini mtapokea nguvu Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu ..."

Petro alisema kuwa kila mtu atapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

Matendo 2:38 Kisha Petro akawambia, "Tubuni, na kila mmoja wenu abatizwe katika jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi; na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

Kipawa Kizuri

Tunatakiwa kutamani kila kipawa kizuri ambacho Baba anatoa kwetu.

Luka 11:11-13 Je, mwana akiuliza mkate kutoka kwa babaye yeyote hapa, atampa jiwe? Au ikiwa atauliza samaki, atampa nyoka badala ya samaki? Au ikiwa atauliza yai atapewa nzige?

Ikiwa basi, mkiwa waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, basi ni kiasi gani zaidi Baba wenu wa mbinguni kutoa Roho Mtakatifu kwa wale wanaomwuliza!

Ili kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu tunatakiwa tu kuuliza, na kisha kupokea kwa imani!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Wakati Yesu alizungumza juu ya kuja kwa Roho Mtakatifu, je alitumia maneno gani akieleza haya?

2. Je, mtu hupokea vipi ubatizo wa Roho Mtakatifu kulingana na Neno la Mungu?

3. Eleza tofauti kati ya ubatizo “wa” Roho Mtakatifu na ubatizo “ndani” ya au “na” Roho Mtakatifu.

4. Je, ubainifu upi umeandikwa katika Agano Jipya kama ushahidi ambao hufuatia ustadi wa kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu?

Somo la Tatu

Kunena Katika Ndimi

Usizuie

Je, si ni jambo lisilo kawaida kuwa kipawa cha pekee cha Roho Mtakatifu ambacho tumeambiwa tusizuie, hupingwa na makundi mengi sana leo? Ni kama Paulo hakuandika,

1 Wakorintho 14:39 Kwa hiyo, wezangu, tamanini sana kutoa unabii, na msipinge kunena katika ndimi.

Je, kwa nini kuna utofauti sana kuhusu kipawa cha ndimi? Je, kwa nini kipawa chochote cha Roho Mtakatifu hukataliwa na kupuuzwa?

Je, inawezekana kuwa kipawa cha ndimi ni roho wetu akiomba moja kwa moja kwa Mungu – roho wetu akimpa sifa – fikira zetu zikifanywa upya kama vile mtume Paulo alivyosema?

Lakini, Shetani, atajaribu kupinga chochote chenye nguvu kiasi hii. Kipawa cha ndimi ni ushahidi wa mtu aliyepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ni mlango wa kuishi katika hali isiyo ya kawaida ambayo ni wazi kwa kila mwamini.

USHAHIDI WA KUPOKEA UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU

Katika Siku ya Pentekote

Wakati waamini hupokea ubatizo ndani ya Roho Mtakatifu na hapo kujazwa na Roho Mtakatifu, wao huanza kunena katika ndimi zisizo kawaida huku Roho akiwapa usemi. Hii ndiyo ilifanyika katika Siku ya Pentekote.

Matendo 2:4 Na wote walijazwa na Roho Mtakatifu na kuanza kunena katika ndimi, huku Roho akiwapa usemi.

Mataifa ya Kaisaria

Mara nyingi, wakati ufunuo wa nguvu za Mungu katika Roho Mtakatifu hushirikishwa kwa watu, upako unakuwa mkubwa kuwa Roho Mtakatifu "huanguka" juu yao na huanza kunena katika ndimi na kumwinua Mungu.

Matendo 10:44-46a Petro alipokuwa angali akinena maneno haya, Roho Mtakatifu akaja juu ya wote waliolisikia neno. Na wale wa tohara walioamini walishangazwa, hata kwa wote waliokuja na Petro, kwa kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu alimwagwa juu ya mataifa pia. Kwa kuwa waliwasikia wakinena katika ndimi wakimtukuza Mungu.

Paulo Akiwa Efeso

Mara nyingi watu hupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu wakati mikono ya waamini waliobatizwa na Roho huwekelewa juu yao. Mara nyingi, hawaanzi tu kunena katika ndimi bali hata vipawa vingine vya Roho Mtakatifu huanza kufanya kazi maishani mwao.

Matendo 19:2,6 Akawaambia, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?"

Nao wakamwambia, "Wala hatujasikia kuwa kuna Roho Mtakatifu."

Naye Paulo alipowawekelea mikono, Roho Mtakatifu alikuja juu yao, nao wakanena katika ndimi huku wakitoa unabii.

Paulo Alinena katika Ndimi

Paulo alishukuru na kugundua umuhimu wa kunena katika ndimi kila mara na kwa muda mrefu. Ikiwa mtume Paulo aliitajika kunena katika ndimi kila mara, je, mara ngapi zaidi tunaitaji wenyewe maishani mwetu?

1 Wakorintho 14:18 Ninamshukuru Mungu kuwa ninanena katika ndimi zaidi yenu wote ...

Ndimi Aina Mbili ya Msingi

➢ *Ya Wanadamu na Malaika*

Tunaponena katika ndimi za wanadamu, tunanena katika mojawapo ya lugha ya ulimwengu huu. Lakini Paulo pia alisema kuwa ananena katika ndimi ambazo malaika pia hunena, lugha ya kimbinguni.

1 Wakorintho 13:1a Hata kama nanena katika ndimi ya wanadamu na malaika ...

Mara nyingi tunapoonyesha upendo wetu kwa Mungu wakati wa sifa na ibada za kibinafsi, tunaishiwa na maneno katika lugha yetu ya mwanadamu kuweka mioyo yetu kwa Mungu. Baada ya kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, tunaweza, kama Paulo, anza kunena katika lugha mpya ya kimbinguni, lugha isiyo na mwisho wa misamiati yetu, lugha hiyo hiyo ambayo malaika wanatumia kumwabudu Mungu, mchana na usiku mbele ya kiti cha enzi.

JE, NINI HUFANYIKA TUNAPONENA KATIKA NDIMI?

Roho Yetu Huomba

Tunapoomba katika ndimi, roho yetu huomba katika kudhihirishwa kusio kawaida kwa Roho Mtakatifu. Fikira zetu hazina matunda.

1 Wakorintho 14:14 Kwa kuwa nikiomba katika ndimi, roho yangu huomba, lakini fikira zangu hazina matunda.

Hutangaza Kazi ya Mungu

Wakati waamini waliobatizwa na Roho hunena katika ndimi, wao huleta sifa kwa Mungu kwa kunena juu ya kazi Yake ya ajabu.

Matendo 2:11 Wakiriti na Warabu–tunawasikia wakinena katika ndimi zetu kazi ya Mungu ya ajabu.

Roho Huombeza

Ninapoomba katika ndimi, mawazo hayaji akilini mwangu, wala hayajapimwa kwa kuelewa kwangu tu. Bali Roho Mtakatifu anaomba kupitia roho wa mwanadamu kwa Baba.

Waefeso 6:18 Kuomba wakati wote kwa maombi yote ya maitaji katika Roho, hata kukesha hadi hapa kwa uvumilivu wote na maitaji kwa watakatifu wote.

Warumi 8:26,27 Vivyo hivyo Roho pia hutusaidia katika unyonge wetu. Kwa kuwa hatujui tuombee nini inavyotakiwa, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kilio kisichoweza kuelezwa. Na sasa yeye atafutaye katika mioyo hutambua kile mawazo ya Roho, kwa kuwa huombeza kwa ajili ya watakatifu kulingana na mapenzi ya Mungu.

ROHO MTAKATIFU HUWEZESHA

Tunapopokea ubatizo katika Roho Mtakatifu, tunatakiwa kuanza kunena! Roho Mtakatifu atakupa usemi katika mwito. Hatuwezi kunena lugha mbili wakati mmoja. Tunatakiwa kunena katika lugha yetu ya mbinguni. Hatutakiwi kufikiria katika lugha hii kwa kuwa "ufahamu wetu hauna matunda" tunaponena katika ndimi. Basi, tutanena nini?

Walianza Kunena

Matendo 2:4 Na wote walijazwa na Roho Mtakatifu na kuanza kunena katika ndimi, huku Roho akiwapa usemi.

Tunaanza Kunena

Lugha zote zimetungwa kwa maneno yatokanayo na sauti. Ikiwa Roho atatupa uwezo au usemi, kama katika Siku ya Pentekote, tunaanza kunena lakini sio katika lugha tunayoifahamu. Sisi, kama waamini wa awali lazima tuanze kunena kwa sauti. Tunapoanza kuyaweka mawazo yetu kwa Yesu, baada ya kuuliza na kupokea ubatizo katika Roho Mtakatifu kwa imani, lazima tuanze kunena. Itakuwa sisi tunaonena, kama walivyofanya Siku ya Pentekote. Roho Mtakatifu atatupa uwezo.

Mito ya Maji

Lugha ambayo itaanza kutiririka kutoka kwetu itakuwa kama “mito ya maji ya uzima” ikitiririka kutoka ndani yetu.

Hata wakati Mungu aliyafanya maji kuwa ngumu chini ya miguu ya Petro alipotoka nje ya chombo na kuanza kutembea juu ya maji, Roho Mtakatifu atafanya sauti kuwa “ngumu” chini ya vilimi vyetu tunapoanza kwa ujasiri kunena kwa sauti.

KUPOKEA UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU

Omba Ombi Hili

Baba wa Mbinguni,

Nakushukuru kwa kipawa cha Wokovu!

Lakini Baba, Nataka kila kipawa ulicho nacho kwangu. Nataka kipawa chako cha Roho Mtakatifu! Nataka nguvu Zake maishani mwangu!

Yesu, nakuuliza unibatize katika Roho Mtakatifu! Napokea kipawa hiki kwa imani!

Sasa hivi, Baba, nainua mikono yangu kwako nikisifu. Nafungua kinywa changu wazi na nitaanza kukusifu, lakini si kwa lugha yoyote ninayofahamu.

Kama vile katika siku ya Pentekote, ninaanza kunena. Na ninapofanya hivyo, ninakushukuru Baba, kuwa Roho Mtakatifu atanipa uwezo wa kufanya hivyo!

Maagizo Yaonekanayo

Sasa, mikono yako ikiinuliwa katika sifa kwa Mungu, anza kumsifu Yeye. Anza kunena kwa sauti katika ndimi. Mito ya maji ya uzima inaanza kutiririka kutoka kwako, wakati Roho Mtakatifu anakupa usemi na uvuvio.

Endelea kumwabudu na kumsifu Mungu kwa sauti katika lugha yako mpya ya mbinguni hadi kuachiliwe mtiririko wa sifa kwa Mungu.

Hebu na atoke ndani yako katika roho yako.

Hebu na sauti yako iunganike na sauti ya malaika katika sifa na kuabudu kwa Mungu.

KUSUDI LA LUGHA YA KIMBINGUNI

Sifa

➢ *Kuimba katika Roho*

Tunapoimba katika roho, Roho Mtakatifu hutupa sio tu sauti, bali pia hutupa wimbo. Anza kumwabudu Mungu sasa kwa kuimba katika lugha ya kimbinguni.

1 Wakorintho 14:15 Je, majibu yake ni gani basi? Nitaomba katika roho, na pia nitaomba kwa ufahamu. Nitaimba na roho, na pia nitaimba kwa ufahamu.

Lugha yetu ya "mbinguni" au "maombi" ni kupitia roho yetu hadi kwa Mungu. Kipawa cha ndimi, na kipawa kiambatanacho nayo cha utafsiri, ni Mungu akinena na mwanadamu.

Maombi

Huenda tusijue jinsi ya kumwombea mtu fulani au hali. Tunapoanza kuombeza katika ndimi, Roho Mtakatifu huomba kupitia roho yetu zaidi ya fikira zetu. Tutakuwa tukiomba tukikubaliana na mapenzi ya Mungu!

Tunaposifu na kumwabudu Mungu na kuombeza kila siku bila kukoma katika lugha yetu mpya, nguvu kuu itaendelea kutiririka nje ya maisha yetu. Tunapoomba na kusifu katika roho, mito ya maji ya uzima itaendelea kutiririka. Tutaendelea kujengeka kiimani kwa kuomba katika Roho.

Yude 1:20 Lakini ninyi, wapendwa, mkijijenga katika imani takatifu, mkiomba katika Roho Mtakatifu ...

Ishara kwa Wasioamini

Mungu anatamani kulihakikisha Neno Lake tunaposhiriki injili katika hali isiyo kawaida ya kunena katika ndimi. Tusijaribu kuficha au kuhisi kuwa wasioamini watakasirika iwapo tutanena katika ndimi. Ni ishara kutoka kwa Mungu kutumiwa wazi na waamini.

1 Wakorintho 14:22a Kwa hiyo ndimi ni za ishara, sio kwa waaminio bali kwa wasioamini ...

➢ *Mfano katika Pentekote*

Matendo 2:4,5 Na wote walijazwa na Roho Mtakatifu na kuanza kunena katika ndimi, huku Roho akiwapa usemi. Na palikuwa wakaazi Yerusalemu Wayahudi, watu waliojitolea, kutoka kila taifa chini ya mbingu.

Kipawa cha ndimi ni ishara kwa asiye mwamini, wanasilikiza, hushangaa na kisha kuamini.

➢ *Kuvutia Umati*

ms. 6-8 Na wakati sauti hii ilikuja, umati ukaja pamoja na kushangaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakinena katika lugha yao. Nao wote wapigwa na mshangao na kuambiana, wakisema, "Tazama, si hawa watu wote waongeao Kigalilaya? Na inakuwaje tunawasikia, kila mmoja katika lugha yetu wenyewe ya kuzaliwa?"

➢ *Kutangaza Miujiza ya Mungu*

ms. 9-12 "Wapathi na Wamedi na Waelamiti, wale waishio Mesopotamia, Yuda na Cappadocia, Pontus na Asia, Phrygia na Pamphylia, Misri na sehemu ya Libya ikishikana na Sirene, wageni kutoka Roma, wakiwemo Wayahudi na wengine, Wakiriti na Warabu–tunawasikia wakinena katika lugha yetu maajabu ya Mungu." Kwa hivyo wakashangaa sana na kushtuka, wakiambiana, "Je, hii ina maana gani?"

➢ *Kunena katika Lugha Isiyo ya Kawaida*

Yesu alisema kuwa kunena katika ndimi itakuwa mojawapo ya ishara zitakazowafuata wakati "watahubiri" injili. Kama ilivyofanyika katika Siku ya Pentekote, ambayo mara nyingi haijulikani kwa yule anenaye katika ndimi, wananena katika lugha ijulikanayo kwa yule anayewasikiliza akinena. Kuna mifano mingi ya haya kutendeka leo. Kila mara ni ishara isiyo ya kawaida kwa waamini ambayo itawaongoza kupokea ujumbe wa Injili.

Hali Isiyo ya Kawaida

Kunena katika ndimi ni mojawapo ya ishara na miujiza ambayo Yesu anarejesha kwa kanisa Lake leo. Ni ya kila mwamini! Leo kama katika siku za kanisa la awali, ni ushahidi kuwa umepokea ubatizo katika Roho Mtakatifu. Ni ishara isiyo ya kawaida kwa wasio waamini.

Si lazima tuwe na hisia au kujaribu kuigiza " isiyo kawaida" tunaponena katika ndimi. Tunaweza kuongea kwa sauti au kwa upole, haraka au polepole, tukioongozwa na Roho Mtakatifu. Achilia kipawa cha ndimi kitiririke kwa hali isiyo ya kawaida na katika hali ya kawaida.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza sehemu yetu dhidi ya sehemu ya Mungu kwa kunena katika ndimi ya hali isiyo kawaida.

2. Je, kunena katika ndimi ni tukio la mara moja, au kila wakati katika maisha ya mwamini?

3. Je, tutaweza kujali kuwakasirisha wasioamini wanapotusikia tukinena katika ndimi?

Somo la Nne

Sanaa Muhimu za Huduma

Utangulizi

Vipawa vya Roho Mtakatifu huleta njia mpya kabisa ya kuishi kwa ajili ya mwamini aliyejazwa na roho. Kama vile Petro alipotoka chomboni na kutembea juu ya maji, inatupasa kupiga hatua kutoka kwa hali nzuri ya kawaida na kutembea juu ya "maji ya kiroho." Tunatakiwa kuishi katika roho na kutenda katika vipawa Vyake vyote tisa maishani mwetu kila siku.

1 Samueli 10:6 Roho wa Mungu atakuja juu yako kwa nguvu, na utatoa unabii nao; na utabadilishwa na kuwa mtu tofauti.

SANAA ZA WAAMINI WOTE

Ufahamu

Ni muhimu kuwa waamini wote waelewe na kufahamu jinsi ya kutenda katika vipawa vyote vya Roho Mtakatifu. Paulo alituambia haya mwanzo wa mafundisho haya juu ya vipawa vya Roho Mtakatifu.

1 Wakorintho 12:1 Na sasa kuhusu vipawa vya kiroho, wenzangu, sitaki muwe wa kupuuza.

Mlango kwa ajili ya Vipawa

Ubatizo katika Roho Mtakatifu ni mlango wa kuingia katika vipawa hivi. Tunaitajika kuanza kutenda katika vipawa vya Roho Mtakatifu mara tu baada ya kupokea ubatizo katika Roho Mtakatifu. Nguvu za Roho Mtakatifu zimekuja juu yetu wakati huo na ni lazima tuanze kuachilia nguvu hizo kupitia mojawapo ya njia ya Roho Mtakatifu.

Yoeli 2:28 Na itatimika baadaye kuwa nitamwaya Roho Wangu juu ya viumbe wote; wazee wenu wataota ndoto, vijana wenu wataona maono.

Matendo 1:8 "Lakini mtapokea nguvu Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu; na mtakuwa mashahidi wangu Yerusalemu, na kote Yudea na Samaria, na hadi mwisho wa dunia."

Vipawa vya Kiroho Tisa

1 Wakorintho 12:4-10 Na sasa kuna vipawa tofauti, lakini Roho ni yule yule. Kuna huduma mbalimbali, lakini Bwana mmoja. Na kuna vitendo tofauti tofauti, lakini ni Mungu yule yule atendaye yote ndani ya yote.

Lakini Roho hutolewa kwa kila mmoja ili kuwafaidi wote:

Kwa kuwa kwa mmoja amepewa neno la hekima katika Roho, kwa mwingine neno la maarifa kupitia Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji wa miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi.

Kumbuka: Biblia *NIV* inatumia neno "kubainisha katika ya roho." Kwa kuwa hii inaeleweka zaidi kwa kueleza juu ya kubainisha juu ya roho, tutaitumia katika mafunzo haya.

VIPAWA VYOTE KWA KILA MWAMINI

Katika msitari wa saba, vipawa vya Roho vimeitwa vipawa vionekanavyo. Vyote hupewa kila aaminiye kwa ajili ya mema ya kawaida. Kwa mwamini kushindwa kutenda katika mojawapo ya vipawa hivi vya Roho Mtakatifu itakuwa ni kukosa kile ambacho "kinafaidi wote." Mwamini huyo atakuwa amekosea matokeo ya muhimu ya kukua kiroho na huduma bora ambayo Mungu alipanga katika maisha yake.

1 Wakorintho 12:7 Lakini Roho hutolewa kwa kila mmoja ili kuwafaidi wote ...

Jumla ya Huduma ya Mwili Wote

Paulo alipofundisha kuhusu vipaji vya Roho Mtakatifu katika 1 Wakorintho, alikuwa pia akizungumzia kazi ya vipawa katika mkutano kanisani. Katika 1 Wakorintho 11, alijadili mavazi bora kanisani na kisha mwisho wa kifungu mtazamo ulio bora katika kupokea Meza ya Bwana.

Kumekuwa na kutokuelewa kuhusu utumizi wa maneno katika msitari wa nane "kwa mmoja amepewa" na "kwa mwingine." Kwa matumizi ya maneno haya, tumefundishwa kuwa kila mmoja anatakiwa kutenda katika kipawa kimoja tu, au labda mbili. Mafundisho haya yanakosea.

Paulo alikuwa akifundisha jinsi vipawa vinatakiwa kufanya kazi katika mkutano kanisani. Mmoja asienende katika vipawa vyote kwa kila mkutano. Mkutano wa kanisa ni kwa ajili ya huduma ya mwili. Mmoja ataenenda katika kipawa hiki, mwingine katika kikingine.

Tunapokuwa waangalifu katika Roho Mtakatifu, kila mwamini anaweza kuwahudumia washirika wengine kupitia vipawa vya Roho Mtakatifu. Sote tu wa maana kwa kila mmoja tunaporuhusu vipawa vya Roho Mtakatifu kutiririka.

1 Wakorintho 12:11,12 Lakini mmoja na ni yule atendaye haya yote, akitoa kwa kila mmoja kadri apendavyo. Kwa kuwa kama vile mwili ni mmoja nao una sehemu nyingi, lakini sehemu zote

ni za mwili huo mmoja, zikiwa nyingi, ni mwili mmoja, naye pia alivyo Kristo.

Tafuteni Vipawa Kujenga Kanisa

Tunatakiwa kutafuta vipawa vya kiroho sio kwa ajili ya kujiinua, bali tuwe sehemu ya kuinua mwili wa Kristo.

1 Wakorintho 14:12 Hata pia wewe, kwa kuwa unatamani vipawa vya kiroho, hebu na iwe kwa ajili ya kuinua kanisa ambapo unatafuta kuinua.

Gundua utumizi wa neno "vipawa" katika wingi.

Vipawa vyote ni kwa ajili ya kuinua mwili wote wa Kristo, sio tu kumwinua mtu mmoja katika ubora.

Kila mwamini anayo huduma. Waamini wengine wameitwa na Mungu katika huduma-tano (Mtume, Nabii, Mwalimu, Mwinjilisti au Mchungaji). Vile vipawa tisa vya kiroho vinaweza kufanya kazi zaidi kupitia waamini hawa wamejiweka wazi na kumruhusu Roho Mtakatifu atiririke katika njia hii. Wanapoanza kufanya kazi zaidi katika sehemu moja kuliko nyingine, vipawa hivi vinaweza kuonekana katika huduma zao.

Kila mwamini anatakiwa kuenenda katika vipawa vyote. Wasiwe na hofu kuonekana wapumbavu. Lazima wawe tayari kutoka na kuhadharisha katika kufanya makosa. Hiyo ndiyo njia ya pekee ya kujifunza.

Kati wanafunzi wote, Petro tu ndiye aliyetembea juu ya maji. Ni yeye tu aliyekuwa tayari kuhadharisha kupiga hatua nje ya chombo.

Vivyo hivyo Tamanini Vipawa Vikuu

1 Wakorintho 12:31 Lakini kabisa tamanini vipawa bora. Na basi niwaonyeshe njia bora zaidi.

Vipawa vikuu kwa kila mwamini kupata kikitenda kazi kwa ubora zaidi maishani mwao ni vile vinavyoitajika katika kila hali ili kutimiza huduma waliyopewa na Mungu.

MIFANO YA KUMTAFUTA MUNGU KWA KWELI

Mfano wa Yakobo

Mwanzo 32:24-30 Kisha Yakobo akaachwa peke yake; na Mtu akapigana naye wakimenyana hadi kucha. Naye alipoona kuwa hatamshinda, akamgusa kwenye kiungo katika pacha lake; nayo sehemu hiyo ikawa imetoka katika nafasi yake. Akasema, "Niache niende, kwa kuwa kumekucha."

Lakini alisema, "Sitakuachilia hadi unibariki!"

Basi akamwambia, "Jina lako nani?"

Naye akasema, "Yakobo."

Naye akasema, "Jina lako halitakuwa tena Yakobo, bali Israeli; kwa kuwa umemenyana na Mungu na wanadamu, nawe umeshinda."

Kisha Yakobo akamwuliza Yeye, akisema, Niambie jina lako, nakuomba."

Naye akamwambia, "Kwa nini unauliza kuhusu jina Langu?"

Naye akambariki hapo. Naye Yakobo akaita jina la pale Penieli: "Kwa kuwa nimeona Mungu uso kwa uso, na maisha yangu yameokolewa."

Yesu Anaeleza Msemo

➢ *Kuuliza Mkate*

Luka 11:5-13 Naye akawambia, "Nani kati yenu atakuwa na rafikiye, na amwendee usiku akimwambia 'Rafiki, niazime mikate mitatu; kwa kuwa rafiki yangu amefika kwangu akiwa safarini, na sina chochote kuweka mbele yake'; naye atamjibu akiwa ndani akisema, 'Usinisumbue; mlango sasa umefungwa, na wanangu wako nami kitandani; siwezi kuamka na kukupatia'?

"Nawaambia, hata kama hatainuka na kumpa kwa kuwa ni rafikiye, lakini kwa kutokukata tamaa ataamuka na kumpatia yote atakayoitaji.

➢ *Uliza, Tafuta, Bisha*

"Na nawaambia, uliza, na mtapewa; tafuta, nanyi mtapata; bisha, na mtafunguliwa. Kwa kuwa yeyote aulizaye hupokea, naye atafutaye hupata, na kwa yule abishaye atafunguliwa.

Je, mwana akiuliza mkate kutoka kwa baba yeyote hapa, atampa jiwe? Au ikiwa atauliza samaki, atampa nyoka badala ya samaki? Au ikiwa atauliza yai atapewa nzige?

Ikiwa basi, mkiwa waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, basi ni kiasi gani zaidi Baba wenu wa mbinguni kutoa Roho Mtakatifu kwa wale wanaomwuliza!"

Chochea Kipawa

2 Timotheo 1:6 Kwa hiyo nakukumbusha kuchochea kipawa cha Mungu kilicho ndani yako kwa kuwekelea mikono.

JIWEKE KWA MUNGU

Jipeleke Mwenyewe

Warumi 6:13 Nanyi msiweke miili yenu kama vyombo visivyo na haki kwa dhambi, bali jiwekeni kwa Mungu kama mlio hai kutoka wafu, na sehemu zenu kama vyombo vya haki kwa Mungu.

Warumi 12:1 Nawasihi basi, wenzangu, kwa rehema zake Mungu, kuwa mlete mili yenu kama dhabihu iliyo hai, takatifu, inayokubalika kwa Mungu, ambayo ni kazi bora iliyokubalika.

Ingia Katika Ulimwengu wa Kiroho

Kama waamini waliojazwa, hatutakiwi kuenenda katika hali yetu ya awali. Tunaitajika kuishi katika hali isiyo ya kawaida, katika ulimwengu wa Roho Mtakatifu. Tunapoishi katika Roho, tutaendelea kuwa waangalifu Kwake. Tutakuwa katika hali isiyo ya kawaida. Utenda kazi wa vipawa vya kiroho itakuwa sehemu ya maisha yetu kila siku.

1 Wakorintho 2:14 Lakini mtu wa asili hawezi kupokea vitu vya Roho wa Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake; wala hawezi kuvijua, kwa kuwa vinaonekana tu katika roho.

Wagalatia 5:25 Ikiwa tutaishi katika Roho, hebu na tutembee katika Roho.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Orodhesha vipawa tisa vya Roho Mtakatifu

2. Kwa kuwa vipawa vya Roho Mtakatifu hupewa kila aaminiye kuwafaidi wote, kwa nini vipawa vingine huonekana wazi vikifanya kazi katika waamini fulani?

3. Kwa nini tutamani “vipawa vikuu” ambavyo hasa ni muhimu kwa kutimiza huduma ambayo Mungu ametuitia?

Somo la Tano

Vipawa Kutengwa na Kufafanua

Ukumbusho kwa Mwalimu: Kwa somo hili unatakiwa kutayarisha mifano kutoka maisha yako binafsi kuonyesha utenda kazi wa vipaji vya Roho Mtakatifu, na kisha uwahimize wanafunzi kushiriki vipawa vionekanavyo maishani mwao. Hii itaonyesha utenda kazi na tofauti ya vipawa wazi na kueleweka.

MAANDIKO TISA KUZUNGUZIA VIPAWA VYA KIROHO

1 Wakorintho 12:1 Na sasa kuhusu vipawa vya kiroho, wenzangu, sitaki muwe wa kupuuza ...

1 Wakorintho 13:2 Na hata nikiwa na kipawa cha unabii, na kuelewa miujiza na ufahamu wote, na hata nikiwa na imani yote, hata niweze kuhamisha milima, na nikose upendo, mimi si kitu.

1 Wakorintho 14:1,12 Tafuta upendo, na tamanini vipawa vya kiroho, hata kuweza kutoa unabii.

Hata hivyo wewe, kwa kuwa unatamani vipawa vya kiroho, hebu na iwe kwa ajili ya kuliinua kanisa ambalo unatafuta kuinua.

2 Timotheo 1:6 Kwa hivyo nawakumbusha kuchochea kipawa cha Mungu kilicho ndani yako kupitia kukuwekelea mikono yangu.

Waeburania 2:4 Mungu pia akiwa shahidi katika ishara na miujiza, kwa miujiza mingi, na vipawa vya Roho Mtakatifu, kulingana na mapenzi Yake mwenyewe.

1 Petro 4:10 Kwa kuwa kila mmoja amepokea kipawa, hudumianeni ninyi kwa ninyi, kama walinzi wazuri katika neema ya Mungu.

Warumi 1:11 Kwa kuwa natamani kuwaona, ili niweze kuwawekea ndani yenu vipawa vya kiroho, ili muweze kuimarishwa.

Mithali 18:16 Kipawa cha mtu huleta nafasi ndani yake, na humleta mbele ya watu wenye sifa.

VIPAWA TISA VYA ROHO

Vipawa tisa vya Roho ni sehemu ambazo Roho Mtakatifu hudhihirisha Uwepo Wake. Ni vionyesho vya neema ya Mungu ikiwa kazini ulimwenguni sasa. Vinaonyesha nguvu za Mungu zikihudumu kwa ajili ya wema wa mwanadamu.

1 Wakorintho 12:7-10 Lakini Roho hutolewa kwa kila mmoja ili kuwafaidi wote:

Kwa kuwa kwa mmoja amepewa neno la hekima katika Roho, kwa mwingine neno la maarifa kupitia Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi.

Vipawa kwa Kila Mmoja

Mungu hakukusudia watu wakae hapa duniani bila kuwa sehemeu ya ulimwengu wa kiroho. Kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu, wamepewa kila kipawa wanachoitaji to kushinda vita vya dunia hii.

- ➢ Mungu ni Roho.
- ➢ Shetani ni roho.
- ➢ Mwanadamu ni roho.

Waefeso 6:12 Kwa kuwa hatushindani dhidi ya mwili na damu, bali dhidi ya ngome, dhidi ya nguvu, dhidi ya utawala wa giza la nyakati hizi, dhidi ya wenye maovu kiroho katika mbingu.

Vipawa vya Roho Mtakatifu vimetolewa kwetu ili kutumia. Sio "vyombo vya ushindi" kwa ajili ya uaminifu wetu. Vipawa ni sanaa na humtayarisha mwamini kwa ajili ya vita maishani.

MAKUNDI MATATU AU VITENGO

<u>Vipawa vya Kutia Moyo – Kunena</u>

Ndimi
Kutafsiri Ndimi
Unabii

<u>Vipawa vya Ufunuo – Kusikiliza</u>

Kubainisha Kati ya Roho
Neno la Ufahamu
Neno la Hekima

<u>Vipawa vya Nguvu – Kutenda</u>

Kipawa cha Imani
Vipawa vya Uponyaji
Kutenda Miujiza

VIPAWA VYA UNENAJI ULIOVUVIWA

Vipawa vya kwanza tatu ambavyo tutajifunza ni vipawa vya kunena au vipawa vya unenaji uliovuviwa. Hii ni Roho Mtakatifu akinena nasi, kupitia sisi.

Vipawa vya unenaji viliovuviwa hupatikana wakati Mungu anaponena na waamini. Wakati waamini wanaenenda katika vipawa hivi wengine hutiwa nguvu, wanatiwa moyo au kutulizwa. Wakati Mungu ataleta marekebisho, hataleta lawama kupitia vipawa hivi.

Ndimi

Vipawa vya ndimi ni usemi usio kawaida kutokana na uvuvio unaoletwa na Roho Mtakatifu kwa kutumia sanaa za kawaida za sauti.

Ni lugha ambayo mnenaji hajawai kujifunza, wala kueleweka na akili za mnenaji.

Lugha inayozungumzwa inaweza kuwa ya kimbinguni inayotumika na malaika, au lugha ya wanadamu.

Vipawa vya ndimi vinaweza kueleweka na msikilizaji katika lugha yake.

Kufafanua

Kipawa cha kufafanua ndimi huonekana kwa Roho na hueleza au kutoa maana ya usemi wa ujumbe katika ndimi nyingine.

Hii sio utenda kazi, wala kuelewa, kwa akili. Imetolewa na Roho wa Mungu.

Kufafanua maana yake, kueleza wazi, au kufunua wazi. Sio kwa maneno yenyewe, neno kwa neno, tafsiri.

Unabii

Kipawa cha unabii hutokea ghafla, usemi usio kawaida uonyeshao uvuvio katika ndimi ijulikanayo ambayo hutia nguvu, kuhimiza, na kutia moyo mwili wa Kristo.

Ni ujumbe ulio wazi kutoka kwa Mungu kwa mtu fulani, au kundi la watu.

VIPAWA VYA UFUNUO

Vipawa vya ufunuo ni Mungu akidhihirisha roho, ufahamu, au hekima kwa watu Wake kwa ajili ya hali fulani. Vipawa hivi vinaweza kutolewa kwetu kupitia ndimi na kufafanua au kipawa cha unabii. Vinaweza kutolewa kwetu kupitia ndoto, maono, au ufahamu wa ndani.

Kubainisha Kati ya Roho

Kubainisha kati ya roho ni ufahamu wa ndani katika ulimwengu wa roho. Huonyesha aina ya roho, juu ya mtu, hali, kitendo au ujumbe.

Sehemu tatu za roho katika kubainisha ni:

- ➢ Ya Mungu – Mungu na malaika Wake
- ➢ Kutoka kwa Shetani – Shetani na mapepo
- ➢ Roho wa mwanadamu – mwili, au mtu wa kawaida

Neno la Ufahamu

Neno la ufahamu ni ufunuo usio kawaida na Roho Mtakatifu kwa ajili ya kweli fulani, sasa au iliyopita, kuhusu mtu au hali, ambazo hazikufunzwa kupitia akili ya kawaida. Kipawa hiki hutoa habari kutoka kwa Mungu ambayo haingefahamika kwa kawaida.

Kipawa hiki ni neno, sehemu, sio picha nzima, sio ufahamu kamili wa Mungu juu ya jamboa fulani. Hii hushughulikia mamabo yenyewe hasa. Hutuonyesha jinsi mambo yalivyo sasa.

Neno la Hekima

Neno la hekima ni ufunuo usio kawaida wa Roho Mtakatifu kumpa mwamini hekima ya Mungu jinsi ya kuendelea katika njia fulani ili kutenda kwa kawaida, au isiyo kawaida, ufahamu. Hudhihirisha mpango wa Mungu na kusudi maishani mwetu na huduma. Hudhihirisha kile Mungu angependa kifanyike haraka, kwa muda mfupi, au hivi karibuni au siku za usoni. Hudhihirisha kile mtu au mkusanyiko wa makundi wanatakiwa kufanya na jinsi ya kuendelea katika mapenzi ya Mungu. Neno la hekima mara nyingi hutendeka pamoja na neno la ufahamu.

VIPAWA VYA NGUVU

Vipawa vya nguvu ni Mungu akiachilia nguvu Zake kutiririka ndani yetu. Hii Mungu akitenda kitu kupitia ndani yetu!

- ➢ Mungu hunena nasi – vipawa vya usemi
- ➢ Yeye hudhihirisha mambo kwetu – vipawa vya ufunuo.
- ➢ Huachilia nguvu Zake zifanye kazi – vipawa vya nguvu

Kipawa cha Imani

Kipawa cha imani ni imani isio kawaida kwa ajili ya muda na kusudi fulani. Ni kipawa cha nguvu ili kutimiza kazi fulani katika hali yoyote wakati fulani.

Kutenda Miujiza

Kutenda miujiza ni kuingilia kusio kawaida katika njia ya kawaida. Hii ni kutenda kazi katika nguvu za Mungu ambazo sheria za kiasili hubadilishwa, hutupiliwa mbali au kuelekezwa kwa muda.

Kutenda miujiza hali ya kusimamisha kwa muda na kuahirisha mpango wa kawaida unaofuatwa katika kutenda nguvu za Mungu katika hali isio kawaida.

Vipawa vya Uponyaji

Vipawa vya uponyaji ni kiingilio cha nguvu za uponyaji wa Mungu kwa watu. Hii huelezwa kama nguvu za (wingi) kwa kuwa kuna njia nyingi za kuingiza, au kuhudumu uponyaji kwa mgonjwa.

Ni utenda kazi usio kawaida wa Roho Mtakatifu na si sawa na sayansi ya kimatibabu.

MTAFUTENI ATOAYE-VIPAWA NA PIA VIPAWA

Njaa na Kiu

Matayo 5:6 Wamebarikiwa wale wenye njaa na kiu kwa ajili ya haki, kwa kuwa wao watajazwa.

Tafuta Fikira za Roho

Warumi 8:5,6 Kwa kuwa wale wanaoishi kufuatana na matakwa ya mwili, hutawaliwa na fikira za mwili. Lakini wale wanaoishi kufuatana na matakwa ya Roho Mtakatifu, hutawaliwa na fikira za Roho.

Fikira za mwili huleta kifo; fikira za Roho huleta uzima na amani.

Warumi 8:13,14 Kwa maana, mkiishi kufuatana na mwili mtakufa; lakini mkiishi kwa Roho mnayaua matendo yenu maovu, basi mtaishi. Kwa kuwa wengi wanaoongozw na Roho wa Mungu, hawa ni wana wa Mungu.

Kupokea Ubainifu

1 Wakorintho 12:7 Lakini Roho hutolewa kwa kila mmoja ili kuwafaidi wote:

Yohana 14:12 Amini Amini, nawaambia, yeye aniaminiye, kazi ninayofanya atafanya pia yeye; na kazi nyingi zaidi kuliko hii yeye atafanya, kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu.

2 Timotheo 1:6 Kwa hivyo nakukumbusha kuchochea kipawa cha Mungu kilicho ndani yako kupitia kukuwekelea mikono yangu.

Endelea, lindeni vipawa vyote vya Roho vilivyochochewa ndani yako!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Orodhesha na kueleza kila mojawapo ya vipawa vya uvuvio vya usemi.

2. Orodhesha na kueleza kila mojawapo ya vipawa vya ufunuo.

3. Orodhesha na kueleza kila mojawapo ya vipawa vya nguvu.

Somo la Sita

Vipawa vya Utumainifu wa Usemi
Ndimi na Kufafanua

1 Wakorintho 12:8-10 Kwa kuwa Roho humpa mmoja ujumbe wa hekima, na mwingine neno la maarifa kupitia Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji wa miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi.

Utumainifu wa Usemi	*Vipawa Tisa vya Roho Mtakatifu*	**Nguvu**
➥ **Ndimi**	**Ufunuo**	Kipawa cha Imani
➥ **Kufafanua Ndimi**	Kutofautisha kati ya Roho	Vipawa vya Uponyaji
Unabii	Neno la Ufahamu	Utendakazi wa Miujiza
	Neno la Hekima	

VIPAWA VYA NDIMI – KUFAFANUA – UNABII

Utangulizi

Vipawa vya utumainifu wa usemi hubainika Mungu anaponena kwa hali isiyo kawaida kwa waamini. Waamini wanapoenenda katika vipawa hivi, wengine hutiwa nguvu, kuhimizwa na kutiwa moyo. Ingawa Mungu anaweza kuleta marekebisho, Yeye hatawai leta lawama kupitia vipawa hivi.

1 Wakorintho 14:3 Lakini yeye atoaye unabii hunena kujenga na kuinua na kuwatia moyo wanadamu.

Kutambua kuwa vipawa hivi hutegemea chombo cha mwanadamu anayenena, neno linalotolewa kamwe lisiangaliwe katika mamlaka sawa na Maandiko. Ni lazima kila mara lipimwe na kuchunguzwa kwa makini kubaini iwapo limetoka kwa Mungu.

1 Wakorintho 14:29 Hebu na nabii wawili au watatu wanene, na hebu wengine watoe hukumu.

Kwa Ajili wa Waamini

Kama tulivyojifunza katika somo la tatu, ubainifu wa ndimi ni kwa waamini wote wanapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Paulo aliwaamuru waamini waombe ili wapewe ufafanuzi.

1 Wakorintho 14:13 Kwa hivyo hebu na yule anenaye katika ndimi aombe kuwa atafafanua.

Paulo anasema kuwa kipawa cha unabii ni kwa ajili ya faida zaidi ya kipawa cha ndimi na kuwa mapenzi yake ilikuwa kwa unabii wote.

1 Wakorintho 14:5 Ningependa nyote mnene katika ndimi, lakini hata zaidi kuwa mtoe unabii; kwa kuwa yule atoaye unabii ni zaidi ya yule anenaye katika ndimi, hasa iwapo atafafanua, kuwa kanisa lipate kujengeka.

Wote inawapasa kunena katika ndimi. Wote inawapasa kuomba kuwa waweze kufafanua, lakini ni bora kutoa unabii. Kutokana na mafundisho haya ya Paulo tunaweza kusema kuwa vipawa vyote tatu vya utumainifu wa usemi ni vya kila mwamini.

KULINGANISHA VIPAWA VYA UTUMAINIFU WA USEMI

Ndimi na Ufafanuzi

Vipawa vya ndimi na kufafanua ndimi ni vipawa rahisi kabisa kufanya. Hupatikana kwa urahisi, na hivyo, huchukuliwa kimzaha mara nyingi.

Ujumbe lazima utolewe katika ndimi kwanza kabla mtu mwingine apokee ujumbe kutoka kwa Mungu kupitia kipawa cha kutafsiri. Kwa hivyo, vipawa vya ndimi na tafsiri yake huenda pamoja.

Ndimi na Unabii

Wakati mtu ananena katika lugha yao isiyo kawaida, yeye huongea miujiza kwa Mungu.

1 Wakorintho 14:2-5,39 Kwa kuwa yule anenaye katika ndimi haneni kwa wanadamu bali kwa Mungu, kwa kuwa hakuna amwelewaye; lakini, katika roho yeye hunena miujiza.

Wakati mtu hutoa unabii yeye huwasaidia waamini wengine.

v.3 Lakini yeye atoaye unabii hunena katika kujenga na kuinua na kuwatia moyo wanadamu.

Kunena katika ndimi hujenga, huinua, mwamini binafsi katika Roho. Kipawa cha unabii hujenga kanisa.

v. 4 Yeye anenaye katika ndimi hujiinua, lakini anayetoa unabii hujenga kanisa.

Unabii ni kubwa kwa kuwa moja kwa moja hujenga kanisa.

v.5 Ningependa nyote mnene katika ndimi, lakini zaidi kuwa mweze kutoa unabii; kwa kuwa yule atoaye unabii yu zaidi ya yuke anenaye katika ndimi, asipo kwa kweli kufafanua, kuwa kanisa liweze kupokea nguvu na kuinuliwa.

Neno “kanisa” limetumika mara tisa katika kifungu hiki kuashiria umuhimu wa utumizi wa vipawa kwa ajili ya kanisa.

Kwa nini Ndimi?
Kwa nini Unabii?

Kwa nini Mungu anene katika ndimi na kufafanua wakati fulani na kupitia kipawa cha unabii wakati mwingine?

1 Wakorintho 14:22 Kwa hivyo ndimi ni kwa ishara, si kwa wale wanaoamini bali wasioamini; lakini unabii si kwa wasioamini bali kwa wale waaminio.

Ndimi ni kwa ajili ya ishara kwa asiyeamini. Ufafanuzi wa ndimi ni ujumbe wa Mungu kwa mwili Wake.

Unabii ni kwa asiyeamini. Unabii unaitaji imani ya hali ya juu ili kutenda wakati ndimi haikutolewa kwanza kuachilia utumainifu wa kipawa hiki.

VIPAWA VYA NDIMI

Maelezo

Kipawa cha ndimi ni usemi usio kawaida uonyeshao uvuvio hutokana na Roho Mtakatifu kwa kutumia sauti ya kawaida. Ni lugha mnenanji hajawai jifunza, wala kufahamika kwa akili za mnenaji.

Ujumbe unaonenwa huenda iwe lugha ya mbinguni itumikayo na malaika, au lugha ya mwanadamu. Kipawa cha ndimi kinaweza kueleweka na msikilizaji.

Kuelewa Ndimi

Kipawa cha ndimi, mojawapo ya vipawa tisa vya kiroho, lazima vitofautishwe na utumainifu wa kunena katika ndimi ambayo ni lugha isiyo kawaida yenye kusifu na kuombeza ambayo mwamini hupokea anapobatizwa katika Roho Mtakatifu.

Katika kipawa cha ndimi, Mungu hunena na mwanadamu. Utumainifu wa lugha yetu ya maombi na sifa ni Roho Mtakatifu kupitia roho ya mwanadamu akinena kwa Mungu. Mojawapo hutoka kwa Mungu hadi kwa mwanadamu na ingine ni kutoka kwa mwanadamu hadi kwa Mungu.

Ndimi katika Utendaji

Wakati upako uko juu ya mtu naye atoe katika mkutano wa jumla, ujumbe katika ndimi ambayo haieleweki na watu, inatakiwa kufuatishwa na kipawa cha ufafanuzi wa ndimi.

1 Wakorintho 14:27 Iwapo yeyote atanena katika ndimi, hebu na kuwe na wawili au zaidi watatu, kila mmoja fursa yake, na kuwe na yule atakayefafanua.

Wakati kundi lote linaimba katika ndimi, ni wakati wa sifa kwa Mungu ambayo ni kwa Baba moja kwa moja. Hakuna tafsiri itakayoitajika kufuatia kipindi cha maombi. Ikiwa kuna watu katika kikundi wasioweza kuelewa kilichotendeka, basi na kuwe na ufafanuzi juu maana ya kuimba katika ndimi.

Penye Watu Wengi

Ujumbe unaweza kutolewa ambao haueleweki na mtu anayeutoa, lakini unaeleweka na mtu, au watu, walisimama maeneo ifikapo sauti.

Matendo 2:4-6 Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu na kuanza kunena katika ndimi kama alivyowawezesha Roho.

Sasa walikuwepo Yerusalemu Wayahudi-wamchao Mungu kutoka kila taifa chini ya mbingu. Waliposikia sauti hii, kundi likakusanyika kwa mshangao, kwa kuwa kila mmoja wao aliwasikia wakinena katika lugha yake mwenyewe.

Kusudi

Mungu anapenda kunena na watu Wake. Njia mojawapo Yeye hufanya hivyo ni kupitia utenda kazi wa kipawa cha ndimi pamoja na ufafanuzi wa ndimi.

MAAGIZO KWA UTUMIZI

Kuwa na Upako

Wakati Mungu anatamani kutoa ujumbe kwa mwili kupitia ndimi, mtu atakayetumiwa Naye kumpa ujumbe huo atagundua mwongozo wa Roho Mtakatifu akifanya hivyo. Mtu huyo atapata upako na kuashwa na Roho akiwa na wazo litokalo ndani kabisa kati ya roho yake atoe ujumbe katika ndimi wakati ufaao katika mkutano. Yeye asiingilie mpangilio wa mkutano, kile ambacho kinasemwa au kutendeka sasa, bali asubiri hadi wakati unaofaa. Kumbuka, Roho Mtakatifu hatajiingiza Mwenyewe.

Tambulika

Katika mikutano mikubwa ya waamini, ni bora kutambulika na uongozi kabla ya kutoa ujumbe. Biblia inasema “kuwatambua wale ambao wanatenda kazi kati yenu.” Ujumbe usitolewe kabla mtu fulani yuko pale kwa ajili ya kufafanua. La sivyo yule atoaye ujumbe katika ndimi atatazamiwa kutoa tafsiri.

Neno kwa Uwazi

Maneno yasiwe sauti kubwa, bali yanenwe vizuri kwa hisia sozote ambazo Roho atakuwezesha. Kwa mfano, wakati mwingine Roho atatoa ujumbe kwa ujasiri, au furaha. Base onyesha hisia unapotoa maneno.

Uwe na Ufafanuzi

Wakati ujumbe fulani umetolewa, lazima kuwe na kimya wakati waamini wanamsubiri Mungu atoe tafsiri kupitia kipawa cha ufafanuzi.

1 Wakorintho 14:19,28 Hata kanisani afadhali ninene maneno matano katika ufahamu wangu, ambayo naweza kuwafundisha wengine pia, kuliko maneno elfu katika ndimi.

Lakina pakiwa na mkalimani, hebu na anyamaze kanisani, naye anene mwenyewe kati yake na Mungu.

Ni Tatu Tu!

Paulo aliliagiza kanisa kuwa watu watatu wasiwe na jumbe tatu kila mmoja katika ndimi kwa mkutano wa kawaida.

1 Wakorintho 14:27 Iwapo yeyote atanena katika ndimi, hebu na kuwe na wawili au zaidi watatu, kila mmoja fursa yake, na kuwe na yule atakayefafanua.

Isizuiliwe

Kunena katika ndimi ni kipawa cha pekee tumeamuriwa tusizuie.

1 Wakorintho 14:39 Basi, wenzangu, tamaneni kutoa unabii, na msijizuie kunena katika ndimi.

Vipawa Vingine

Wakati kipawa cha ndimi kinafanya kazi, kipawa cha kufafanua na kutofautisha kati ya roho pia hutendeka. Hii itajadiliwa zaidi katika mafundisho juu ya vipawa hivi.

KIPAWA CHA KUTAFSIRI

Ufafanuzi

Kipawa cha kufafanua ndimi hudhihirishwa katika mwujiza na Roho wa kueleza, au maana, kwa lugha ya msikilaji mwenyewe, ya kuonyesha katika usemi wa ujumbe katika ndimi nyingine.

Hii sio utenda kazi, au ufahamu, wa akili. Hutolewa na Roho wa Mungu.

Tafsiri maana yake kueleza, kupanua, au kufunua. Hii si tafsiri ya neno kwa neno kabisa.

Mtu anayenena katika nchi ya kigeni huenda aitaji mtafsiri. Hii sio kipawa cha Roho, bali mtu anayeelewa na kuongea lugha mbili vizuri.

Sio kwa Urefu Sawa wa Maneno

Tafsiri huenda isiwe ndefu sawa na ujumbe wa awali katika ndimi kwa sababu mbili.

Hii sio tafsiri yenyewe. Ni kufafanua na huenda usichukue maneno mengi kutaja kile kimesemwa katika Roho, au ichukue maneno mengi zaidi.

Mtu anayetoa tafsiri anaweza kusonga na kuingia katika kipawa cha unabii. Mara nyingi kuna upako tofauti na unapogundua mwelekeo wa Roho Mtakatifu utajua tofauti.

Kusudi

Kipawa cha tafsiri kinalo kusudi moja kuu ambayo ni kufanya kipawa cha ndimi kieleweke na wasikilizaji ili kanisa lijue kile kimesemwa na liweze kujengeka.

UTENDA KAZI WA KIPAWA CHA TAFSIRI

Kati ya Umati

Sharia zile zile hutumika katika kipawa cha tafsiri pia hutumika katika kunena katika ndimi penye mikutano ya wengi. Roho Mtakatifu hatafanya kitu chochote kuleta utata au katika hali ya usumbuvu.

Mtu mmoja anaweza kunena ujumbe katika ndimi na kisha atoe tafsiri yeye mwenyewe.

Mtu mmoja anaweza kunena na mwingine atoe tafsiri.

Wakati mwingine mtu anaweza kuanza tafsiri na mwingine aichukue na kuimaliza. Hii hufanyika iwapo mtu huyo ni mgeni katika utenda kazi katika tafsiri na kuogopa anapotoka kwa imani. Kisha mtu aliye na ujuzi zaidi katika kipawa cha tafsiri anaweza kukamilisha ujumbe. Roho wa mashindano asiruhusiwe katika utenda kazi wa vipawa vya Roho. Kiburi cha kusema "Mimi naweza kutoa usemi mzuri kuliko huo" si wa Mungu.

Katika utenda kazi wa vipawa vya Roho, kila mara ni muhimu kuwa kipawa cha kutofautisha roho kitendeke. Wakati vipawa vinafanya kazi katika mkutano kwa uwazi, mtu aliye katika uongozi anatakiwa abaini roho ya kila kitendo na kukomesha chochote ambacho ni kinyume na Neno na/au Roho wa Mungu.

Ukiwa Binafsi

Paulo alitaja kuwa aliomba katika ndimi zaidi ya wengine, lakini aliendelea kusema kuwa katika ibada alinena katika unabii. Ikiwa hakunena katika ndimi kwenye ibada, basi lazima ailiandika kuhusu kunena katika ndimi akiwa peke yake.

Paulo pia anatuamuru kuomba kwa ajili ya kipawa cha tafsiri.

1 Wakorintho 14:13-15 Kwa hivyo hebu na yule anenaye katika ndimi aombe kuwa atafafanua. Kwa kuwa nikiomba katika ndimi, roho yangu huomba, lakini ufahamu wangu hauna

matunda. Je, basi majibu ni yapi? Nitaomba katika roho, na pia nitaomba katika ufahamu. Nitaimba na roho, na pia nitaimba katika ufahamu.

Tunapoomba katika ndimi tukiwa binafsi, tunaweza kuongozwa kumwuliza Mungu atupe tafsiri. Mara nyingi tunaposumbuka kwa ajili ya hali fulani na kuanza kuomba katika ndimi, tutaanza basi kuomba katika lugha yetu. Tunaweza kujikuta tukiomba vitu ambavyo hatuelewi, au kumwuliza Mungu ashughulikie shida kwa njia ambayo hatujaelewa awali. Hicho ni kipawa cha tafsiri ndimi itendekayo katika maisha ya maombi binafsi.

Si lazima tutafsiri kila kitu tunachoomba binafsi katika ndimi. Mara nyingi tunamsifu Mungu na hii haitaitaji tafsiri. Au, labda katika Roho tumekuwa tukiomba jibu lakini Mungu hataki jibu lidhihirishwe kwetu wakati huo huo.

1 Wakorintho 14:2 Kwa kuwa yule anenaye katika ndimi haneni kwa wanadamu bali kwa Mungu, kwa kuwa hakuna amwelewaye; lakini, katika roho yeye hunena miujiza.

Tunapoenenda katika kipawa cha tafsiri katika upweke, tunajitayarisha kutenda katika kipawa cha tafsiri mbele ya watu wengi.

KUPOKEA KIPAWA

Katika vipawa vyote vya Roho, mtu lazima awe katika uhusiano bora na Mungu ili kipawa kifanye kazi kwa uwazi.

Tumeamuriwa kumwuliza Baba kwa utenda kazi wa bure wa vipawa tunavyoitaji zaidi katika huduma yetu, kwa hivyo hatua ya kwanza ni kuuliza! Wakati tafsiri inakuja inaweza kuwa na maneno machache ya utangulizi, na mengine yatafuata tutakaponena maneno hayo kwa imani. Tunaweza kupata picha, ishara, au wazo. Wakati mwingine ujumbe hutolewa katika wimbo, na tafsiri inaweza kutolewa katika wimbo pia.

Jihadhari!

Mtu kamwe hatapewa tafsiri ya ndimi ambayo hulaani kwa kuwa laana inatoka kwa Shetani.

Mtu hatapewa tafsiri ambayo ni kinyume na Neno la Mungu.

Kuendelea kutoa tafsiri kamwe haitarekebisha kile mtu mwingine anayeenenda katika kipawa cha tafsiri ya ndimi amesema. Kiongozi, katika upendo, anaweza kuitajika kumkosoa mtu ambaye hakufuata katika Roho na kisha aulize, au atoe tafsiri ya kweli.

Roho Mtakatifu pia ametupatia kipawa cha kubainisha kati ya roho na ni muhimu sana kuwa kipawa hiki kifanyike wakati vipawa vya usemi vinatendeka. Tutajifunza haya zaidi katika somo juu ya kubainisha kati ya roho. Lakini, kwa sasa ni muhimu kuelewa kuwa kama vile tunatakiwa kuomba kwa ajili ya kipawa cha tafsiri wakati ujumbe unatolewa katika ndimi tunatakiwa kuomba kwa ajili ya kubainisha kati ya roho. Mungu hafanyi makosa kamwe, lakini sote tu wanadamu, na wanadamu hufanya makosa. Mungu ametoa kwa kila mmoja wetu jukumu la kutambua roho mgani tunayemsikiliza.

YESU NA VIPAWA VYA UTUMAINIFU

Yesu alitenda katika vipawa vyote vya Roho isipokuwa vipawa vya ndimi na kufafanua. Hatuna nakili ya hali ambapo vipawa hivi viwili vilitumika katika maisha Yake.

Jizoeshe

Ni muhimu kuwa tusitumie muda wetu kujifunza tu zile kweli. Ndimi na tafsiri yake inaweza tu kueleweka wakati zimeachiliwa kufanya kazi!

Wakati umefika mwisho wa somo hili ingia katika kipindi cha sifa na umruhusu Roho Mtakatifu atende akikutumia katika vipawa vya ndimi na tafsiri yake.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza katika maneno yako mwenyewe nini maana ya kipawa cha ndimi.

2. Eleza nini maana ya kipawa cha tafsiri.

3. Je, vipi unaweza kutoa ujumbe katika ndimi au tafsiri yake?

Somo la Saba

Kipawa cha Utumainifu Sauti
Kipawa cha Unabii

1 Wakorintho 12:8-10 Kwa kuwa Roho humpa mmoja ujumbe wa hekima, na mwingine neno la maarifa kupitia Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji wa miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi.

Utumainifu wa Sauti	*Vipawa Tisa vya Roho Mtakatifu*	**Nguvu**
Ndimi	**Ufunuo**	Kipawa cha Imani
Tafsiri ya Ndimi	Kutofautisha Kati ya Roho	Kipawa cha Uponyaji
➥ **Unabii**	Neno la Ufahamu	Kutenda Miujiza
	Neno la Hekima	

KIPAWA CHA UNABII

Ufafanuzi

Kipawa cha unabii hutokea ghafla, kwa usemi usiokawaida katika utumainifu kwa lugha ijulikanayo ambayo hutia nguvu, kuhimiza, na kuutia moyo mwili wa Kristo. Ni ujumbe utokao kwa Mungu moja kwa moja kwa mtu fulani au kundi la watu.

Neno la kigiriki la unabii ni "propheteia" maana yake kunena fikira na wasia wa Mungu.

Kusudi

Kusudi la kipawa cha unabii ni kutia nguvu, kuhimiza na kutia moyo.

1 Wakorintho 14:3 Lakini yeye atoaye unabii hunena kujenga na kuinua na kuwatia moyo wanadamu.

➢ *Kutia Nguvu au Kuinua*

Katika maana ya kimsingi, "kutia nguvu" au "kuinua" huashiria kusimamisha, au kujenga.

1 Wakorintho 14:4,5 Yeye anenaye katika ndimi hujiinua mwenyewe, lakini yeye atoaye unabii huinua kanisa. Ningependa kila mmoja wenu anene katika ndimi, lakini afadhali ningewaona mkitoa unabii. Yeye atoaye unabii ni mkubwa kwa yule anenaye katika ndimi, ikiwa atatafsiri, ili kanisa liweze kuinuliwa.

➢ *Kuhimiza au Kuinua*

Tafsiri ya neno "himiza" ni neno la Giriki maana yake kuitana karibu na Mungu. Kamusi inasema "kuhimiza" ni kutoa matumaini ya kweli, au kutoa ujasiri.

➢ *Kutia Moyo*

Kurejelea 1 Wakorintho 14:3 neno la Giriki, "paramuthia," maana ya kimsingi kunena kwa karibu na mtu, na huonyesha kutia moyo. Kamusi inasema "kutia moyo" ni kufanya nyepesi au kupunguza huzuni au shida, kubembejea, kuchekesha au kufurahisha.

UNABII NI

Sehemu ya Fikira za Mungu

Unabii ni sehemu ya fikira za mungu – wala si picha kamili.

1 Wakorintho 13:9 Kwa kuwa tunafahamu kwa sehemu na tunatoa unabii kwa sehemu.

Ni Kipawa Kikuu kati ya Vitatu

Unabii uko juu ya vipawa vya usemi vya utumainifu.

1 Wakorintho 14:1,5,39 Tafuta upendo, na utamani vipawa vya kiroho, hasa kuwa uweze kutoa unabii.

Ningependa nyote mnene katika ndimi, lakini zaidi kuwa mweze kutoa unabii; kwa kuwa yule atoaye unabii ni mkuu kwa yule anenaye katika ndimi, lakini afadhali ningewaona mkitoa unabii. Yeye atoaye unabii ni mkubwa kwa yule anenaye katika ndimi, ikiwa atatafsiri, ili kanisa liweze kuinuliwa.

Kwa hivyo, wapendwa, tamaneni sana kutoa unabii, na wala msijizuie kunena katika ndimi.

Ishara kwa Waamini

1 Wakorintho 14:24,25 Lakini wote wakitoa unabii, naye asiye mwamini au mtu asiyehamu aingie, yeye hukisia kwa wote, naye hupata hukumu na wote. Na basi siri za moyo wake hudhihirishwa; na kwa hivyo, huanguka kwa uso wake, atamwabudu Mungu na kutoa taarifa kuwa kwa kweli Mungu yu kati yenu.

Hubadilika

Yeremia 18:7,8 Punde tu ninaponena kuhusu taifa na kuhusu ufalme, kung'oa, kuvunja chini, na kuharibu, ikiwa taifa hilo ambalo dhidi yake nimenena linapogeuka kutoka kwa maovu yake, nitabadili juu ya maafa niliyodhani kuleta juu yake.

VIPAWA KUHUKUMIWA

Tahadhari!

Unabii ni kwa ajili ya kundi la watu fulani, kwa wakati fulani, kupitia mtu fulani. Haitakiwi kupewa uzito kama ule wa Neno la Mungu lililoandikwa.

Mtu, au watu, wakisikia unabii wanaweza kupea ujumbe mtazamo fulani tofauti na ule wanapea alichosema Roho wa Mungu.

Mtu atoaye unabii ni mwanadamu, na kwa hivyo ana makosa. Baadhi ya "unabii" hutolewa kutokana na fikira za kutamani, tamaa fulani au matakwa ya anayetoa, au hata kutokana na roho mwongo.

Mtu atoaye unabii katika mwili wa waamini lazima ajulikane kwa mwili huo wa waamini. Ikiwa mtu huyo ni mgeni kwa kundi hilo naye ajisikie anao unabii, basi na ajitambulishe na aombe kibali kwa kiongozi wa kikundi kabla hajanena.

Pima kwa Makini

Unabii, ndimi, na tafsiri ya ndimi vinatakiwa kupimwa kwa Neno na Roho.

Vipawa vya utumainifu wa usemi vinatakiwa kupimwa kwa makini na mtu, au watu, wanaosikia ujumbe.

1 Wakorintho 14:29-32 Hebu nabii wawili au watatu wanene, nao wengine waweze kupima. Na ikiwa chochote kitadhihirishwa kwa mwingine karibu, basi na yule wa kwanza anyamaze. Kwa kuwa nyote mnaweza kutoa unabii mmoja mmoja, ili wote wajifunze na wote wahimizwe. Na roho za unabii ziko china ya nabii wenyewe.

Hukumu

Paulo, ingawa ni mtume, aliwaamuru waupime ujumbe wake.

1 Wakorintho 10:15 Ninanena kama kwa watu wenye hekima; yapimeni wenyewe ninayosema.

MAJARIBIO SABA ILI KUFAFANUA UNABII, NDIMI NA TAFSIRI

Hukubaliana na Maandiko

"Neno" linenalwo na Mungu kamwe halitaweza kwenda kinyume na Neno Lake lililoandikwa. Mungu hayabadili mafundisho Yake. Tunatakiwa kupima chochote kionekanacho kipya kwa mafundisho yote juu ya somo katika maandiko. Hapatakuwa na utofauti.

Wagalatia 1:8 Lakini hata kama sisi, au malaika kutoka mbinguni, akiwahubiria injili nyingine yoyote kando na ile mmehubiriwa, basi na alaaniwe.

Matunda Katika Maisha ya Mtu

Ni kweli kuwa Mungu pekee ndiye anaweza kumhukumu mtu, lakini kila mmoja wetu inampasa kujua matunda ya wale tunapokea "kweli" kutoka kwao.

Matayo 7:15,16a Basi kuweni macho kwa manabii wa uongo, ambao huja wakiwa wamevalia mavasi ya kondoo, lakini ndani yao ni umbwa mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao.

Humtukuza Kristo

Je, ujumbe humtukuza Kristo? Je, ujumbe huleta utukufu kwa mtu ambaye hupokea ujumbe?

Yohana 16:13,14 Lakini, wakati Yeye, Roho wa kweli, akija, Atawaongoza katika kweli zote; kwa kuwa Yeye hatanena kwa mamlaka yake mwenyewe, bali chochote atakachosikia atanena; Naye atawambia mambo yatakayokuja. Yeye atanitukuza, kwa kuwa atachukuwa yaliyo yangu Naye atawatangazia ninyi.

Ufunuo 19:10b Kwa kuwa ushuhuda wa Yesu ni roho wa unabii.

Inapotimia

Ikiwa ujumbe umetoka kwa Mungu, utakuja kutimia. Labda, sio kwa nyakati zetu, lakini itatendeka.

Kumbukumbu 18:20-22 Lakini nabii anenaye neno katika jina Langu, ambalo sijamwamuru anene, au yule anenaye katika jina la miungu wengine, nabii huyo atakufa.

Na iwapo utasema moyoni mwako, `Je, tutajua vipi neno ambalo BWANA hajanena?' – wakati nabii ananena katika jina la BWANA, ikiwa mambo hayo hayatatendeka wala kutimia, basi kitu hicho BWANA hakunena; nabii amenena tu kwa kukizia; wala msimwogope."

Zakieli 12:25 "Kwa kuwa mimi ni BWANA. Ninenaye, nalo neno ninenalo litatimia; kamwe halitaahirishwa; kwa kuwa katika siku nne, ewe nyumba yenye uasi, nitalisema neno na kulitenda," asema Bwana Mungu.

Huongoza hadi kwa Mungu

Kuna nabii za uongo na kuna manabii wa uongo. Unabii kutoka kwa Mungu kila mara utatuongoza kwake. Ujumbe kutoka kwa Shetani utatuelekeza mbali na Mungu!

Kumbukumbu 13:1-3 Ikiwa patatokea kati yenu nabii au aotaye ndoto, naye awape ishara au mwujiza, nayo ishara au mwujiza aliowapa upate kutimia, ukisema, `Hebu na tuwafuate miungu wengine ambao hamkuwafahamu, nasi tuweze kuwatumikia,' msiyasikilize maneno ya nabii huyo au aotaye ndoto, kwa kuwa BWANA Mungu wenu anawajaribu kujua iwapo mnampenda

BWANA Mungu wenu kwa mioyo yenu yote na kwa nafsi zenu zote.

Huleta Uhuru

Ikiwa ujumbe utamfanya mtu anayetafuta kumtumikia Mungu kujihisi mnyonge, huzuni, au uzito katika roho zao, hiyo si kutoka kwa Mungu.

1 Wakorintho 14:3 Lakini yeye atoaye unabii hunena kujenga na kuinua na kuwatia moyo wanadamu.

Warumi 8:15 Kwa kuwa hamkupokea roho wa utumwa katika hofu, bali mlipokea Roho wa kupitishwa ambapo kwake tunalia, "Abba, Baba."

Shahidi wa Ndani

Tunaye Roho Mtakatifu ndani yetu na ikiwa tutajijunza kusikiliza, Yeye atatushuhudia ikiwa ujumbe unatoka kwa Mungu.

1 Yohana 2:20,27 Lakini mnao upako kutoka kwa Yule aliye Mtakatifu, na mnajua mambo yote.

Lakini upako mliopokea kutoka Kwake unakaa ndani yenu, na kuwa hamtaitaji kuwa yeyote awafundishe juu ya mambo haya, na ni kweli, na wala sio uongo, na kama vile amewafundisha, mtakaa ndani Yake.

Waefeso 1:17-19 Na kuwa Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, aweze kuwapa roho wa hekima na ufunuo katika ufahamu Wake, macho ya ufahamu wenu ipate nuru; ili mweze kujua nini tumaini la mwito Wake, ni utajiri wa utukufu wa urithi Wake katika watakatifu, na nini ukuu wa nguvu Zake kwa ajili yetu tunaoamini, kutokana na utenda kazi wa wa nguvu Zake kuu ...

UNABII WA KIBINAFSI

Ikiwa mtu atapokea "unabii wa kibinafsi," wanatakiwa kuupima kutumia zile hatua saba. Ni baada ya kutumia hatua hizi kupima ndipo ujumbe upokelewe katika roho zao kama neno la kweli kutoka kwa Bwana.

Hatua Saba za Kupima

- ➢ Je, inakubaliana na maandiko?
- ➢ Je, kuna matunda katika maisha ya mwamini?
- ➢ Je, inamtukuza Kristo?
- ➢ Je, huongoza kwa, au mbali na Mungu?
- ➢ Je, inaleta uhuru, au tutumwa?
- ➢ Je, ushahidi wa ndani wa Roho ni upi?
- ➢ Je, imetimia?

Kutumikia

Hasa katika sehemu ya unabii wa kibinafsi, mtu atambue unabii wa "kutumikia". Kwa maneno mengine, je, unabii unaleta kiburi kwa anayepokea.

"Wewe ni mpendwa wangu..."

"Nimekuita ufanye kitu ambacho hakuna mtu mwingine amewai fanya..."

Je, inamwinua atoaye katika mahali pema maalumu?

"Msikilize mwanamume/mwanamke huyu nimemtuma..."

Kuthibitisha

Je, ujumbe unathibitisha kile Bwana amesema tayari kwenu?

Ikiwa ujumbe ni kitu kigeni kabisa, nanyi mmepima roho na kujua kuwa mtu huyo ni wa Mungu, wekeni ujumbe huo katika roho zenu na msubiri kuthibitisha kutokana na njia nyingine, au kupitia mtu mwingine.

Zihukumuni

Nabii za binafsi zimetumika vibaya awali, lakini hii haimaanishi nabii za binafsi zitupiliwe mbali. Badala yake, chukua muda ufaao kuzipima na kuzipokea.

Ikiwa unabii ni tahadhari kuhusu hali fulani unayojihuzisha nayo au mtu unayejihuzisha naye au unawaza kujihuzisha naye, chukua muda na kuuombea uhusiano na umwulize Bwana akupe ufahamu zaidi katika sehemu hiyo.

Ni mazoea mazuri kuandika unabii chini ili uweze kuurejelea baadaye. Hii inaweza kuwa ya msaada katika kuhimiza na kupembejea, lakini tena, zisiwahi kuchukua nafasi ya Neno la Mungu.

KIPAWA CHA UNABII KULINGANISHWA NA MWITO WA NABII

Kipawa cha unabii si sawa na mwito katika ofisi ya unabii. Mungu alichagua huduma-tano.

Waefeso 4:11 Naye Mwenyewe aliwapa wengine kuwa mitume, wengine manabii, wengine wainjilisti, na wengine wachungaji na walimu ...

Huduma ya Kipawa cha Nabii

Kila mwamini ana fursa ya kuenenda katika kipawa cha unabii, lakini si kila mwamini anao mwito wa nabii.

1 Wakorintho 12:7,28,29 Lakini Roho hutolewa kwa kila mmoja ili kuwafaidi wote.

Naye Mungu ameweka hawa kanisani: kwanza mitume, pili manabii, tatu walimu, baada ya hawa miujiza, kisha vipawa vya uponyaji, misaada, usimamizi, ndimi mbalimbali.

Je, wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni walimu? Je, wote ni watenda miujiza?

Kwa mfano, mabinti wane wa Filipo walienenda katika kipawa cha unabii, lakini Mungu alimutuma Agabus kwa Paulo kama nabii ili kutoa unabii kwa Paulo.

Wote wanaweza Kutoa Unabii

1 Wakorintho 14:31 Kwa kuwa nyote unaweza kutoa unabii mmoja kwa mmoja, ili wote wajifunze na wote waweze kuhimizwa.

Hata kama kipawa cha unabii hutumika kupitia mtu hii haimaanishi wao ni manabii.

JE, KIPAWA CHA UNABII NI CHA SASA?

Neno la Mungu lilitabiri kuwa kutakuwepo unabii siku zetu.

Yoeli Aliandika

Yoeli 2:28 Na itatimika baadaye kuwa nitamwaga Roho Wangu juu ya viumbe wote; wazee wenu wataota ndoto, vijana wenu wataona maono ...

Petro Alisema

2 Petro 1:19 Nasi pia tunalo neno la unabii lenye uhakika zaidi, ambalo mnashika vizuri kama nuru inayong'aa gizani, hadi siku iche na nyota ya asubuhi iinuke mioyoni mwenu ...

Luka Alinakili

Matendo 2:16-18 Lakini hii ndiyo ilinenwa na nabii Yoeli: 'Na itatimia katika siku za mwisho, asema Mungu, Kuwa nitamwaga Roho Wangu juu ya miili yote; waume na mabinti wenu watatoa unabii, vijana wataona maono, wazee wenu wataota ndoto. Na kwa watumwa wangu wanaume na wanawake nitamwaga Roho Wangu siku hizo; nao watatoa unabii.'

Paulo Alieleza

1 Wakorintho 13:8-13 Upendo hauna kikomo. Pakiwa unabii utaisha; pakiwa ndimi, zitaisha; pakiwa ufahamu, itatoweka. Kwa kuwa tunafahamu kwa sehemu na kutoa unabii kwa sehemu. Lakini kile ambacho kimekamilika kinapowadia, basi kile kilicho kwa sehemu tu kitapotelea. Nilipokuwa mtoto, nilinena kama mtoto, nilielewa kama mtoto, niliwaza kama mtoto; lakini nilipokuwa mwanamume, niliweka mbali tabia za kitoto.

Kwa kuwa sasa tunaona katika kioo, hafifu, lakini tena uso kwa uso. Sasa ninajua kwa sehemu, lakini nitajua kama vile

ninavyojulikana. Na sasa inakaa imani, tumaini, upendo, hizi tatu; lakini kuu kati ya hizi ni upendo.

Hadi Iliyokamilika Kuwadia

Unabii utakuwa kanisani hadi "kile ambacho ni kikamilifu kimewadia."

Wengine wameshawishi kuwa maneno "wakati kile ambacho ni kikamilifu kimewadia" inazungumzia juu ya Maandiko yaliyokamilika, hapo basi wakieleza kuwa vipawa fulani vilikuwa vya muda hadi Maandiko yalipokamilika. Lakini, katika kifungu, tunaona kuwa maneno haya kwa wazi yanaashiria siku ambapo tutakuwa uso kwa uso na Yesu Kristo.

MAAGIZO YA MATUMIZI

Kipawa cha unabii ni tofauti na kipawa cha ndimi kwa kuwa hakitendeki tupendavyo. Tunaweza kupokea unabii tukiwa mahali peke yetu, au katika mkutano.

Kipawa cha unabii mara nyingi hufanyika wakati wa sifa na kuabudu, au kufuatia kipindi cha utendaji wa kipawa cha ndimi na tafsiri ya ndimi.

Ukiwa Peke Yako

Tunaweza kupokea unabii kuhusu kitu tumekuwa tukitafakari juu yake, au kuombea kwa ajili ya kujengeka wenyewe. Inaweza kuwa, au isiwe kitu ambacho tutashiriki tukiwa mbele ya watu.

Mbele ya Watu

➢ *Mtu Aongozaye*

Anayetoa unabii lazima achukue usukani kamili mwenyewe.

1 Wakorintho 14:32 Na roho za unabii ziko chini ya manabii.

➢ *Sauti ya Kawaida*

Unabii lazima utolewe katika sauti ya kawaida ila sauti ibadilishwe na Roho Mtakatifu kwa kutilia mkazo.

➢ *Lugha ya Kisasa*

Unabii kwa kawaida utolewe kwa njia rahisi, ya kisasa na maneno yanayoeleweka kwa urahisi. Usitumie maneno ya zamani yanayoweza kupotosha kutokana na urahisi wa ujumbe.

➢ *Bila Hisia Nyingi*

Unabii usitolewe katika hisia nyingi kwa kuwa hii huenda mbali na ujumbe. Isitolewe katika ukulele, bali utolewe katika sauti inayosikika vizuri.

➢ *Usiwe na Uoga Kurudia Rudia*

Mtu anayetoa unabii asiwe wa kurudia rudia maneno mara kwa mara. “Asema Bwana” mara nyingi hurudiwa kwa uoga. Ikiwa hakika ujumbe unatoka kwa Bwana, Roho Wake atalithibitisha ndani ya roho za wasikilizaji.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, kipawa cha unabii ni nini?

2. Pimanisha kipawa cha unabii na kile cha ndimi na tafsiri yake.

3. Je, nini majaribu saba ambayo tunatakiwa kutumia kupima iwapo ujumbe unatoka kwa Mungu?

Somo la Nane

Kipawa cha Ufunuo
Kutofautisha Kati ya Roho

1 Corinthians 12:8-10 Kwa kuwa Roho humpa mmoja ujumbe wa hekima, na mwingine neno la maarifa kupitia Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji wa miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi.

	Vipawa Tisa vya Roho Mtakatifu	
Utumainifu wa Sauti	**Ufunuo**	**Nguvu**
Ndimi	➥**Kutofautisha Kati ya Roho**	Kipawa cha Imani
Tafsiri ya Ndimi	Neno la Ufahamu	Kipawa cha Uponyaji
Unabii	Neno la Hekima	Kutenda Miujiza

VIPAWA VYA UFUNUO

Utangulizi

Vipawa vya ufunuo huonekana wakati Mungu anajitambulisha kwa hali isiyo kawaida, kawaida au kazi ya roho, au anapodhihirisha ufahamu au hekima kwa watu Wake. Ufunuo huu huja katika mawazo yetu kupitia roho zetu katika umbo la wazo, fikira, hisia, ndoto au maono. Vile vipawa tatu vya ufunuo ni kubainisha kati ya roho (au kutofautisha kati ya roho), neno la ufahamu, na neno la hekima.

Kama vile vipawa vya utumainifu wa usemi hufanya kazi pamoja, vipawa vya ufunuo hutiririka karibu kama moja. Tunazitenganisha katika somo hili kwa ajili ya kuzielewa. Tunapojifunza aina ya ubainifu wa Roho Mtakatifu, tunafanyika huru zaidi kuzipokea maishani mwetu.

Panaweza kuwa na utata akilini mwetu iwapo tunaenenda katika neno la hekima au neno la ufahamu, au kutofautisha kati ya roho. Mojawapo ya utata huo ni kuwa mara nyingi tunatenda katika zaidi moja ya vipawa hivi. Si lazima ujue ni kipawa kipi tunapokea. Tunaweza kuziachilia kwa rahisi zitiririke ndani yetu kadri Mungu apendavyo.

Kwa Mfano

Kipawa cha kutofautisha kati ya roho inaweza kutuweka macho kuwa mtu aliyekuja kwa ajili ya maombi ana roho wa pepo.

Kisha neno la hekima linaweza kutuambia wakati na jinsi ya kumhudumia mtu kwa ajili ya matokeo ya haraka.

KUBAINISHA KATI YA ROHO

Ufafanuzi

Kipawa cha kutofautisha kati ya roho ni mtazamo usio kawaida katika ulimwengu wa kiroho. Hii huweka wazi aina ya roho, au roho wengi, juu ya mtu, hali, kitendo au ujumbe. Ni kujua katika roho yako ambayo huja na ufunuo usiokawaida kuhusu chanzo, hali na kitendo cha roho yoyote.

Neno "kubainisha" katika Kigiriki maana yake ubaguzi wa wazi kabisa.

Sio

Hii sio "kipawa cha kubaini" – hakuna kipawa kama hicho kimetajwa katika Biblia. Biblia inagusia juu ya kipawa cha kubaini roho, wala sio kipawa cha ubaguzi. Ubaguzi ni kitendo cha hekima ya mwanadamu katika sehemu ya nafsi.

Kubainisha kati ya roho si kusoma akili, au kuingia kiakili, au mtazamo wa kisaikolojia. Sio kukosoa au tabia ya kuhukumu.

Kutofautisha kati ya roho sio kuchunguza tabia, au makosa.

Matayo 7:1 Msihukumu, nanyi hamtahukumiwa.

SEHEMU TATU YA KAZI YA ROHO

Tunapotenda katika kubaini kati ya roho, ni muhimu kuelewa kuwa kuna sehemu tatu ya kazi ya roho. Kubaini kati ya roho itafanyika katika sehemu hizi zote tatu, sio tu kwa roho wachafu. Hizi ni:

- ➢ Roho wa Mungu
- ➢ Roho wa Mwanadamu
- ➢ Ufalme wa Shetani

Roho wa Mungu

Roho wa Mungu hujumlisha malaika wake wa mbinguni ambao hutumwa kutufanyia vita na kuleta jumbe kwetu.

Roho wa Mwanadamu

Roho wa mwanadamu hufanya uamuzi kati ya Roho wa Mungu na ufalme wa Shetani au kuhusu mema na maovu. Kupitia njia ya kujihuzisha katika maisha na uamuzi, roho wa mwanadamu ataleta labda mambo ya Mungu au ya hali ya mwili.

Roho wa mwanadamu anaweza kuwa amejazwa na upendo wa Mungu na kwa hivyo aonyeshe usafi, na tabia ya upendo kupitia mtu, au inaweza kuwa mnafiki, mwongo na hasira, na kuleta chuki, tabia iliyo kinyume na binadamu na uchoyo.

Shetani na Mapepo

Kuna ufalme wa uovu wa Shetani na mapepo. Baadhi ya mifano ni roho wa tamaa, wivu, kiburi, uongo, uchawi na uasi.

KUSUDI LA KIPAWA CHA KUTOFAUTISHA KATI YA ROHO

Tunapotenda katika kipawa cha kutofautisha kati ya roho, tunaweza kuzijaribu roho huku tukitumia ndimi, tafsiri yake, au unabii. Katika ukombozi na uponyaji tunaweza kujua roho anayehusika.

Hatubainishi roho waovu tu, lakini pia roho wa mwanadamu, au uwepo wa viumbe wa kimalaika. Nyakati za mahitaji, mwamini anaweza kupewa wazo kali juu ya malaika au viumbe waovu.

Tukiwa na utenda kazi wa kubaini kati ya roho ndani ya mwili wa Kristo:

- watakatifu waliofungwa watakombolewa;
- mipango ya Shetani inaweza kubainishwa;
- dhambi inaweza kuwekwa mbali kati ya wateule;
- na ufunuo potovu unaweza kugundulika.

Umuhimu wa Kipawa

Vipawa vyote ni kwa ajili ya kusudi fulani na vitawafaidi wote. Lakini kumekuwa na mafundisho machache juu ya kubainisha kati ya roho kwa miaka mingi.

1 Yohana 4:1-3 Wapendwa, msiamini kila roho, bali pimeni roho, hata zikiwa ni za Mungu; kwa kuwa manabii wengi wa uongo wameenda kule ulimwenguni. Kwa haya mtamjua Roho wa Mungu: kila roho anayekiri kuwa Yesu Kristo amekuja katika mwili ni wa Mungu, na kila roho asiyekiri kuwa Yesu Kristo amekuja katika mwili si wa Mungu. Na huyu ndiye roho Mpingakristo, ambaye mmesikia atakuja, naye tayari yuko ulimwenguni.

Kwa Ajili ya Kinga Yetu

Ukosefu wa mafundisho haya umeacha mwili wa Kristo bila kinga!

Kila mwamini inambidi aombe kwa ajili ya kuchochea kipawa cha kubainisha roho kwa ajili ya kinga yake mwenyewe, kinga ya jamii yake, na kinga kwa ajili ya mwili wa Kristo.

UDANGANYIFU

Tahadhari ya Mtume Paulo

Paulo alionya juu ya udanganyifu ulioko kote karibu nasi.

➢ *Mitume wa Uongo*
➢ *Watenda kazi Wadanganyifu*

2 Wakorintho 11:13-15 Kwa kuwa hawa ndio mitume wa uongo, watendakazi wadanganyifu, wakijibadilisha na kuwa mitume wa Kristo. Ndiyo maana! Kwa kuwa Shetani mwenyewe hujibadilisha na kuwa malaika wa nuru. Kwa hivyo si jambo kubwa watumishi wake wanapojibadilisha na kuwa watumishi wa haki, ambao mwisho wao ni kulingana na kazi yao.

➢ *Kutoweka kutoka kwa Imani*

1 Timotheo 4:1,2 Na sasa Roho anasema wazi kuwa nyakati za mwisho wengine watatoka katika imani, wakiwafuata roho na kanuni za mapepo, wakinena uongo kwa udanganyifu, wakiwa na mawazo yao wenyewe yakiwa juu ya chuma moto.

➢ *Having Form of Godliness*

2 Timotheo 3:1-9 Lakini jueni haya, kuwa katika siku za mwisho nyakati ngumu zitakuja: kwa kuwa wanadamu watajipenda wenyewe, wapenda pesa, wanaojivuna, wenye kiburi, kufuru, wasiotii wazazi, wasio na shukrani, wasiotakatifu, wasio na upendo, wasiosamehe, kusingizia, bila kujizuia, wabaya, wenye kudharau mema, wasaliti, vichwa ngumu, kiburi, wapenzi wa anasa badala ya kumpenda Mungu, wakiwa na dalili ya kiungu lakini wanaokana nguvu zake.

Na kutoka kwa watu hao kaa mbali! Kwa kuwa kati yao kuna wale wanaonyapia katika manyumba na kuwafanya watumwa wanawake waliojaa dhambi, waongozwao na tamaa nyingi, kila mara wanajifunza bila ya kufikia ufahamu wa kweli hizo.

Nao Janes na Jambro walipompinga Musa, nao hawa wanapinga ukweli: wanadamu wenye fikira fisadi, ipingayo kuhusu imani; lakini wataendelea pasipo, kwa kuwa upumbavu wao utaonekana kwa wote, kama vile wao ulivyokuwa.

➢ *Kukua Ukiharibika zaidi*

2 Timotheo 3:13 Lakini watu waovu na walaghai watakua wabaya zaidi, wakihadaa na kuhadaiwa.

JUKUMU LETU!

➢ *Kupima kila Roho*

Mungu hakutaka tuwe bila kinga dhidi ya roho waovu. Yeye ametuamuru kupima roho naye ametupatia maagizo jinsi ya kufanya hivyo. Pia ametupatia kipawa cha kutofautisha kati ya roho ili tuweze kujua yanayotendeka karibu nasi.

1 Yohana 4:1-6 Wapendwa, msiamini kila roho, bali wapimeni roho, kama zinatoka kwa Mungu; kwa kuwa nabii wengi wa uongo wameenda kule nje ulimwenguni. Kupitia haya mtajua kuwa Roho wa Mungu: kila roho anayemkiri Yesu Kristo amekuja katika mwili ametoka kwa Mungu.

➢ *Kipimo ni Kipi?*

Na kila roho ambaye hakiri kuwa Yesu Kristo amekuja katika mwili hatoki kwa Mungu. Na hii ndiyo roho apingaye Kristo, ambaye mlimsikia atakuja, naye tayari yuko ulimwenguni.

Ninyi ni wa Mungu, watoto wadogo, nanyi mmewashinda, kwa kuwa Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yule aliye ulimwenguni. Wao ni wa ulimwengu. Kwa hivyo wao hunena kama wa ulimwengu, nao ulimwengu unawasikia. Sisi ni wa Mungu. Yeye amjuaye Mungu hutusikia; yeye asiye wa Mungu hatusikii. Kwa haya tunajua roho wa kweli na roho adanganyaye.

SEHEMU MBILI YA UDANGANYIFU

Udanganyifu wa Mwanadamu

➢ *Watu Wanaoasi*

Watu huwadanganya wengine kwa sababu nyingi, lakini faida ya kifedha na tamaa ya cheo na sifa ni aina tatu muhimu iletayo haya.

Tito 1:10 Kwa kuwa kuna wagaidi, wanaoongena tupu na wadanganyifu, hasa wale katika tohara.

Warumi 16:18 Kwa kuwa walio hivyo hawamtumikii Bwana Yesu Kristo, bali matumbo yao, na kwa maneno matamu na usemi uliojaa kiburi hudanganya mioyo wa wanyonge.

➢ *Anania na Safira*

Petro, kupitia zawadi, ilibaini kuwa mioyo ya Anania na Safira ilijaa uongo wa Shetani. Walibakisha sehemu ya pesa iliyotolewa kwa ajili ya huduma. Kubainisha kati ya roho hulinda mwili wa Kristo dhidi ya wadanganyifu.

Matendo 5:1-3 Lakini mtu mmoja aitwaye Anania, pamoja na Safira mkewe, waliuza mali. Naye akabakisha sehemu ya malipo, mkewe pia alijua haya, na kuleta sehemu na kuweka miguuni mwa mitume.

Lakini Petro, akasema, "Anania, kwa nini Shetani mejaza moyo wako umdanganye Roho Mtakatifu na kujibakishia sehemu ya bei ya shamba?"

➢ *Walaghai*

2 Timotheo 3:13 Lakini watu waovu walaghai wataendelea kuharibika, wakidanganya na kudanganywa.

Ulaghai wa Kishetani

2 Yohana 1:7 Kwa kuwa wadanganyifu wengi wameenda nje ulimwenguni wasiokiri Yesu Kristo kama aliyekuja katika mwili. Huyu ni mdanganyifu na mpingakristo.

Matayo 24:24 Kwa kuwa kristo waongo na nabii waongo watakuja na kuwaonyesha ishara kubwa, ili kuwahadaa, ikiwezekana, hata wateule

Kupitia kubainisha roho, tunaweza kujua wakati tunadanganya na aidha Shetani kupitia watu au hali, au na watu wenyewe. Ufahamu huu uliodhihirishwa hufanyika kinga yetu.

YESU ALITENDA KATIKA KUBAINISHA KATI YA ROHO

"Wewe Ndiye Kristo"

Tunayo mifano miwili ya maneno yaliyosemwa na Petro. Moja ni ya Mungu nayo nyingine ni ya Shetani. Wakati Yesu alienenda katika kubainisha kati ya mapepo, tunaweza kuona jinsi nasi tunaitajika pia kuenenda katika kipawa hiki.

Matayo 16:16,17 Naye Simoni Petro akajibu akisema, "We ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aishiye."

Yesu akajibu na kumwambia, "Umebarikiwa wewe Simoni wa Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukutokezea haya, bali Baba yangu aliye mbinguni."

Maneno ya Petro haikusemwa kutokana na ufahamu wa mwanadamu, bali yalidhihirishwa na Baba.

Shetani Kakemewa

Baadaye kufuatiwa maneno haya, Petro alijitwika mwenyewe akimkemea Yesu akisema kuwa Yesu hakuwa ateseke. Tunaweza kubishana kuwa ilikuwa ni katika Petro kumjali Yesu ndiko kulimsababisha kumzuia Yesu. Kwa maneno mengine, hakuonekana kukosea kwa maneno yake. Lakini Yesu alimtaja Petro kama Shetani kwa kuwa Yesu alibaini roho aliyekuwa chanzo cha maneno ya Petro.

Matayo 16:22,23 Kisha Petro akamchukua kando na kuanza kumkemea Yeye, akisema, "Basi na iwe mbali Nawe, Bwana: haya hayatafanyika kwako!"

Lakini Yeye akamgeukia Petro na kumwambia, "Rudi nyuma yangu, Shetani! Wewe ni pingamizi kwangu, kwa kuwa haujali mambo ya Mungu, bali mambo ya wanadamu."

Roho wa Kiziwi na Bubu

Yesu kila mara alihudumu uponyaji kwa kunenea pepo aletaye shida hiyo.

Mariko 9:25b Yeye alikemea pepo mchafu, akimwambia, "Wewe pepo wa kiziwi na bubu, nakuamuru, toka ndani yake, na wala usimwingie tena kamwe!"

MIFANO YA AGANO LA KALE – KUBAINISHA KATI YA MAPEPO

Mjakazi Aona Ulimwengu wa Roho

Elisha aliomba kuwa mjakazi wake ataona ulimwengu wa roho.

2 Wafalme 6:16,17 Basi Akajibu, "Usiogope, kwa kuwa wale walio nasi ni zaidi ya wale walio nao."

Naye Elisha aliomba, na kusema, "BWANA, naomba, fungua macho yake ili aone." Kisha BWANA akayafungua macho ya kijana huyo, naye akaona. Na tazama, mlima ulijaa farasi na magari ya mioto kila pande za Elisha.

Wakati wowote mtu anapoona katika ulimwengu wa roho – ukidhihirisha roho wa mema au maovu, hii ni kubainisha kati ya roho.

Tunatakiwa kuomba, kama Elisha, kuwa macho yetu ya kiroho yatafunguliwa.

Isaya Aliona

Isaya 6:1 Mwaka ule mfalme Uzia alikufa, nilimwona Bwana ameketi kwenye kiti cha enzi, juu na ameinuliwa, nayo ncha ya vazi Lake lilijaza hekalu.

MIFANO YA AGANO JIPYA – KUBAINISHA KATI YA MAPEPO

Paulo na Msichana Mjakazi

➢ *Usemi Mzuri Kutoka kwa Roho Mwovu*

Matendo 16:16-18 Sasa ikafanyika, tulipoingia katika maombi, msichana mmoja kijakazi aliyepagawa na pepo wa kutabiri alikutana nasi, aliyemletea mkubwa wake faida kubwa kwa kutabiri-mema.

Msichana huyu alimfuata Paulo nasi, na akalia, akisema, "Watu hawa ni watumishi wa Mungu Aliye Juu, wanaotutangazia njia ya wokovu."

Na haya alifanya kwa siku nyingi. Lakini Paulo, kwa kukasirika sana, akageuka na kuiambia roho hiyo, "Nakuamuru katika jina la Yesu Kristo utoke ndani yake." Naye akatoka wakati huo huo.

Je, roho wa kutabiri ndani ya msichana huyo alikuwa akijaribu kufunika kuwepo kwake kwa kutoa "taarifa nzuri?" Yale msichana alisema yalikuwa kweli.

Tumeambia kuwa Paulo alisumbuka kwa siku nyingi. Kwa nini? Paulo alikuwa akikojea kutambua roho wa msichana huyo.

➢ *Kiini*

Inawezekana sana, pepo ndani yake walikuwa wakitafuta kukubalika na kujihuzisha.

KIPAWA CHA KUBAINISHA KATI YA ROHO LEO

Usiwe wa Kupuuza

Kumbuka – Mungu hataki sisi tuwe wa kupuuza roho walio karibu nasi – roho tunaojumuika nao – roho wapatikanao maeneo yetu.

Hatuwezi tu kuwaza kuwa kitu fulani ki sawa, ni lazima tujue ni roho gani wanatenda kutoka kwa Mungu.

Hatujui roho ambaye mtu anatumikia hadi Mungu atuonyeshe.

1 Yohana 4:6 Sisi ni wa Mungu. Yeye amjuaye Mungu hutusikia; yeye asiye wa Mungu hawezi kutusikia. Kwa haya tunajua roho wa kweli na roho wa makosa.

Sisi ni wa Mungu na tunayo haki kujua tofauti kati ya roho za kweli na roho wa makosa.

Chukua Hatua

Mungu haleti roho mwovu kwa mwamini bila kusudi. Wakati roho waovu wanapobainika, inatakiwa mara moja wafungwe au kukemewa kulingana na hali.

Mariko 16:17 Na ishara hizi zitawafuata wale wanaoamini: katika jina Langu watawakemea mapepo; watanena katika ndimi mpya ...

Luka 10:19,20 Tazama, Nawapa mamlaka kuwakanyaka nyoka na nge, na juua ya nguvu zote za adui, na hakuna kitu kitakachowadhuru kamwe. Hata hivyo msifurahi kwa ajili ya haya, kuwa roho zinawatii, bali furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa mbinguni.

Tayari mmepewa mamlaka juu ya adui. Yesu alituambia kile tutafanya.

➢ Wakemee mapepo

➢ Wakanyage nyoka na nge

➢ Shindeni dhidi ya nguvu zote za adui

➢ Kutokufurahia kuwa mapepo yanatutii – bali kuwa sisi ni wa Mungu

HATARI YA KUWA NA KIINI MBAYA

Tunaonywa juu ya hatari ya kujaribu kujifaidisha na vipawa vya Roho Mtakatifu kupitia maazimio mabaya.

Simoni

Matendo 8:7-9 Kwani roho wachafu, wakilia kwa sauti kubwa, waliwatoka wengi waliopagawa; na wengi waliopooza na kulemaa waliponywa. Na pakawa furaha kuu katika mji ule.

Lakini palikuwepo mtu mmoja aliyeitwa Simoni, ambaye awali alifanya uchawi katika mji na kuwashangaza watu wa Samaria, akijidai kuwa alikuwa mtu mkuu.

Matendo 8:13,18-24 Kisha Simoni mwenyewe pia akaamini; naye alipobatizwa aliendelea na Filipo, na akashangaa, kwa kuona miujiza na ishara iliyotendeka.

➢ *Kutoa Fedha*

Basi Simoni alipoona kuwa Roho Mtakatifu alikuja kupitia kuwekelea mikono kwa mitume, aliwapa fedha, akisema, "Nipe nguvu hizi pia, ili kuwa yeyote nitakayemwekelea mikono aweze kupokea Roho Mtakatifu."

➢ *Kunyimwa na Petro*

Lakini Petro akamwambia, "Fedha zako na ziangamie nawe, kwa kuwa umedhania kuwa kipawa cha Mungu kinaweza kunuliwa kwa pesa! Nawe hauna nafasi wala sehemu katika mambo haya, kwa kuwa roho yako haiku sawa machoni mwa Mungu. Tubu basi juu ya uovu huu, na umwombe Mungu kuwa labda wazo la moyo wako lisamehewe.

Petro alibaini roho aliyesababisha kitendo cha Simoni.

Kwa kuwa naona kuwa umeadhirika na chuki na kufungwa na uovu."

Kisha Simoni akajibu akisema, "Niombeeni Bwana, ili kusitokee vitu mlivyosema juu yangu."

Wa-Yesu

➢ *Kupinga Mitume*

Matendo 13:6-12 Na sasa walipopita kisiwa kwenda Pafosa, walimkuta mchawi fulani, nabii mwongo, Myahudi jina lake Wa-Yesu, aliyekuwa na kiongozi Sajio Paulo, mwenye hekima ya juu. Mtu huyu aliwaita Barnaba na Saulo na kutaka kusikia neno la Mungu. Lakini Elima mchawi (ambayo ndiyo tafsiri ya jina lake) wakawazuia, wakitaka kumpinga kiongozi mbali na imani.

➢ *Kutambulika kwa Wazi*

Naye Saulo, ambaye pia anaitwa Paulo, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, alkimtazama na kumwambia, "Ewe uliyejaa ulaghai na fujo yote, ewe mwana wa ibilisi, wewe uliye adui wa haki zote, je hautakoma kupotosha njia nyoofu ya Bwana? Na sasa, hakika, mkono wa Bwana uko juu yako, nawe utakuwa kipofu, usiweze kuliona jua kwa muda."

➢ *Hukumu*

Na punde umande mweusi ukaja juu yake, naye akaenda akimtafuta mtu atakayemwongoza kwa mkono. Naye kiongozi akaamini, alipoona kile kiletendeka, akishangaa kwa mafundisho ya Bwana.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza kipawa cha kubainisha kati ya roho katika maneno yako mwenyewe.

2. Je, nini utenda kazi wa kipawa hiki ni muhimu kwako?

3. Eleza kwa kina sehemu tatu za kazi ya roho ambazo unaweza kujihuzisha nazo.

Somo la Tisa

Kipawa cha Ufunuo
Neno la Ufahamu

1 Wakorintho 12:8-10 Kwa kuwa Roho humpa mmoja ujumbe wa hekima, na mwingine neno la maarifa kupitia Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji wa miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi.

Utumainifu wa Sauti	*Vipawa Tisa vya Roho Mtakatifu*	**Nguvu**
Ndimi	**Ufunuo**	Kipawa cha Imani
Tafsiri ya Ndimi	Kutofautisha Kati ya Roho	Kipawa cha Uponyaji
Unabii	➥**Neno la Ufahamu**	Kutenda Miujiza
	Neno la Hekima	

NENO LA UFAHAMU

Kufafanua

Neno la ufahamu ni ufunuo usiokawaida katika Roho Mtakatifu juu ya kweli fulani, ya sasa au awali, kuhusu mtu au hali, ambayo haikufunzwa katika fikira za kawaida. Mara nyingi itaingilia kati ya mawazo yetu ya kawaida. Itakuja kama wazo, neno, jina, hisia, onyo, maono au "ufahamu wa ndani." Hata kama neno ni sehemu ndogo ya sentensi, neno la ufahamu ni sehemu ndogo ya ufahamu kamili wa Mungu kuhusu hali.

Neno la ufahamu isiwe sababu ya kutokusoma Neno la mungu.

2 Timotheo 2:15 Kuweni watimilifu katika kukubalika mbele za Mungu, mtenda kazi asiye na aibu, na agawaye neno la kweli.

Neno la ufahamu, hata hivyo, sio ufahamu utokanao na miaka ya ujuzi katika kutembea na Bwana na kuwa na muda na Neno Lake.

Aina Nne ya Ufahamu

➢ *Wa Kibinadamu*

Ufahamu wa kibinadamu huja kawaida kupitia elimu, utafiti wa kisayansi na ustadi maishani. Mengi yamekuja kupitia sehemu hii ya ufahamu. Lakini bila ufahamu wa Mungu, uamuzi wa kimakosa na na usiokamilika umefanywa ambao husababisha mawazo mabaya.

➢ *Uovu Usiokawaida*

Ufahamu usiokawaida ambao chanzo chake ni uovu hutokana na mafunzo ya kichawi, kujihuzisha na ulozi, kuabudu sanamu, miungu wa kidini, uchunguzi wa kisayansi, na sehemu zingine za kishetani. Sehemu hii ya ufahamu inaweza kuwa ya kuvutia na lazima ikataliwe kabisa. Imekataliwa na Mungu.

➢ *Ufahamu wa Kiroho*

Ufahamu wa sehemu ya kiroho huanza wakati tunapompokea Yesu kama Mwokozi wetu.

Yohana 17:3 Na huu ndio uzima wa milele, kuwa waweze kukujua Wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo ambaye umemtuma.

Ufahamnu huu huongezeka kupitia kujifunza Biblia, mafundisho, kuomba, na kuzungumza na Mungu.

➢ *Neno la Ufahamu*

Ufunuo usiokawaida utokao kwa Mungu juu ya kweli fulani, za sasa au awali, ambazo hatukujifunza kupitia fikira za kawaida.

Kusudi

Mungu kamwe hakutaka watu Wake waishi katika hali za kawaida. Sisi tu watu-wa kiroho na lazima tujifunze kuenenda katika ulimwengu wa kiroho, na pia walio kati yetu.

Mungu anapenda kuwasiliana nasi kupitia neno la ufahamu kwa sababu nyingi. Mojawapo ya kusudi la msingi ni kusaidia katika kukamilisha makusudi ya Mungu kati ya watu Wake.

Neno la ufahamu litadhihirishwa, kutolewa na kuhudumia katika njia iletayo utukufu kwa Mungu, wala kamwe si kwa mtu. Itasaidia na kuwaletea msaada walio katika huduma kila mara likiwaelekeza kwa Mungu anaye chanzo.

Hutusaidia kuhudumu kwa makini na vizuri. Litaonya juu ya hatari yoyote, kuleta himizo, kuweka wazi ndambi na kutuweka “njiani” inayofaa katika maisha na huduma kila siku.

Kwa Kila Mtu

Je, neno la ufahamu litafanya katika waamini wote? Ndiyo!

1 Wakorintho 12:7 Lakini Roho hutolewa kwa kila mmoja ili kuwafaidi wote.

➢ *Mfano wa Anania*

Anania hakuwa mtume, mchungaji, mwinjilisti au mwalimu. Alikuwa wa kawaida, mwamini. Bibilia inamwita mwanafunzi.

Matendo 9:10-12 Basi palikuwa mtu mmoja mwanafunzi hapo Damaski jina lake anania; naye Bwana akamwambia katika maono, "Anania."

Naye akasema, "Ndiyo, Bwana."

Naye Bwana akamwambia, "Inuka na uende barabarani iitwayo Iliyonyooka, na uulize katika nyumba ya Yuda kwa kuwa yule aitwaye Saulo wa Tarsa, tazama, yeye anaomba. Na katika maono amemwona mtu aitwaye Anania akimjia na kumwekelea mkono wake, ili apate kuona."

Mungu alimwambia Anania:

- ➢ Jina la barabara
- ➢ Jina la Saulo
- ➢ Kuwa Saulo alikuwa amepewa maono

Yaliyomo katika maono hayo ni neno la ufahamu na pia neno la hekima. Ufahamu ulikuwa kweli. Hekima ilikuwa ufunuo kuhusu kile Anania alitakiwa kufanya na kitakachotendeka.

NENO LA UFAHAMU KATIKA KUTENDEKA

Tunaweza kuona kitu katika Roho juu ya mtu au mahali.

Tunaweza kusikia neno au usemi kutoka ndani yetu.

Tunaweza kuhisi mwilini mwetu ubainifu wa kitu kuhusu mwu mwingine.

Tunapopokea neno la ufahamu haimaanishi kuwa tunaitajika kulitenda mara moja. Mara nyingi tunaitajika kungojea kupata neno la hekima kutuambia jinsi tunaweza kuendelea. Wakati mwingine neno la ufahamu na hekima itafanyika kwa wakati mmoja na kuruhusu kutimika kwa kusudi la Mungu mara moja.

Neno la ufahamu linaweza kutumika na Mungu kumkabidhi mtu mwingine akiwa katika hali mbaya, au juu ya dhambi maishani mwao. Maneno kama haya ni lazima yatolewe kwa upendo, mara nyingi mbali na watu, na kila mara kutendeka katika neno la hekima!

Tahadhari!

Roho Mtakatifu hatoi maneno ya ufahamu ili kumwinua mtu mmoja juu ya wengine. Uwe macho kuhusu "neno la ufahamu" lolote ambalo linaweza kuleta sifa kwako, au kujenga huduma fulani. Mungu hatendi katika "siri."

Yesu hakutenda akijituma Mwenyewe. Kila mara alikuwa na Roho Mtakatifu akikazia mbinguni. Alipomwona Baba akifanya au kusema, kitu, Yeye basi angefuata juu ya neno la ufahamu au neno la hekima.

Yohana 5:19 Kisha Yesu akajibu akiwambia, "Amini amini, nawambia, Mwana hatafanya chochote Mwenyewe, bali kile anamwona Baba akifanya; kwa kuwa chochote afanyacho, Mwana pia hufanya kwa njia hiyo hiyo."

"Kipawa chochote cha ufunuo" ambacho huchangia ukweli katika matukio ya kibiblia itakuwa ya kuchunguzwa. Neno la ufahamu kila mara litaangazia Neno la Mungu kama lilivyoandikwa. Roho Mtakatifu akiwa mwanzilishi wa Neno, kamwe hatabadilisha, au kurekebisha alichoandika.

"Kweli" yoyote itakayobadilisha ua kuongezea juu ya wokovu au ufahamu juu ya utatu wa Mungu lazima ikataliwe kama isiyotoka kwa Mungu.

Ikiwa Roho wa Mungu anatenda katika sehemu fulani ya wazo au huduma wakati wa mkutano, hapo hapatakuwa na neno la ufahamu ambalo litaruka katika sehemu nyingine tofauti kabisa. Mungu anakutarajia utende juu ya ufunuo, lakini ni lazima ifuate mtiririko, upako na wakati wa kila mkutano fulani.

Tunaitajika kufuata maagizo ya Roho Mtakatifu kulingana na muda wa Mungu na mpango Wake. Yeye kamwe siye mwanzilishi wa mchanganyiko.

MIFANO YA NENO LA UFAHAMU KATIKA AGANO LA KALE

Ahija Alionywa Juu ya Ulaghai

Ahijaa nabii alionywa na Mungu juu ya ulaghai ambao ungekuja juu yake.

1 Wafalme 14:2-6 Naye Yeroboamu akamwambia mkewe, "Inuka, na ujigeuze, ili wasikutambue kama mke wa Yeroboamu, na kisha uende Shiloh. Kwa kweli, Ahija nabii yuko huko, aliyeniambia kuwa nitakuwa mfalme juu ya watu hawa. Pia beba mikate kumi, keki pia, na chupa ya asali, nawe umwendee; yeye atakwambia kitakachotokea kwa mtoto."

Naye mkewe Yeroboamu akafanya hivyo; akainuka na kuenda Shilo, naye akaja kwa nyumba ya Ahija. Lakini Ahija hakumwona, kwani macho yake yalikuwa mazito kwa ajili ya umri wake. Na sasa Bwana alikuwa amemwambia Ahija, "Hapa kuna mkewe Yeroboamu, akija kukuuliza kitu kuhusu mwanawe, kwa kuwa yu mgonjwa. Nawe basi utamwambia; nayo itakuwa, atakapoingia kwako, kuwa amejifanya mwanamke mwingine."

Na basi ikawa, wakati Ahija aliposikia sauti ya hatua zake akija mlangoni, alisema, "Ingia ndani, mke wa Yeroboamu. Kwa nini unajifanya kuwa mtu mwingine? Kwa kuwa nitumwa kwako nikiwa na habari mbaya."

Neno la ufahamu na neno la hekima lilitendeka Bwana alipomwambia:

➢ Yeye alikuwa nani – mke wa Yeroboamu

➢ Kwa nini alikuja – Kuuliza juu ya mtoto

➢ Kile anatakiwa kusema – basi utasema

➢ Kile atakachofanya – kujifanya mtu mwingine

Ahija kisha akaendelea kutoa unabii kwake kuhusu mwisho wa utawala wa Yeroboamu. Neno lake la ufahamu kuhusu ulaghai huu uliufanya unabii wake kuwa kweli zaidi.

Eliya Kuhimizwa

Baada ya Nabii Eliya kuita mota wa Mungu mlimani Kameli, Yezebeli alitishia maisha yake. Eliya alikimbia na kisha katika kukata tamaa alimlilia Mungu.

➢ *Yachukue Maisha Yangu*

1 Wafalme 19:4,14 Lakini yeye mwenyewe akaenda safari ya siku moja jangwani, naye akaja na kuketi chini ya mti mpana. Naye akaomba kuwa afe, akasema, "Imetosha! Sasa, BWANA, yachukue maisha yangu, kwa kuwa mimi si mwema kuliko baba zangu!"

➢ *Mimi tu Ndiye Nimesalia*

Kisha akasema, "Nimekuwa na bidii sana kwa ajili ya BWANA Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wametupilia mbali agano Lako, wamezivinja dhabihu zako, na kuwaua nabii wako kwa upanga. Mimi pekee nimesalia; nao wanayatafuta kuyatoa maosha yangu."

➢ *Mungu Alikuwa na 7,000*

Mungu akajibu,
1 Wafalme 19:18 "Nami nimeweka katika Israeli elfu saba, wote ambao magoti yao haijainama mbele ya Baal, na kila kinywa kisichombusu."

Gehazi Ajulikana

Neno la ufahamu lilitendeka mara nyingi kumpitia Elisha kuliko mtu mwingine aliyeandikwa katika Agano la Kale.

Baada ya Namani kuponywa alijitolea kumzawadi Elisha mara mbili lakini Elisha alikataa malipo aina yoyote, au kuonyeshwa shukrani.

➢ *Kumhadaa Namani*

2 Wafalme 5:20-27 Lakini Gehazi, mtumishi wa Elisha Mtu wa Mungu, akasema, "Tazama bwana wangu amemsamehe Namani Msiria huyu, kwa kutokupokea mikononi mwake alichaletewa; lakini aishivyo Bwana, nitakimbia nyuma yake na kupata kitu kutoka kwake."

Kwa Gehazi akamfuata Namani. Wakati Namani alipomwona akimukimbilia, alishuka kutoka gari la farasi kukutana naye, na kusema, "Je, kilatu ni sawa?"

Naye akasema, "Yote ni sawa. Bwana wangu amenituma, akisema, 'Kwa kweli, sasa hivi vijana wawili wa nabii wamekuja kwangu kutoka milimani Ifraimu. Tafadhali wape talanta ya fedha na mavasi mawili ya kubadilisha.'"

Kwa hivyo Namani akasema, "Naomba uchukue talanta mbili." Naye akamsihi na kufunganisha talanta mbili za fedha katika mifuko miwili, na mavasi mawili ya kubadilisha na kuwapa watumishi wake wawili; nao wakazibeba wakimtangulia.

➢ *Alificha Vitu Vilivyoibiwa*

Alipofika Sitateli, alichukua kutoka mikononi mwao, na kuzifukia mbali na nyumba; naye akawaachilia waende, nao wakaondoka.

➢ *Alimdanganya Elisha*

Naye akaingia ndani na kusimama mbele ya bwana wake. Naye Elisha akamwambia, "Ulienda wapi, Gehazi?" Naye akasema, "Mtumwa wako hakuenda popote."

Elisha alikuwa ameona katika hali isiyokawaida, (kitendo cha neno la ufahamu), yote aliyofanya Gehazi. Alieleza kwa kina yale aliona kupitia kipawa hiki.

➢ *Matokeo Yalikuwa Ukoma*

Kisha akamwambia, "Je, moyo wangu haukuenda nawe mtu huyo aliposhuka kutoka gari lake na kukutana nawe? Je, ni wakati wa kupokea fedha na mavazi, sehemu za mizeituni na bustani, kondoo na ngombe, watumwa waume kwa wa kike? Kwa hivyo ukoma wa Namani utakushika pamoja na vizazi vyako milele." Naye akaondoka pale akiwa mwenye ukoma, mweupe kama theluji.

Onyo Kuhusu Mpango wa Adui

Elisha alikuwa sana karibu na sauti ya Mungu hata mfalme wa Syria akaanza kmtafuta msaliti kati yake. Kisha mtumwa wake akamwambia, Elisha, nabii, humwambia mfalme wa Israeli maneno yale yale unayoongea katika chumba cha ndani!

2 Wafalme 6:9-12 Naye mtu wa Mungu akamwendea mfalme wa Israeli, akisema, "Chunga usipite sehemu hii, kwa kuwa Wasyria wanakuja kule chini."

Kisha mfalme wa Israeli akamtuma mtu mahali ambapo mtu wa Mungu alimwambia. Basi akamwonya, naye akawa mwangalifu pale, sio tu mara moja au mbili.

Kwa hivyo roho ya mfalme wa Syria ilifadhaika sana juu ya jambo hili; naye akawaita watumishi wake na kuwaambia, "Je, hamwezi kusema nani kati yetu yuko upande wa mfalme wa Israeli?"

Naye mmoja wa watumwa wake akasema, "Hakuna, bwana wangu, ewe mfalme; bali Elisha, nabii aliye Israeli, humwambia mfalme wa Israeli maneno usemayo katika chumba cha ndani."

NENO LA UFAHAMU KATIKA MAISHA YA YESU

Tunapojifunza maisha ya Yesu ni rahisi kufikiria, "Aha, Angefanya hiyo. Alienenda kama Mungu." Lakini Yesu aliweka kando uwezo wake kama Mungu na kutembea hapa duniani kama Adamu kamili alivyoumbwa kutenda. Yeye ni mfano wetu. Mambo aliyofanya tunatakiwa kufanya pia! Alienenda hapa duniani katika nguvu za Roho Mtakatifu sawa na jinsi waamini wa leo wanatakiwa kufanya.

Mwanamke Msamaria

Yesu aliponena na mwanamke kisimani, alipokea neno la ufahamu kuhusu mabwana wake. Ufahamu huu juu ya kitu ambacho hangejua katika hali ya kawaida uliongoza hadi wokovu wa wengi katika kijiji hicho. Ni muhimu kugundua kuwa hata kama Yesu alijua kitu kilichokua cha kuhukumu, hakutumia ufahamu huo kuhukumu. Kupitia neno la hekima, alitumia ufahamu huo kumleta kwa wokovu.

Yohana 4:16-18,39-42 Yesu akamwambia, "Nenda, ukamwite mumeo, na uje hapa."

Mwanamke akamjibu na kusema, "Sina mume."

➢ *"Umekuwa na Watano"*

Yesu akamwambia, "Umesema vyema, `Sina mume,' kwa kuwa umekuwa na waume watano, na yule uliye naye sasa si mumeo; kwa hivyo umesema ukweli."

Nao Wasamaria wengi kutoka mji huo wakamwamini Yeye kwa sababu ya neno la mwanamke aliyeshuhudia, "Aliniambia yote niliyowai kufanya."

➢ *Matokeo – Wengi Waliamini*

Kwa hivyo Wasamaria walipomjia Yeye, walimsihi akae nao; Naye akasalia hapo siku mbili. Na wengi zaidi wakaamini maneno Yake mwenyewe.

Kisha wakamwambia mwanamke, "Sasa tunaamini, si kwa yale uliyotuambia, kwa kuwa tumemsikia wenyewe na tunajua kuwa huyu kwa kweli ni Kristo, Mwokozi wa ulimwengu."

Mtu Kipofu

Yesu alijua kuwa chanzo cha upofu wa mtu huyo haukuwa kwa ajili ya dhambi zake au za babaye. Haiwezekani kuwa kawaida angejua haya. Ilikuwa kupitia neno la ufahamu.

Yohana 9:3 Yesu alijibu, "Si mtu huyu wala wazazi wake walitenda dhambi, bali kazi ya Mungu iweze kudhihirishwa ndani yake."

Kulipa Kodi

Ilipokuwa muda wa kulipa kodi ya Kirumi Yesu alimwamuru Petro kunasa samaki, kufungua kinywa chake na kutoa sarafu waliyoitaji. Tena, hakuna uwezekano kwa kawaida Yeye angejua hili.

Matayo 17:27 Hata hivyo, tusije tukawakasirisha, nenda baharini, rusha ndoana, kisha utoe samaki atakayekuja kwanza. Na utakapofungua mdomo wake, utakuta kipande cha fedha; chukua hiyo uwape kwa ajili yangu nawe.

Katika Pasaka

Yesu alijua kuwa wanafunzi watakutana na mtu akibeba mtungi wa maji. Walikuwa wamfuate hadi nyumbani na kuwa nyumba hii itakuwa na chumba cha juu kilichotayarishwa kwa ajili yao kutumia.

Luka 22:10-12 Naye akawaambia, "Tazama, mnapoingia mjini, mtu atakutana nanyi akiwa amebeba mtungi wa maji; mfuate hadi nyumbani atakamoingia. Kisha mtamwambia mkuu wa nyumba, 'Mwalimu anakwambia, "Je, chumba cha wageni kiko wapi ambamo naweza kula Pasaka na wanafunzi Wangu?" 'Kisha atawaonyesha chumba, cha juu, kikubwa; hapo kitayarisheni."

Atakayemsaliti

Yesu alijua atakayemsaliti.

Johana 13:26 Yesu akajibu, "Ni yeye yule nitakayempa kipande cha mkate baada ya kuuzamisha." Na baada ya kutia mkate, akampa Yuda Isikarioti, mwana wa Simoni.

MIFANO KATIKA AGANO JIPYA

Konelio

Konelio alipokea maagizo kupitia maono. Maagizo yalikuwa kwamba angemwita Petro atakayemwambia kile atafanya.

Matendo 10:1-6 Palikuwa mtu mmoja Kaisaria jina lake Konelio, askari wa kiitaliano, mtu mtiifu na aliyemja Mungu na nyumba yake yote, aliyetoa sadaka kwa ukarimu, naye alimwomba Mungu kila mara. Yapata saa tisa ya siku aliona wazi katika maono malaika wa Mungu akimjia na kumwambia, "Konelio!"

Naye alipomwona, aliogopa, na kusema, "Ni nini, bwana,?"

Naye akwambia, "Maombi yako na sadaka zako vimemfikia Mungu katika ukumbusho. Sasa watume watu Joppa, na uwatume kwa Simoni ambaye jina lake Petro. Yeye ameishi na Simoni, mtengenezaji wa ngozi, ambaye nyumba yake iko ukingoni mwa bahari. Yeye atakuambia kile ambacho ni lazima ufanye."

Neno la ufahamu lilimwambia:

- ➢ Mtu aitwaye Simoni Petro,
- ➢ Aliishi na Simoni mtengenezaji wa ngozi,
- ➢ Nyumba ilikuwa ukingoni mwa bahari.

Neno la ufahamu litenda kazi likitoa ukweli, lakini neno la hekima lilitenda kazi katika kumwambia atakachofanya.

Petro

Petro hangeenda nyumba ya mtu wa dunia bila Mungu kuingilia katika maono yasio kawaida.

Matendo 10:17-19 Sasa wakati Petro alihangaika yeye mwenyewe maana ya maono haya aliyoona, tazama, watu waliotumwa kutoka kwa Konelio walikuwa wameulizia nyumba ya Simoni, nao wakasimama mlangoni. Nao wakaitana na kuuliza kama Simoni, ambaye jina lake Petro, alikuwepo.

➢ *Neno la Ufahamu*

Wakati Petro aliwaza juu ya maono, Roho akamwambia, "Tazama, watu watatu wanakutafuta."

Petro alishangaa juu yay ale aliona katika ndoto. Ilienda kinyume na yote aliyofundishwa. Lakini Mungu mara moja akathibitisha maono kwa kuja kwa watu hao. Katika hali hii neno la ufahamu lilifungua ulimwengu wa wengine kwa ajili ya injili ya Yesu Kristo.

Matendo 10:44 Wakati Petro alikuwa angali akiongea maneno haya, Roho Mtakatifu alikuja juu ya wote waliolisikia neno.

Kwa kuwa Konelio aliomba, neno la ufahamu wa Mungu ungekuja.

Paulo

Akiwa Lystra, Paulo alitazama na kuona imani ya mtu tasa. Hii ilikuwa neno la ufahamu kwa vitendo.

Matendo 14:8-10 Na katika Lystra mtu mmoja bila nguvu miguuni mwake alikuwa ameketi, kilema tangu tumboni mwa mama yake, ambaye hakuwai tembea. Mtu huyu akamsikia Paulo akinena. Paulo, kumchunguza na kuona kuwa alikuwa na imani kuponywa, akasema kwa sauti, "Simama kwa miguu yako!" Naye akaruka na kutembea.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, ni ufahamu gani wa neno la ufahamu? Linganisha na sehemu zingine za ufahamu.

2. Je, mtu anawezaje kupokea neno la ufahamu?

3. Toa mfano kutoka maishani mwako wa neno la ufahamu ukutenda kazi ndani yako.

Somo la Kumi

Kipawa cha Ufunuo
Neno la Hekima

1 Wakorintho 12:8-10 Kwa kuwa Roho humpa mmoja ujumbe wa hekima, na mwingine neno la maarifa kupitia Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji wa miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi.

	Vipawa Tisa vya Roho Mtakatifu	
Utumainifu wa Sauti	**Ufunuo**	**Nguvu**
Ndimi	Kutofautisha Kati ya Roho	Kipawa cha Imani
Tafsiri ya Ndimi	Neno la Ufahamu	Kipawa cha Uponyaji
Unabii	➥**Neno la Hekima**	Kutenda Miujiza

NENO LA HEKIMA

Ufafanuzi

Kipawa cha neno la hekima ni ufunuo usiokawaida wa Roho Mtakatifu ukimpa mwamini hekima ya Mungu kuendelea katika njia ya kitendo katika ufahamu wa kawaida au usiokawaida. Hudhihirisha mpango na kusudi la Mungu maishani mwetu na huduma. Hudhihirisha kile Mungu anakusudia kifanyike haraka, kwa wakati mfupi au hivi karibuni au mbali. Hudhihirisha kile mtu au shirika wanatakiwa kufanya na jinsi ya kuendelea katika mapenzi ya Mungu. Neno la hekima mara nyingi huenda pamoja na neno la ufahamu.

Huja Katika Njia Nyingi

Neno la hekima linaweza kuja katika aina nyingi:

- ➢ Sauti ya ndani,
- ➢ Kupitia maono tukiwa macho,
- ➢ Kupitia ndoto tunapolala,
- ➢ Kupitia watu wengine watendao katika vipawa vya ndimi na tafsiri ya ndimi, au kipawa cha unabii.

Si Hekima ya Kawaida

Neno la hekima si kipawa hekima ya kawaida. Ni neno, au kifungu, au sehemu si nzima.

1 Wakorintho 13:9 Kwa kuwa tunafahamu kwa sehemu, tunatoa unabii kwa sehemu.

Wakati neno la hekima linaanza kufanya kazi, ni sehemu tu ya hekima ya Mungu hushirikishwa mwamini. Mungu atadhihirisha sehemu ya uwezo wake wa kutabiri kwa mwamini kupitia roho wa mwanadamu. Mara nyingi hutolewa kwa mwamini kwa haraka na kupinga mtindo wa mawazo ya kawaida. Mawazo ya kawaida ya mwanadamu kwa muda hushikanishwa na/au kuingiana na mawazo ya Mungu. Matokeo ni kuwa mwamini ghafla anagundua mpango wa Mungu na kusudi na jinsi ya kuendelea katika mapenzi ya mungu.

Itakuja kama alama au maono ambapo tutajiona wenyewe katika roho tukifanya kitu kwa njia fulani kabla ya kukifanya.

1 Wakorintho 2:11-13 Kwa kuwa ni nani ajuaye mambo ya mwanadamu isipokuwa roho ya mwanadamu aliye ndani yake? Na hata hivyo hakuna ajuaye mambo ya Mungu isipokuwa Roho wa Mungu.

Sasa tumepokea, si roho wa ulimwengu huu, bali Roho ambaye anatoka kwa Mungu, ili tuweze kuyajua mambo tuliyopewa bure na Mungu. Mambo haya pia tunanena, sio kwa maneno ambayo hekima ya mwanadamu hufundisha bali yale Roho Mtakatifu hufundisha, kwa kulinganisha mambo ya kiroho na kiroho.

Uliza Hekima

Mungu aliposema kuwa yeyote kati yetu anaweza kuuliza hekima alikuwa akiongea juu ya hekima isiyokawaida kutenda katika hali ya kawaida.

Yakobo 1:5 Ikiwa mmoja wenu anakosa hekima, naye amwulize Mungu, atoaye kwa wote na bila upendeleo, naye atapewa.

Tafuta Hekima

Tunapomruhusu Roho Mtakatifu kuenenda maishani mwetu katika maneno ya hekima, tunaweza kutoka kwenye hali ya kawaida hadi hali isiyokawaida. Tunapoomba kwa ajili yetu wenyewe na wengine, tunaweza kupokea hekima isiyo kawaida ambayo itatuonyesha jinsji ya kuomba na cha kusema.

Neno Likolee Ndani yako

Neno la hekima isichanganyishwe na hekima ya kawaida au ya kujifunza. Sio kisingizio cha kukosa kutafuta hekima kama tunavyoambia katika kitabu kizima cha Mithali.

Zaburi 2:1-6 Mwanangu, ikiwa utapokea maneno yangu, na kuzingatia amri zangu ndani yako, nawe uyaweke masikio yako kwa hekima, na uweke moyo wako juu ya ufahamu; ndiyo, ikiwa utaulilia ubainifu, na kuiinua sauti yako kwa ajili ya ufahamu, ikiwa utamtafuta kama fedha, na kutafuta kama vile vitu vya dhamani vilichofichwa; basi utaelewa hofu ya BWANA, na kupata ufahamu wa Mungu.

Yoshua aliambiwa kuwa alitakiwa atafakari juu ya Neno, usiku na mchana. Kwa kufanya hivyo tunaweka msingi imara wa Neno ambapo tunapata utendaji wa neno la la hekima.

Yoshua 1:8 Kitab hiki cha sharia hakitakutoka kinywani mwako, bali utatafakari mchana na usiku, ili uweze kushika na kutenda kulingana na yote yaliyoandikwa humo. Kwa kuwa hapo ndipo utafanya njia zako kunawiri, nawe basi utapata kufaulu.

Kusudi

Neno la hekima hutolewa kwa ajili ya ulinzi na maagizo.

Neno la hekima mara nyingi litadhihirisha kwetu jinsi ya kutumia ufahamu utokanao na neno la ufahamu au kubainisha kati ya roho. Inaweza kutoa ufahamu wa ndani juu ya jinsi ya kuomba katika hali fulani. Inaweza kutupatia "ufunguo" ili kumsaidia mtu tunayeomba naye.

Mwamini ghafla atasikia maneno mapya, yajengayo au semi katika roho yake. Maneno haya mara nyingi yataingilia mawazo ya kawaida kana kwamba yamedungwa mawazoni haraka. Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu inayomfanya mwamini kujua mapenzi ya Mungu katika hali hiyo. Inaweza kufanyika wakati wowote, popote, wakati mwingine bila kutarajia. Hivyo ndivyo unaweza kujua ni Roho Mtakatifu na wala sio wewe mwenyewe unayefikiria mambo haya. Funuo hizi mara nyingi hutusaidia kufanya mpango wa Mungu na kusudi katika hali hiyo.

KUPOKEA NENO LA HEKIMA

Vipawa vyote hupokelewa kwa imani. Ikiwa hatutendi katika kipawa fulani, tunaweza kumwuliza Mungu aachilie kipawa chochote ndani yetu.

Matayo 7:7,8,11 Uliza, na mtapewa; tafuta, nanyi mtapata; bisha, na mtafunguliwa. Kwa kuwa yeyote aulizaye hupokea, naye atafutaye hupata, na kwa yule abishaye atafunguliwa.

Ikiwa basi, mkiwa waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, basi ni kiasi gani zaidi Baba wenu wa mbinguni kutoa Roho Mtakatifu kwa wale wanaomwuliza!

Hatua katika kupokea neno la hekima:

- ➢ Omba na umwulize Mungu kipawa cha hekima kibainike maishani mwako.
- ➢ Kwa imani tazamia Mungu atende.
- ➢ Enenda katika uongozi wowote, hata kama itaonekana ya kijinga kwako.
- ➢ Tazamia kuthibitishiwa.

KULINGANISHA KATI YA MANENO YA UFAHAMU NA HEKIMA

Tofauti kati ya neno la ufahamu na neno la hekima ni kuwa neno la ufahamu hukasia kweli aidha za sasa au za zamani. Neno la hekima hukasia ufahamu jinsi kweli hizo zinatakiwa kushughulikiwa kulingana na mpango bora wa Mungu.

Kwa kuwa neno la ufahamu hukasia kweli aidha za sasa au za zamani, haishughulikii siku za baadaye. Neno la hekima hukasia siku za baadaye na hekima isio kawaida katika kutenda mapenzi ya Mungu kama yaonekanavyo, kabla yatendeke.

Vipawa Hufanya Kazi Pamoja

Kwa kusudi la kujifunza, na kwa kuwa zimeorodheshwa kando katika Wakorintho tunajifunza vipawa hivi viwili kando. Lakini mara nyingi vinatendeka pamoja hata ni tofauti kuzitofautisha.

➢ *Yohana Akiwa Patmo*

Wakati Yohana alikuwa amefungwa katika kisiwa cha Patmo, hakuwa na ufahamu wa kisasa kuhusu makanisa ya Asia. Mungu alimtokea na kumpa hali ilivyokuwa sasa ya makanisa alipoandika barua kwa saba kati yao. Hiyo ilikuwa ni utenda kazi wa neno la ufahamu kwa kuwa lilishughulikia kweli hizo. Kisha Mungu akaendelea na kumwambia kile kila kanisa litafanya siku zijazo. Hiyo ilikuwa utenda kazi wa neno la hekima.

➢ *Anania*

Anania, kama tulivyojadiliana katika Somo la Tisa alipewa kweli nyingi Mungu alipomwambia aende kwa Saulo na kumwekelea mikono. Lakini, Anania alipokuwa na uoga kuendea, Mungu alimhakikishia akimwambia kile alimchagulia Saulo kufanya na mambo yatakayomfanyikia Saulo siku za usoni. Hiyo ilikuwa utendakazi wa neno la hekima.

YESU ALIENENDA KATIKA NENO LA HEKIMA

Ni muhimu kukumbuka tunapojifunza maisha ya Yesu kuwa Yesu alijitolea katika mambo ya kimungu na kutenda hapa duniani kama wanadamu walivyoumbwa kutenda.

Mwanamke Kisimani

Yesu alipokea neno la ufahamu kuwa mwanamke kisimani alikuwa na wanaume watano naye alikuwa akiishi katika uzini na mmoja. Badala ya kutenda katika ufahamu huu kwa kawaida, alipokea neno la hekima na kutenda katika ufunuo usio wa kawaida. Badala ya kumwita mzini kulingana na sharia, alitenda kulingana na neno la hekima alilopokea. (Yohana 4:16-29).

Kwa kutenda katika neno la hekima, sisi pia tutakuwa wa kufaulu zaidi katika huduma zetu.

Lazaro

Yesu aliposikia ugonjwa wa Lazaro, Yeye mara moja alijua kifo hiki kingeleta utukufu kwa Mungu katika ufufuo.

Yohana 11:4,14,17,23 Yesu aliposikia hayo, Alisema, "Ugonjwa huu sio kwa ajili ya mauti, bali kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kuwa Mwana wa Mungu aweze kutukuzwa katika hii."

Kisha Yesu akawaambia wazi, "Lazaro ameaga."

Kwa hivyo Yesu alipofika, alipata kuwa tayari alikuwa kaburini kwa siku nne.

Yesu akamwambia, "Kakako atainuka tena."

Kijana Tajiri

Wakati kijana tajiri alimkimbilia Yesu, alimwuliza Yeye,

Matayo 19:16b,17,21 "Mwalimu Mwema, je, nifanye kitu gani kizuri ili nipate uzima wa milele?"

Yesu hakulijibu swali lake. Badala yake, aliiendea shida yenyewe.

Basi akamwambia, "Kwa nini mwaniuliza mwalimu mwema? Hakuna aliye mwema ila tu Mmoja, ambaye, ni Mungu. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, basi linda amri."

Naye Yesu akaorodhesha sita ya zile amri kumi. Kijana akajitahidi kuwa alifanya haya kutoka ujana wake. Naye Yesu akamjibu,

"Ikiwa unataka kuwa mkamilifu, nenda, kisha uza kile ulicho nacho na kisha uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; nawe uje, unifwate."

Je, Yesu alijua vipi kuwa shida yenyewe ilikuwa katika upendo na kujihuzisha kwa mtu huyu juu ya mali yake? Kupitia utenda kazi wa neno la ufahamu.

Je, alijua vipi njia bora ya kushughulikia shida hiyo? Kupitia utenda kazi wa neno la hekima.

Tahadhari Kuhusu Mateso

Yesu aliwahadharisha wanafunzi wake juu ya mateso yatakayokuja, lakini kwa tahadhari, Yeye aliwaahidi hekima isiyo ya kawaida.

Luka 21:12-15 Lakini kabla ya haya mambo yote, watawekelea mikono yao juu yenu na kuwatesa, wakiwaleta mbele ya masinagogi na gerezani, nanyi mtaletwa mbele ya wafalme na watawala kwa ajili ya jina Langu.

Lakini itabadilika kwenu na kuwa wakati wa ushuhuda. Kwa hivyo yatilie mioyoni mwenu msisumbuke juu ya kile mtajibu; kwa kuwa nitawapa kinywa na hekima ambayo wapinzani wenu wote hawataweza kupinga wala kubishana.

MIFANO KATIKA AGANO LA KALE

Hezekia

Maisha ya Hezekia yaliongezeka.

2 Wafalme 20:1-6 Katika siku hiyo Hezekia alikuwa mgonjwa hata kukaribia kufa. Naye Isaya nabii, mwana wa Amozi, akamwendea na kumwambia, "Naye asema BWANA: 'Iweke nyumba yako sawa, kwa kuwa utakufa, na hutaishi.' "

Naye akageukia uso wake kwa ukuta, na kumwomba BWANA, akisema, "Kumbuka sasa, ewe BWANA, naomba, jinsi nimetembea mbele zako katika kweli na moyo mkunjuvu, na nimefanya yaliyo mema machoni Mwako." Naye Hezekia akalia kwa uchungu.

Basi ikafanyika, kabla Isaya kuondoka pale sebuleni ya katikati, kuwa neno la BWANA likaja kwake, akisema, Rudi na umwelezee Hezekia kiongozi wa watu wangu, 'Basi asema BWANA, Mungu wa Daudi baba yako: "Nimeyasikia maombi yako, nimeyaona machozi yako; kweli nitakuponya. Siku ya tatu utaenda juu katika nyumba ya BWANA. Nami nitaongeza kwa siku zako miaka kumi na tano. Nitakukomboa wewe na mji huu kutoka kwa mkono wa mfalme wa Asiria; na nitalinda mji huu kwa ajili Yangu, na kwa ajili ya watu wangu"

Kuja kwa Gharika

Ufunuo kwa Nuu juu ya kuja kwa gharika kuu uliowaokoa watu na wanyama.

Mwanzo 6:12,13 Kwa hivyo Mungu aliutazama ulimwengu, na kwa kweli ulikuwa na ufisadi; kwa kuwa nafsi zote walikuwa

na njia fisadi duniani. Naye Mungu akamwambia Nuu, "Mwisho wa watu wote umewadia mbele Zangu, kwa kuwa dunia imejaa unyang'anyi ndandi yao; na tazama, nitawaangamiza na dunia."

Agano la Mungu

Wakati mwingine neno la hekima halina masharti. Mfano wa hili ni agano ambalo Mungu alifanya na Nuu.

Mwanzo 9:12-16 Naye Mungu akasema "Hii ndiyo ishara ya agano ambayo nimefanya kati Yangu na wewe, na kila kiumbe aishiye aliye nawe, kwa ajili ya vizazi vijavyo: Ninaweka upinde angani, nayo itakuwa ishara ya agano kati Yangu na na arthi. Itakuwa, ninapoleta wingu juu ya arthi, kuwa upinde utaonekana juu ya mawingu; Nami nitakumbuka agano Langu ambalo ni kati yangu na wewe na mimi na kila kiumbe wa aina yote; maji kamwe hayatakuwa gharika na kuharibu viumbe wote. Upinde utakuwa mawinguni, Nami nitaitazama ili kukumbuka agano kati ya Mungu na kila kiumbe aishiye wa kila kiumbe duniani."

Lutu Alihadharishwa

Wakati mwingine neno la hekima lina matakwa na huu ni mfano wa haya. Lutu alionywa aondoke Sodom na kwa kuwa aliitikia tahadhari hiyo maisha yake yaliokolewa. Wengine hawakuitikia tahadhari hizo, waliasi na kupotea.

Mwanzo 19:12-16 Kisha watu wakamwambia Lutu, "Je, hauna mtu mwingine hapa? Mume mkweo, wanao, mabinti wako, na yeyote uliye naye mjini – watoe nje ya hapa! Kwa kuwa tutaharibu mahali hapa, kwa kuwa vilio dhidi yao vimekuwa kubwa mbele ya uso wa BWANA, naye BWANA ametutuma tuiharibu."

Kwa hivyo Lutu akaondoka na kunena na wanawe, waliowaoa mabinti zake, na kusema, "Inuka, ondoka hapa; kwa kuwa BWANA atauangamiza mji huu!" Lakini kwa wanawe alionekana kama mzaha.

Kulipokucha, malaika walimsihi Lutu kuharakisha, wakisema, "Inuka, mchukue mkeo na mabinti wako walio hapa, usije ukaangamia katika adhabu ya mji." Naye alipochelea, wale watu wakamshika mkono, mkono wa mkewe, mikono ya binti wao, BWANA akimhurumia, nao wakamtoa nje na kumweka nje ya mji.

Danieli

Nebuchadneza alikuwa na ndoto na roho wake alisumbuka, lakini alisahau ndoto. Kisha akawataka watu wenye wasia kumwambia ndoto na pia tafsiri yake. Ikiwa hawangefanya hivyo, wote "wenye wasia" wa pale wangeuawa. Hii pia ilimjumlisha Danieli. Danieli alipokea maono ya usiku iliyomwambia ndoto pamoja na tafsiri yake.

Danieli 2:19 Basi siri ilidhihirishwa kwa Danieli katika maono ya usiku. Kwa hivyo Danieli alimbariki Mungu wa mbinguni.

MIFANO KATIKA AGANO JIPYA

Kuja kwa Ukame

Waamini walionywa juu ya kuja kwa ukame na msaada ulitumwa.

Matendo 11:28-30 Kisha mmoja wao, aliyeitwa Agabusi, akasimama na kuonyesha katika Roho kuwa kutakuwepo ukame mkubwa kote duniani, ambayo pia ilifanyika katika siku za Claudia Kaisari.

Kisha wanafunzi, kila mmoja kulingana na uwezo wake, wakapanga kutuma msaada kwa wandugu waliokuwa Yudea. Haya walifanya pia, na wakatuma kwa wazee kwa mikono ya Barnaba na Saulo.

Kufungwa kwa Paulo

Agabusi alitabiri kufungwa kwa Paulo.

Matendo 21:10,11 Nasi tulipoishi siku nyingi, nabii mmoja aitwaye Agabusi alikuja kutoka Yudea. Alipokuja kwetu, aliuchukua ukanda wa Paulo, akajifunga mikono na miguu yake mwenyewe, na kusema, "Basi asema Roho Mtakatifu, 'Basi Wayahudi Yerusalemu watamfunga mtu yule aliye na ukanda huu, na kumtoa mikononi mwa wamataifa.' "

Chombo Kwenda Mrama

Kabla ya kuenda Kriti, Paulo alionywa kuhusu chombo kwenda mrama na pia kupotea maisha na mali. Alitoa tahadhari, lakini kwa kuwa hawakufuata, chombo, mapato, na mizigo kupotea.

Matendo 27:10,21-26 Kusema, "Enyi watu, Ninaamini safari hii itaishia vibaya na hasara kubwa, sio tu kwa ajili ya mizigo na chombo, bali hata maisha yetu."

Wao hawakusikia onyo hii ya kwanza.

Lakini baada ya kujinyima chakula kwa muda mrefu, Paulo alisimama kati yao, akasema, "Enyi watu, laiti mngenisikia, na msingefunga safari kutoka Krete na kupata shida hii na hasara hizi zote. Lakini sasa ninawaombeni muwe na moyo, kwa kuwa hakuna mmoja wenu atakayepoteza maisha, meli tu ndiyo itakayopotea. Kwa kuwa palisimama kando yangu usiku huu malaika wa yule Mungu ambaye mimi ni wake na ambaye mimi ninamwabudu alinitokea, akaniambia: 'Usiogope, Paulo; lazima uletwe mbele ya Kaisari; naye Mungu, kwa wema wake, amekufadhili kwa kuwaokoa wote wanaosafiri nawe wasiangamie.' Kwa hivyo jipe moyo, enyi watu, kwa kuwa naamini Mungu kuwa itakuwa jinsi nilivyoambiwa. Lakini, ni lazima tutatupwa ufukoni mwa kisiwa fulani."

Hata baada ya Paulo kuwapa maneno haya ya hekima wachache walianza kutotii.

Matendo 27:30,31,44 Na wanamaji walipotaka kutoroka, na walikwisha kuteremsha ule mtumbwi majini, wakijisingizia kwamba wanakwenda kuteremsha nanga upande wa mbele wa meli, Paulo alimwambia yule ofisa wa jeshi na askari wake, "Kama wanamaji hawa hawabaki kwenye meli, hamtaokoka."

Na wengine, wakiwa juu na wengine wakishikilia vipande vya meli vilivyovunjika, ndivyo wote sisi sote tulivyofika salama pwani.

HUTUMIKA KUTENGANISHA KWA AJILI YA HUDUMA MAALUM

Anania atumwa kwa Saulo

Bwana alinena na Anania na kumwambia aende na kumwekelea mikono Saulo ili apate kuona na kutoka wakati huo Saulo akawa Paulo na akatengwa ili apeleke ujumbe wa wokovu kwa mataifa.

Matendo 9:11-15 Naye Bwana akamwambia, "Inuka na uende kwa barabara iitwayo Ya moja kwa moja, nawe uliza nyumba ya Yuda umtake mtu aitwaye Saulo wa Tarso, sasa anaomba. Na katika maono amemwona mtu aitwaye Anania akija ndani na kuweka mkono wake juu yake, ili apate kuona tena."

Kisha Anania akajibu, "Bwana, nimesikia kutoka kwa wengi kuhusu mtu huyu, mateso mengi aliyoyaleta kwa wateule wako Yerusalemu. Na hapa anayo mamlaka kutoka kwa kuhani mkuu kuwafunga wote waliitalo jina Lako."

Lakini Bwana akamwambia, "Nenda, kwa kuwa yeye ni chombo kilichotengwa kwa ajili ya kulibeba Jina Langu mbele ya mataifa, wafalme, na wana wa Israeli."

Saulo na Barnaba

Saulo na Barnaba walitengwa kwa ajili ya kazi maalumu kwa maagizo ya Roho Mtakatifu.

Matendo 13:1-4 Sasa katika kanisa la Antiokia palikuwa na manabii na walimu: miongoni mwao akiwa Barnaba, Simoni aitwaye pia Mweusi, Lukio wa Kurene, Manaeni ambaye alikuwa amelelewa pamoja na mfalme Herode, na Saulo. Walipomhudumia Bwana wakifunga, Roho Mtakatifu alisema, "Sasa mtenganishe kwangu Barnaba na Saulo kwa ajili ya kazi niliyowaitia."

Kisha, baada ya kuomba na kufunga, na kuwawekelea mikono, wakawatuma. Kwa hivyo, wakitumwa na Roho Mtakatifu, walishuka Seleukia, na kutoka hapo walipanda meli hadi kisiwa cha Kupro.

Mtume Yohana

Mtume Yohana alinaswa katika Roho siku ya Bwana, na kitabu kizima cha Ufunuo kikapita mbele zake.

Ufunuo 1:10 Nilikuwa katika Roho siku ya Bwana, nami nikasikia nyuma yangu sauti kuu, kama tarumbeta ...

4:2 Ghafla nikawa katika Roho; na lo, mbinguni kuna kiti cha enzi, na juu yake ameketi mmoja.

17:3 Kwa hivyo akanibeba katika Roho hadi jangwani. Nami nikamwona mwanamke ameketi juu ya mnyama mwekundu aliyejaa majina ya makufuru, akiwa na vichwa saba na pembe kumi.

21:10 Naye akanibeba katika Roho hadi mlima mkubwa na mrefu, naye akanionyesha mji mkubwa, Yerusalemu takatifu, ikishuka kutoka mbinguni kwa Mungu.

Wakati Yohana alizijua zile kweli kuhusu makanisa yale saba, alikuwa akitenda katika neno la ufahamu.

Alipojua juu ya mambo yatakayokuja, alitenda katika neno la hekima.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Andika kwa maneno yako mwenyewe neno la hekima ni nini.

2. Toa mfano wa Yesu akitenda katika neno la ufahamu na neno la hekima.

3. Je, jinsi gani neno la ufahamu na hekima kutendeka pamoja? Toa mifano maishani mwako mwenyewe.

Somo la Kumi na Moja

Kipawa cha Nguvu cha Imani

1 Wakorintho 12:9-11 Kwa mwingine imani na Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji wa miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi. Lakini Roho yule yule hutenda mambo haya yote, akipeana kwa kila mmoja, kadri apendavyo.

Utumainifu wa Sauti	*Vipawa Tisa vya Roho Mtakatifu*	**Nguvu**
Ndimi	**Ufunuo**	**➥Kipawa cha Imani**
Tafsiri ya Ndimi	Kutofautisha Kati ya Roho	Kipawa cha Uponyaji
Unabii	Neno la Ufahamu	Kutenda Miujiza
	Neno la Hekima	

IMANI, KUTENDA MIUJIZA, VIPAWA VYA UPONYAJI

Utangulizi

Kuna vipawa vitatu vya ubainifu wa usemi – ndimi, tafsiri yake, na unabii. Vipawa hivi huonekana Mungu akitutumia.

Kuna vipawa vitatu vya ufunuo – kutofautisha kati ya roho, neno la ufahamu, na neno la hekima. Vipawa hivi ni Mungu anapodhihirisha mambo kwetu; mambo ya ulimwengu wa kawaida au ya kiroho.

Mwisho, kuna vipawa vitatu vya nguvu – kipawa cha imani, kutenda miujiza, na vipawa vya uponyaji. Vipawa vya nguvu huonekana Mungu anapoachilia imani Yake isiyo kawaida au nguvu kutiririka ndani yetu. Zile vipawa tatu vya nguvu ni kipawa cha imani, vipawa vya uponyaji, na kutenda miujiza.

Mungu hupenda kunena na watu wa ulimwengu. Wakati mwingi Yeye hunena kupitia waamini Wake. Mungu anataka kudhihirisha mambo mengi kwa ulimwengu huu. Tena, anataka kufanya hivyo kutumia waamini. Mungu anapenda kuyafikia mahitaji ya kizazi hiki, lakini Yeye hutenda kupitia watu Wake.

Ya Waamini Wote

Kila mojawapo ya vipawa vya Roho ni ubainifu wa Roho, aina tisa tofauti ambapo Yeye hutenda katika mwili wa Kristo.

Kipawa Kimoja kwa Wote

Kumekuwepo na mafundisho awali kuwa kila mwamini anatakiwa kutenda katika kipawa kimoja, au labda viwili. Ili kuyakubali mafundisho haya, ni lazima tujiulize swali moja, "Kwa nini Roho Mtakatifu aonyeshe kupitia kipawa cha ufunuo kuwepo kwa pepo wa saratani naye atunyime nguvu Zake kupitia mojawapo ya vipawa vya nguvu kumkemea pepo huyo?"

Kupimwa na Sisi Wenyewe

Utenda kazi wa vipawa vya Roho Mtakatifu maishani mwetu umepimwa tu na sisi wenyewe. Je, tuko tayari kumruhusu Mungu afanye nini ndani yetu? Je, ni muda gani tutampa Yeye? Je, chombo ni kisafi kiasi gani ili Yeye apewe kwa kukitumia?

1 Wakorintho 12:4 Sasa kuna vipaji vya kiroho vya namna nyingi lakini Roho atoaye ni mmoja.

Vipaji Huenda Pamoja

Kama tulivyojifunza awali, kila kundi la vipawa hutenda kazi kwa pamoja. Tunatakiwa kunena katika ndimi tunapopokea ubatizo katika Roho Mtakatifu. Hii hututayarisha kutenda katika Roho. Kisha tunatakiwa kuomba kwa ajili ya kipawa cha tafsiri. Hiki ni kipaji cha pili. Kisha tunatakiwa kupenda kutoa unabii. Hiyo ni kipawa cha tatu.

Kisha tunasonga hadi kundi la pili la vipawa, vipawa vya ufunuo. Kupitia hivi, Mungu hutuonyesha mambo mengi. Sehemu moja ya ufahamu uonekanao lazima uhusiane na mahitaji maishani mwetu na walioko karibu nasi. Kisha tunasonga hadi vipawa vya nguvu ambavyo ni kuachilia nguvu za Mungu ili kukutana na mahitaji hayo.

VIPAWA VYA IMANI

Maelezo

Kipawa cha imani ni imani isiyo kawaida kwa ajili ya wakati maalum na kusudi. Ni kipawa cha nguvu ili kutimiza kazi fulani katika hali yoyote tutakapokuwa kwa wakati huo.

Kipawa cha imani hutolewa wakati kinahitajika kwa kazi maalum haraka au kwa wakati ujao hivi karibuni. Wakati neno la hekima linatolewa na kutueleza jinsi kazi inatakiwa kufanywa, litawasha kipawa cha imani kutenda kazi ili kuetenda kwa ujasiri kazi hiyo kulingana na kile Mungu tayari amepanga.

Jinsi ya Kupokea

Kipawa cha imani hupokelewa kwa utendakazi wa vipawa vya ufunuo. Imani isiyo kawaida huja juu ya mwamini wakati kipawa cha neno la hekima hudhihirisha utendakazi wa nguvu za Mungu zilizo karibu kuonekana. Hii hutuachilia ili kutumika kwa ujasiri juu ya ufunuo ambao tumepokea.

Jinsi Kinaonekana

Mara nyingi kipawa kisicho kawaida cha imani hujumuika katika utenda kazi wa vipawa cha nguvu. Hii inaweza kuonekana katika maneno ya kuamrisha ya nguvu kama vile Yesu alivyoiambi dhoruba "Amani, tulia!" au alivyosema, "Lazaro njoo!"

Baada ya kupokea ufunuo juu ya kile Mungu anataka kifanyike kupitia neno la hekima, kipawa cha imani kitakuja juu ya mwamini ili kumaliza kazi hiyo. Imani hii maalumu huonekana wakati mpango fulani huonekana kwa neno la hekima. Hii humwachilia mwamini kutenda kwa ujasiri kile amepewa na Mungu.

Ni wakati katika maisha ya mwamini ambapo hana usumbufu katika kuamini. Anajua kile Neno la Mungu linasema, nini mapenzi ya Mungu, na kuwa ana nguvu za Mungu zisizo kawaida ndani yake katika kufanikisha hayo. Kipawa cha imani kinapokuwepo maneno tunayonena hutokana na Roho Mtakatifu na yana mamlaka kama ya Mungu ndiye ameyanena. Matokea ya kipawa cha imani yanaweza kuwa kutenda miujiza au uponyaji.

Kuitikia Kipawa cha Imani

Kunayo matokeo mbalimbali ya kipawa cha imani.

- ➢ Huleta utukufu kwa Mungu.
- ➢ Huwafanya wengine kumwamini Mungu.
- ➢ Huleta mshangao na hofu.

Ukweli wa Mungu aishiye akihuzishwa katika shughuli za wanadamu huonekana.

AIDA NNE YA IMANI

Imani Iokoayo

Imani ambayo tunampokea Yesu kama Mwokozi ni kipaji kutoka kwa Mungu ambacho huja kupitia Neno la Mungu.

Waefeso 2:8 Kwa neema mmeokolewa kwa njia ya imani, na hiyo haikutokana nanyi wenyewe; ni kipawa cha Mungu ...

Matunda ya Imani

Uaminifu huorodheshwa kama mojawapo ya matunda ya Roho. Ni imani inayokuwa katika maisha ya Mkristo ili kumuimarisha katika mienendo ya kiroho.

Wagalatia 5:22,23 Lakini matunda ya Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, ukarimu, wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi. Hakuna sharia inayoweza kupinga mambo hayo.

Imani ya Jumla

Kuna imani ya kijumla, ya kila siku ambayo huja katika kumjua Mungu, kulijua Neno Lake na kuamini. Ni kuwa na imani kuwa kile Amesema atatenda. Imani hii huimarisha kila tunapoomba na kupokea jibu la maombi hayo.

Mariko 11:24 Kwa hivyo nawambia, chochote mtakachouliza mkiomba, amini kuwa mmekipokea, nanyi mtayapokea.

Kipawa cha Imani

Kipawa cha imani ni imani isiyo kawaida kwa ajili ya muda na kusudi maalumu.

MIFANO YA KIPAWA CHA IMANI KUTOKA KATIKA HUDUMA YA YESU

Imani ya Ufufuo

Yesu alihudumu kila mara katika kipawa cha imani. Ifwatayo ni baadhi tu ya nyakati hizo.

➢ *Kumfufua Mtu aliyekufa*

Luka 7:12-15a Naye alipofika langoni la mji, tazama, mtu mfu alikuwa anatolewa, mwana wa pekee wa mamaye; naye alikuwa mjane. Nao umati mkubwa kutoka mjini ulikuwa naye.

Bwana alipomwona, akamhurumia na kumwambia, "Usilie."

Kisha akaja na kuliguza jeneza lililofunguliwa, na waliombeba wakasimama kimya. Naye akasema, "Kijana, Nakuamuru, inuka."

Na yule aliyeaga akaketi na kuanza kuzungumza.

➢ *Lazaro*

Hata wakati Yesu aliambiwa juu ya ugonjwa wa Lazaro, alijua kuwa kifo cha Lazaro na ufufuo vitaleta wakati wa mafundisho juu ya kifo chake mwenyewe na ufufo.

Yohana 11:43b,44 ... Akalia kwa sauti kuu, "Lazaro, toka nje!"

Naye yule aliyeaga akatoka nje akiwa amefungwa sanda mikono na miguu, na uso wake ulikuwa umefunikwa. Yesu akawaambia, "Mfungueni, mkamwache aende zake."

➢ *Kwa Ajili ya Ufufuo Wake Mwenyewe*

Kazi kuu ya kipawa cha imani ilikuwa Yesu alaze uhai Wake ili kulipia adhabu ya dhambi za watu wote na kujua kuwa Yeye atafufuka.

Yohana 11:25,26 Yesu akamwambia, "Mimi ndimi ufufuo na uzima. Yeye aniaminie, hata akifa, yeye ataishi. Naye aishiye na kuniamini hatakufa. Je, mnaamini haya?"

Imani Itendayo Miujiza

➢ *Dhoruba Kali*

Mariko 4:37,38 Na pakatokea dhoruba kali, na mawimbi yakapiga juu ya chombo na kuwa kikawa kinajaa maji. Lakini yeye alikuwa sehemu ya nyuma ya mashua, amelala juu ya mto. Nao wakamwamsha wakisema, "Mwalimu, haujali kuwa twaangamia?"

Kisha akaamka na kukemea mawimbi, na kuiambia bahari, "Amani, tulia!" Na mawimbi yakatulia na pakawa utulivu mkuu.

➢ *Alitembea Juu ya Maji*

Mara nyingi tunapuuza kweli kuwa Yesu, kama mwanadamu, alitembea juu ya maji. Alitenda hapa duniani kama mwanadamu, sio Mungu. Kila mara tunamtazama Petro kama mfano wa kushindwa katika hali hii. Itakuwa bora sisi kukumbuka kuwa Petro alifanya jinsi Yesu alifanya. Alitimiza kazi za Yesu wakati huu, hata kama kwa muda mfupi.

Matayo 14:25-32 Basi usiku karibu na mapambazuko Yesu aliwaendea, akitembea juu ya maji. Na wanafunzi walipomwona Yeye akitembea juu ya bahari, waliingiwa na hofu, wakasema, "Ni mzimu!" Wakapiga kelele kwa hofu.

Na punde Yesu akasema nao, "Tulieni, ni mimi msiogope!"

Naye Petro akamjibu akisema, "Bwana, kama ni wewe, amuru nitembee juu ya maji nije kwako."

Yesu akasema, "Haya, njoo." Basi Petro akashuka kutoka ile mashua, akatembea juu ya maji akamwendea Yesu.

Lakini alipouona ule upepo, aliogopa; akaanza kuzama; akalia kwa sauti, "Bwana, niokoe!"

Hapo, Yesu akanyosha mkono Wake, akamshika na akamwambia, "Ewe mwenye imani haba, kwa nini uliona shaka?"

Nao walipoingia chomboni, mawimbi yakatulia.

KIPAWA CHA IMANI KATIKA KUNENA HUKUMU YA MUNGU

Hukumu

Kipawa cha imani kinaweza kutendeka katika njia ionekanayo haribifu kwa ajili ya kulinda mwili wa Kristo. Labda, mwili wa Kristo kwa ajili ya dhambi maishani mwao, au hofu kuhusu kile watu watasema, au kwa sababu ya kujihisi kutokuwa wa maana na kutokutenda katika sehemu hizi. Bila vipawa vya ufunuo kutenda kazi maishani mwetu ni vigumu kutenda katika kipawa cha imani kwa njia ifwatayo.

➢ *Na Yesu*

Yesu aliulaani mti.

Matayo 21:19 Na akiuona mti kando ya njia, Aliuendea na kukuta hauna chochote bali matawi, naye akauambia, "Usizae tena matunda milele!" Papo hapo huo mti ukanyauka.

➢ *Na Petro*

Baada Anania kuanguka na kufa, Petro alinena laana kwa Safira kwa kuwa kipawa cha imani kiliachiliwa kwa neno la hekima.

Matendo 5:9-11 Kisha Petro akamwambia, "Vipi kuwa mmekubaliana pamoja kumjaribu Roho wa Bwana? Tazama, miguu ya wale waliomzika mumeo ipo mlangoni, nao watakutoa nje."

Na punde akaanguka miguuni pake na kufa. Nao vijana wakaja na kumkuta ameaga, na kumtoa nje, wakamzika karibu na mumewe. Kwa hivyo hofu kuu ikaja juu ya kanisa nzima na juu ya wote waliosikia mambo haya.

➢ *Na Paulo*

Matendo 13:8-12 Lakini huyo mchawi Elima (Kama alivyokuwa anaitwa Kigiriki) aliwapinga, ili kumzuia mkuu wa kisiwa akaigeukia imani ya Kikristo.

Kisha Saulo, ambaye aliitwa pia Paulo, akijawa na roho Mtakatifu, akamtazama na kumwambia, "Wewe uliyejaa ulaghai na mdanganyifu, ewe mtoto wa ibilisi, adui wa haki zote, hukomi hata mara moja kuzipotosha njia za Bwana zilizonyooka? Na sasa, kweli, mkono wa Bwana uko juu yako, nawe utakuwa kipofu, usilione jua kwa muda." Na punde ukungu ukaja juu yake, naye akaanza kwenda huku na huko akitafuta mtu kumshika mkono amuongoze.

Yule mkuu wa kisiwa akaamini, alipoona yaliyotokea, kwa mshangao kwa mafundisho ya Bwana.

KIPAWA CHA IMANI HULETA ULINZI

Daudi na Koliati

1 Samueli 17:32,38-40,45-49 Kisha Daudi akamwambia Saulo, "Na roho ya mtu yeyote isimshinde; mtumishi wako ataenda na kupigana na Wafilisti."

➢ *Kuziweka kando Mbinu za Mwanadamu*

Kwa hivyo Saulo akamvisha Daudi kwa silaha yake, na kuiweka kichwani dari lake; pia alimvisha koti la vita. Naye Daudi akauweka sawa upanga juu ya silaha yake, akajaribu kutembea, kwa kuwa hakuwa amevijaribu. Daudi akamwambia Saulo, "Siwezi kutembea katika hivi, kwa kuwa sijavijaribu."

Kwa hivyo Daudi akavivua. Kisha akachukua vitu vyake mkononi mwake; naye akajichagulia mawe matano yaliyonyooka kutoka pangoni, na kuyaweka ndani ya mkoba wa mchungaji, katika mfuko aliokuwa nao, na ukanda wake ulikuwa mkononi. Naye akamkaribia Mfilisti.

➢ *Kipawa cha Imani*
Neno la Hekima

Kisha Daudi akamwambia Mfilisti, "Unanijia kwa upanga na mkuki. Lakini naja kwako katika jina la BWANA wa majeshi, Mungu wa jeshi la Israeli, ambaye umemdharau. Siku hii BWANA atakuweka mkononi mwangu, na nitakushinda na nitoe kichwa chako. Na siku hii nitatoa nyama katika kambi ya Wafilisti niwape ngege wa angani na wanyama ardhini, ili dunia nzima ijue kuwa kuna Mungu katika Israeli. Kisha makusanyiko hawa wote watajua kuwa BWANA haokoi kwa upanga na mkuki; kwa kuwa vita ni vya Bwana, naye atakuweka wewe mikononi mwangu."

➢ *Imani Huleta Ushindi*

Na ikawa hivyo, yule Mfilisti alipoinuka na na kumkaribia Daudi, naye Daudi akakimbia kwenye jeshi ili kukutana naye Mfilisti. Kisha Daudi akaweka mkono wake ndani ya mfuko wake na kutoa jiwe; na kuliweka katika kamba na kumpiga nalo Mfilisti kichwani, hata jiwe likazama usoni mwake, naye akaanguka kifudifudi ardhini.

Danieli

➢ *Maneno ya Mfalme ya Imani*

Danieli 6:16-22 Kwa hivyo mfalme akatoa amri, nao wakamleta Danieli na kumtupa ndani ya shimo la simba. Lakini mfalme akasema, akimwambia Danieli, "Mungu wako, unayetumikia kila mara, atakukomboa."

Kisha jiwe likaletwa na kuwekwa mbele ya lango la shimo, naye mfalme akaweka chapa kwa pete yake mwenyewe na chapa za bwana wake pia, ili kusudu kumhusu Danieli lisibatilishwe.

Basi mfalme akaenda katika nyumba ya kifalme na akafunga usiku kucha; na wala hapakuletwa waimbaji mbele zake. Pia alipoteza usingizi. Kisha mfalme akaamka asubuhi mapema na kuenda haraka kwenye shimo la samba. Naye alipofika, akamwita Danieli kwa huzuni. Mfalme akasema, akimwambia Danieli, "Danieli, mtumishi wa Mungu aishiye, je, Mungu wako, unayemtumikia bila kuchoka, ameweza kukukomboa kutoka kwa simba?"

➢ *Ushindi*

Kisha Danieli akamwambia mfalme, "Ewe mfalme, uishi milele! Mungu wangu aliwatuma malaika Wake na kufunga vinywa vya simba, hata hawakunidhuru, kwa kuwa nilipatikana bila hatia mbele Zake; ewe mfalme, sina kosa lolote kwako."

Shadraki, Meshaka Na Abedinego

Walipoamuriwa kumwabudu mfalme, walikataa hata kama ingemaanisha mauti yao. Lakini gundua kwa maneno yao, walimwamini Mungu kwa kuwakomboa.

Danieli 3:16-18,20-26 Shadraki, Meshaka, na Abedinego walijibu na kumwambia mfalme, ewe Nabukadneza, hatuwezi kujibu.

➢ *Kipaji cha Imani*

"Ikiwa ni hivyo, Mungu wetu tunayemtumikia anaweza kutukomboa kutoka kwa moto mkali, Naye atatukomboa kutoka mikononi mwako, ewe mfalme.

➢ *Kujitolea Kikamilifu*

"Lakini hata kama si hivyo, na ijulikane kwako, ewe mfalme, kuwa hatuwatumikii miungu wako, wala hatutaabudu sanamu yako ya dhahabu uliyoumba."

Naye akawaamuru watu wakubwa waliokuwa katika jeshi lake kuwafunga Shadraki, Meshaka na Abednego, na kuwatupa kwenye moto mkali. Kisha watu hawa wakafungwa wakiwa na mavazi yao, vitambaa, koti, vilemba na mavazi mengine, nao wakatupwa katikati mwa jiko la moto.

Kwa hivyo, kwa kuwa amri ya mfalme ilikuwa dharura, na jiko likawa moto zaidi, miale ya moto huo uliwaua wanaume waliowashika Shadraki, Meshaka na Abednego. Nao wanaume hawa watatu, Shadraki, Meshaka na Abednego, wakaanguka ndani kwenye joko la moto mkali wakiwa wamefungwa.

➢ *Mungu kuwa Nao!*

Kisha mfalme Nebukadneza akashangaa; na akainuka kwa haraka na kusema, akiwambia washauri, "Je, tuliwatupa wanaume watatu wakiwa wamefungwa katika moto?"

Walimjibu wakimwambia mfalme, "Ni kweli, ewe mfalme."

"Tazama!" akawajibu, "Nawaona wanaume watano wakiwa wasiofungwa katika moto; nao hawajaumizwa, na umbile la yule

wa nne ni kama Mwana wa Mungu." Kisha Nebukadneza akaenda karibu na lango la jiko la moto na kusema, "Shadraki, Meshaka na Abednego, watumishi wa Mungu Aliye Juu zaidi, tokeni, na mje hapa."

Kisha Shadraki, Meshaka, na Abednego wakatoka kwenye moto.

KIPAJI CHA IMANI KUTENDSA KAZI LEO

Kipaji cha imani hutolewa kwa mwili wa Kristo kwa sababu nyingi. Kama tunavyojifunza kutenda katika hiyo tutatumiwa na Mungu kwa ajili ya kujilinda, walio karibu nasi na mwili wa Kristo.

Bila imani, ni vigumu kumfurahisha Mungu.

Kwa imani, hakuna kisichowezekana kwa kuwa kipawa cha imani kinapotenda kazi, nguvu za Mungu kwa ajili ya miujiza zitaachiliwa.

Tunaanza kwa kutenda imani yetu wenyewe. Tunapofika tamati ya imani, kila mara, kipaji hiki malum cha imani kitaachiliwa wakati Mungu anatupa neno la hekima.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kwa maneno yako mwenyewe eleza vipawa vya nguvu. Orodhesha vyote vikiwa vitatu.

2. Je, kipawa cha imani ni nini?

3. Toa mfano kutoka maishani mwako wa kutendakazi wa kipawa cha imani, au toa mfano kutoka katika Biblia kwa maneno yako mwenyewe.

Somo la Kumi na Mbili

Kipawa cha Nguvu
Kutenda Miujiza

1 Wakorintho 12:9-11 ...kwa mwingine imani na Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji wa miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi. Lakini Roho yule yule hutenda mambo haya yote, akipeana kwa kila mmoja, kadri apendavyo.

	Vipawa Tisa vya Roho Mtakatifu	
Utumainifu wa Sauti	**Ufunuo**	**Nguvu**
Ndimi	Kutofautisha Kati ya Roho	Kipawa cha Imani
Tafsiri ya Ndimi	Neno la Ufahamu	Kipawa cha Uponyaji
Unabii	Neno la Hekima	➥**Kutenda Miujiza**

UTENDA KAZI WA MIUJIZA

Maelezo

Utenda kazi wa miujiza ni uingiliaji usio kawaida katika njia na hali ya kawaida.

Ni matukio isiyo kawaida ya nguvu za Mungu ambapo sharia za kawaida hubadilishwa, kuondolewa na kuongozwa.

Ni kipawa cha Roho kitolewacho kwa mwamini kuwa atende miujiza.

Vipawa vya nguvu hutendeka kwa karibu sana na pia vipawa vya ufunuo.

Jinsi Vipawa hutenda Kazi

Utenda kazi wa miujiza huanza na ufahamu unaopokelewa kwa kawaida na usio kawaida kwa utenda kazi wa kipawa cha kiroho cha neno la ufahamu. Kisha, kipawa cha kiroho cha neno la hekima likitenda kazi. Wakati hii inafanyika, kila mara tunajiona tukitenda mwujiza kabla utendeke. “neno hili la hekima” huachilia kipawa cha imani. Hii inapofanyika, tunaanza kufanya yale tuliyoona tukifanya katika neno la hekima.

Hii inaitwa utenda kazi wa miujiza kwa kuwa sisi tu wahusika katika kutenda miujiza. Kile tunaona kwa neno la hekima katika Roho, tunaanza kutenda wakati kipawa cha imani kinaachiliwa. Tunapoanza kuenda katika utenda kazi wa miujiza, nguvu za Mungu huachiliwa na miujiza hutendeka. Basi, kuna sehemu ya Mungu na sehemu yetu.

Ni Rahisi

Kwa kuwa hii ni rahisi na kuendeleza utenda kazi wa vipawa vya Roho Mtakatifu, tunakuta kuwa ni rahisi kutenda katika kipawa cha kiroho cha kutenda miujiza kama vile ilivyo kutoa tafsiri ya ndimi, au kuenenda katika vipawa vyote tisa vya Roho.

Ufunguo ni kupokea ufunuo kwa kupokea neno la hekima.

Kusudi la Miujiza

Kusudi la kimungu kwa ajili ya miujiza ni:

- ➢ kukombolewa kutoka hatarini
- ➢ kinga
- ➢ kuwapa na kusaidia wanaokosa
- ➢ kutekeleza hukumu
- ➢ kuthihirisha mwito wa mtu
- ➢ kulithihirisha Neno ambalo limehubiriwa

utenda kazi wa miujiza kila mara utaleta utukufu kwa Mungu na kuifanya imani ya watu kupanuka.

UTENDA KAZI WA MIUJIZA KATIKA MAISHA YA YESU

Hapakuwa na miujiza iliyoandikwa wakati wa miaka thelathini ya kwanza katika maisha ya Yesu. Alipokea nguvu za Roho Mtakatifu na baadaye kipawa cha utendaji miujiza ukaanza katika maisha Yake.

Miujiza ya Kwanza ya Yesu

Ubainifu wa kwanza kabisa usio kawaida katika maisha ya Yesu ulikuwa mwujiza. Yeye aliingilia mbinu ya kawaida ya utendeti wa mambo na kugeuza maji na kuwa mvinyo. Yeye hakugeuza maji ya matunda ya mizabibu na kuwa mvinyo ambayo ingekuwa ni kuharakisha mbinu ya kawaida. Aligeuza maji kuwa mvinyo. Hii haingefanyika bila uingiliaji wa kimungu.

➢ *Yesu Alinena – Walitenda*

Yohana 2:7-11 Yesu aliwaambia, "Jazeni mitungi hiyo maji." Nao wakaijaza mpaka juu".

Kisha akawaambia, "Sasa choteni mkampelekee mkuu wa karamu." Nao wakampelekea.

Mkuu wa karamu alipoonja haya maji yaliyogeushwa divai, naye hakujua yalikotoka (bali watumishi waliochota hayo maji walijua), mkuu wa karamu akamwita bwana harusi. Na kumwambia, "Kila mtu mwanzoni huleta divai mzuri, na wakati wageni wametosheka, kisha ile isiyo nzuri; lakini wewe umeiweka divai mzuri hadi sasa."

➢ *Matokeo*

Wanafunzi waliamini.

Hii ilikuwa mwanzo wa ishara Yesu alifanya huko Kana, Galilaya, akaonyesha utukufu wake; nao wanafunzi wake wakamwamini.

Kuwalisha Elfu Nne

Baadhi ya miujiza Yesu alifanya ilikuwa kutosheleza watu.

Matayo 15:33-38 Kisha wanafunzi Wake wakamwambia, "Ni wapi tunaweza kupata mikate ya hapa jangwani ili kuutosheleza huu umati?"

Yesu akawaambia, , "Je, mnayo mikate mingapi?"

Nao wakamjibu, "Saba, na samaki wachache."

Naye akaamuru umati kuketi chini. Naye akaichukua mikate saba pamoja na samaki na kushukuru, akaivunja na kuwapa wanafunzi Wake; nao wanafunzi wakawapa umati. Na wote wakala na kushiba, na wakakusanya makombo na kujaza vikapu vikubwa. Hao waliokula walikuwa wanaume elfu nne, bila kuhesabu wanawake na watoto.

Shuhuda huleta Imani

Yohana 20:30,31 Na kweli Yesu alifanya ishara nyingi mbele mwa wanafunzi Wake, ambayo haikuandikwa katika kitabu hiki; lakini hii imeandikwa ili mwamini kuwa Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu, na kuwa ukiamini utapata uzima katika jina Lake.

MIFANO YA MIUJIZA KATIKA AGANO LA KALE

Musa

Miujiza ilitumika kuimarisha mamlaka ya Musa itokayo kwa Mungu mbele ya Farao.

➢ *Kuimarisha Mamlaka*

Kutoka 7:9 Farao anaponena nawe, akisema, `Tenda mwujiza mwenyewe,' basi utamwambia Haruni, `Chukua fimbo yako na kuirusha mbele ya Farao, na ibadilike na kuwa joka.'

Kutoka 7:4,5 Lakini Farao hatawasikia, ili niuweke mkono wangu juu ya Misri na kuleta jeshi langu na watu Wangu, wana wa Israeli, nje ya nchi ya Misri kwa hukumu kuu. Nao Wamisri watajua kuwa mimi ndiye BWANA, ninaponyosha mkono wangu juu ya Misri na kuwatoa wana wa Israeli kutoka kwao.

Eliya na Elisha

➢ *Eliya Alitenganisha Yordani*

2 Wafalme 2:8 Sasa Eliya alilichukua vazi lake, akalikunja, na kuyapiga maji; nayo yakagawanyika pande mbili, ili wawili hawa wakavuka kwenye inchi kavu.

Eliya alijulikana kama mtu wa Mungu naye alitembea katika miujiza sana nyakati hizo. Ilipokuwa wakati wake kuenda kuwa na Bwana, Elisha aliwekwa kwa jaribio. Wakati Eliya alitoweka katika gari la farasi, Elisha aliweza kuona katika ulimwengu wa roho na kumwona akienda. Elisha hakutenda miujiza mingi hadi alipomwona Eliya akipaa juu.

Kisha Elisha akalichukua vazi la Eliya na kurejea Mto Yordani. Eliya alikuwa amegawanya mto nao wakavuka awali siku hiyo huku nabii hamsini wakiwatazama. Je, Elisha angefanya nini? Elisha aliuliza mara mbili roho wa Eliya. Ahadi ilikuwa, "utakaponiona nikitoweka, itakuwa yako." Alikuwa amemwona Eliya akitoweka. Sasa je, angetenda katika imani?

➢ *Elisha Alitenganisha Yordani*

2 Wafalme 2:13-15 Pia alichukua vazi la Eliya lililoanguka kutoka kwake, na akarudi akasimama kando ya mto Yordani. Kisha akalichukua vazi la Eliya lililoanguka kutoka kwake, na kuyapiga maji, na kusema, "BWANA Mungu wa Eliya yuko wapi?" Na pia alipoyapiga maji, yaligawanyika katikati; naye Elisha akavuka upande wa pili.

Sasa wana wa nabii waliotoka Yeriko walimwona, wakasema. "Roho wa Eliya anakaa juu ya Elisha." Nao wakaja kukutana naye, wakainama na kumsujudia.

Mwujiza ulimweka Elisha kama nabii.

Kichwa cha Shoka Kuelea

Mwujiza huu ulifanyika kwa ajili ya hitaji funali. Sababu mojawapo hatuoni miujiza mingi ni kwa ajili ya kutokuamini kwetu. Tunawaza kuwa hii au ile si muhimu kabisa kuwa Mungu aingilie kati. Tunapoanza kutoka nje kwa imani na kutarajia vipawa vya Mungu kutendeka maishani mwetu, tutaona kipawa cha kutenda miujiza kikifanyika.

2 Wafalme 6:4-7 Basi akaenda nao. Nao walipofika yordani, walikata miti. Lakini mmoja alipokuwa akikata mti, kichwa cha shoka la chuma likaanguka ndani ya maji; naye akapaaza sauti akisema, "Lo, bwana! Kwa kuwa ilikuwa ya kuazimwa."

Na mtu wa Mungu akasema, "Lianguka wapi?" Naye akamwonyesha mahali pale. Basi akakata kijiti, na kukitupa pale, na kuifanya shoka ielee majini. Kwa hivyo akasema,

"Ichukue wewe mwenyewe." Kwa hivyo akanyosha mkono wake na kuichukua.

Samsoni

Samsoni aliwaruhusu wananchi wake wamfunde na kupelekwa mikononi mwa Wafilisti.

Waamuzi 15:14,15 Alipofika Lehi, Wafilisti wakamjia wakimpigia kelele. Kisha roho wa BWANA akamjia juu yake kwa nguvu; na kamba zilizomfunga mikono yake zikawa kama katani iliyochomwa kwa moto, na vifungo vyake vikaanguka chini toka mikononi mwake. Ndipo akaona mfupa mpya wa taya la punda, akanyoosha mkono akauchukua na kuua Wafilisti wapatao elfu.

Baada ya haya, Samsoni akawa na kiu na Mungu akatenda mwujiza mwingine kwa ajili yake.

Waamuzi 15:18,19a Kisha akawa na kiu kikali; akamlilia BWANA akisema, "Umempa mtumishi wako ushindi huu mkuu; je, sasa nife kwa kiu na kuanguka mikononi wa wasiotahiriwa?"

Kwa hivyo Mungu akafunua shimo huko Lehi, pakatoka maji, naye akanywa; na roho wake akarejea, na akapata nguvu. Hivyo chemichemi hiyo ikaitwa En-hakore, nayo iko mpaka leo.

Ikiwa Mungu alijali kutosheleza kiu cha Samsoni, kwa nini asijali mahitaji yetu leo? Mungu anataka kuhuzishwa katika kila sehemu ya maisha yetu.

Samsoni hakuonekana "asiye kawaida" alipomwambia Mungu kuhusu mahitaji yake.

WAAMINI HUTENDA MIUJIZA KATIKA INJILI

Kutembea Juu ya Maji

Yesu alipokuja akitembea juu ya maji, wanafunzi waliogopa.

Matayo 14:27-29 Na punde Yesu akasema nao, "Tulieni, ni mimi msiogope!"

Naye Petro akamjibu akisema, "Bwana, kama ni wewe, amuru nitembee juu ya maji nije kwako."

Yesu akasema, "Haya, njoo." Basi Petro akashuka kutoka ile mashua, akatembea juu ya maji akamwendea Yesu.

Ikiwa tutaenenda katika kutenda miujiza, ni lazima tushinde hofu yetu ya kushindwa na hofu ya kuonekana wajinga. Ni lazima tutoke nje ya mipangilio na mitindo yetu. Gundua kuwa Petro kwanza alitamani kutembea katika vipawa visivyo kawaida aliposema, "niamuru nije Kwako juu ya maji." Petro alipokea neno la hekima na kipawa aliposikia sauti ya Yesu ikisema, "Njoo!" Petro mara moja akatii, akashuka toka mashuani na kuanza

kuenda katika utenda kazi wa miujiza alipotembea juu ya maji.

Kunasa Samaki Wengi

Yesu alimwambia Simoni Petro,
Luka 5:4-7 "Sasa peleka mashua hadi kilindini kisha mshushe nyavu zenu mkavue samaki."

Na walipofanya hivyo, walinasa samaki wengi, hata nyavu zao zikawa zinakatika. wakawaashiria wavuvi wenzao kutoka mashua ya pili waje kuwasaidia. Nao wakaja na kujaza mashua zote mbili, hata zikaanza kuzama.

Yesu alitumia tukio hili kutangaza kusudi Lake la kuwafundisha wanafunzi wake aliposema, "Nitawafanya wavuvi wa watu." Uinjilisti ulikuwa katikati ya huduma ya Yesu. Ikiwa tutafanya huduma nzuri, hata kama ni ya kijinga kwetu, lazima tuwe wepesi kuyatii maneno ya Yesu.

KUTENDA MIUJIZA KATIKA KITABU CHA MATENDO

Miujiza Ilihakikisha Neno

Matendo 8:5,6 Kisha Filipo akaenda mjini Samaria na kuhubiri Kristo kwao. Na umati kwa nia moja wakapokea mambo aliyosema Filipo, wakisikia na kuona miujiza aliyofanya.

Ahadi ya Nguvu za Miujiza

Matendo 1:4,5 Na kwa kukusanyika pamoja nao, Yeye aliwaamuru wasiondoke Yerusalemu, lakini wasubiri Ahadi ya Baba, "ambayo," Alisema, "mmesikia kutoka kwangu; kwa kweli Yohana aliwabatiza kwa maji, lakini mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu kwa siku chache zijazo."

Matendo 1:8 "Lakini mtapokea nguvu Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu; na mtakuwa mashahidi wangu Yerusalemu, na kote Yudea na Samaria, na hadi mwisho wa dunia."

Baada ya Yesu kunena maneno Yake ya mwisho hapa duniani kwa waamini wake na kuwapa kile tunataja kama Agizo Kuu, Marko anatwambia,

Marko 16:20 Nao wakaenda nje wakihubiri kila mahali, Bwana akitenda pamoja nao na kuthihirisha neno ndani yao pamoja na ishara. Amina.

Mahubiri ya Kwanza

Baada ya Roho Mtakatifu kushuka siku ya Pentekote, Petro alisimama na kutoa mahubiri yake ya kwanza. Ishara na miujiza yalikuwa sehemu ya mahubiri hayo.

Matendo 2:22,43 Enyi Waisraeli, sikilizeni maneno haya nisemayo: Yesu wa Nazareti, alikuwa mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu kwa miujiza, maajabu, na ishara, ambayo

Mungu alitenda miongoni mwenu kwa kupitia yeye, kama ninyi wenyewe mjuavyo sasa ...

Kisha hofu ikaja juu ya wote, na maajabu mengi na ishara ilifanyika kupitia mitume.

KUTENDA MIUJIZA KATIKA WAAMINI WA SASA

Miujiza inatakiwa kuthibitisha mjumbe na ujumbe. Je, tunawezaje kuishinda dunia iliyepotea, gonjwa au inayokufa na kuwa katika ufahamu uokoao wa Yesu bila kutenda katika miujiza?

Waebrania 2:3,4 Je, tutaepuka vipi ikiwa tutapuuza wokuvu mkuu, ambao mwanzo ulizungumziwa na Bwana, na kuthibitishwa kwetu na wale waliomsikia Yeye, Mungu pia akiwa shahidi katika ishara na maajabu, pamoja na miujiza mbalimbali, na vipawa vya Roho Mtakatifu, kulingana na mapenzi Yake mwenyewe?

Petro alikamilisha usiku kucha bila matokeo yoyote. Mara nyingi sisi, kama Petro, hujaribu kutenda kulingana na ufahamu wetu. Lazima tujifunze kusema, "hata hivyo kwa Neno lako …" Tunaitajika kuchukua muda kumsikia akinena, kulipokea Neno Lake kupitia vipawa vya ufunuo vya kubaini kati ya roho, neno la ufahamu, neno la hekima. Imani itakuja tunapojifunza kuwa wepesi kutii na kupiga hatua katika kipawa kisicho kawaida cha kutenda miujiza.

Kutenda Kazi Kuu Zaidi

Yohana 14:12 Amini Amini, nawambia, yeye aniaminiye, kazi ninayofanya atafanya pia yeye; na kazi nyingi zaidi kuliko hii yeye atafanya, kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu.

Kwa nini Yesu aseme "kazi zaidi" ikiwa hakumaanisha haya? Kulingana na maneno Yake, tunaweza kufanya hata "mambo makuu" wakati nguvu za Roho Mtakatifu kudhihirishwa kupitia utenda kazi wa Roho Mtakatifu maishani mwetu. Mungu anataka kuendelea kuthibitisha Neno Lake wakati kipawa cha kutenda miujiza kinaachiliwa kuonekana kwa imani yetu. Mungu, sio sisi, atapokea utukufu wote.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza utenda kazi wa miujiza kwa maneno yako mwenyewe.
2. Eleza mpangilio wa vipawa vingine vya Roho Mtakatifu ambavyo hufanyika ili kuachilia kipawa cha kutenda miujiza.
3. Tazama mwujiza wa binafsi Mungu alimfanyia Samsoni. Kwa nini hii ni muhimu?

Somo la Kumi na Tatu

Vipawa vya Nguvu vya Uponyaji

1 Wakorintho 12:9-11 ...kwa mwingine imani na Roho huyo huyo, kwa mwingine kipawa cha uponyaji na Roho huyo huyo, kwa mwingine utendaji wa miujiza, kwa mwingine unabii, kwa mwingine kubainisha roho, kwa mwingine ndimi tofauti tofauti, kwa mwingine kukalimani ndimi. Lakini Roho yule yule hutenda mambo haya yote, akipeana kwa kila mmoja, kadri apendavyo.

	Vipawa Tisa vya Roho Mtakatifu	
Utumainifu wa Sauti	**Ufunuo**	**Nguvu**
Ndimi	Kutofautisha Kati ya Roho	Kipawa cha Imani
Tafsiri ya Ndimi	Neno la Ufahamu	➥**Kipawa cha Uponyaji**
Unabii	Neno la Hekima	Kutenda Miujiza

VIPAJI VYA UPONYAJI

Ufafanuzi

Vipawa vya uponyaji ni dhihirisho la nguvu za Mungu zisizo kawaida ndani ya watu wanaotaka uponyaji.

Vimeelezwa kama vipawa(wingi) kwa kuwa kuna njia nyingi ya kupata, au kuhudumu uponyaji kwa mgonjwa. Vimeelezwa kama Vipawa (wingi) kwa kuwa nyingi ya vile vipawa tisa vya Roho Mtakatifu vinahuzishwa sana tunapomhudumia mgonjwa. Vipawa pia vimezungumziwa kwa wingi kwa kuwa kuna njia nyingi kuweka au kuhudumia mgonjwa.

Huthihirishwa kwa njia isiyo kawaida ya Roho Mtakatifu na wala si sawa na sayansi ya matibabu.

Vipawa Vinapotumika

Vipawa vya uponyaji si kwa ajili ya kutolewa kwa mwamini maalumu, au huduma. Ni vipawa vya Mungu kwa mwili wa Kristo na hasa kwa yule anayetaka uponyaji.

Vipawa hivi vinaweza kutenda kazi katika kila mwamini aliyejazwa.

Waamini wote sharti waenende katika vipawa hivi wanapofanya kazi ya Yesu na wao, kama Yesu, wamepakwa na Roho Mtakatifu.

Uponyaji na Vipawa vya Roho

Mungu ametoa kwa kanisa Lake vipawa vya kiroho aina tisa. Nyingi ya vipawa hivi vinahusiana kwa karibu na kuwaponya wagonjwa. Lazima zote tujifunze kuhudumu katika vipawa hivi tunapowahudumia wagonjwa.

UPONYAJI NA NENO LA UFAHAMU

Ufafanuzi

Je, unakumbuka maelezo juu ya neno la ufahamu? Ni ufunuo usio kawaida wa Roho Mtakatifu juu ya kweli fulani, sasa au awali, kuhusu mtu au hali, ambavyo havikujifunza kupitia fikira za kawaida.

Mara nyingi katika kuhudumu uponyaji, Mungu atadhihirisha neno la ufahamu kuhusu ugonjwa ambao anataka kuponya.

Wakati mwingine ni ya mtu fulani mmojae, na wakati mwingine kwa ajili ya watu wengine.

Huja Kupitia

Neno la hekima huja katika njia tofauti tunapohudumu uponyaji.

➢ *Hisia*

Inaweza kuja kupitia hisia za wasiwasi katika hali fulani kwa mwili wa yule anayehudumu.

Wasiwasi hiyo mara nyingi huelezwa kama msukumo, mchecheto, au mwasho.

Inaweza kuhisiwa kama maumivu madogo.

➢ *Neno au Wazo*

Neno la ufahamu inaweza kuwa kwa neno, wazo, ambalo hueleza ugonjwa, au maumivu.

Hii inaweza kuwa sawa na ugonjwa au jina la sehemu iliyoadhirika.

➢ *Maono*

Inaweza pia kuja kama maono ya sehemu ya mwili inayoitaji uponyaji.

➢ *Mahali*

Wakati mwingine, Mungu atadhihirisha mahali alipo mtu, au hata mtu mwenyewe anayetamani kuponywa wakati huo.

Hii mara nyingi huelezwa kama mvuto (kama vile kwa spaki) kuelekea sehemu hiyo ya chumba, kwa njia fulani, ay mahali alipo mtu.

Wakati mwingine, huu huja kama nuru, au mngaro, au hisia nyingine katika Roho Mtakatifu ambaye hutuvutia kwa mtu fulani.

Bwana anaweza kutoa jina la mtu, au njia nyingine ya kitambulisho, ambayo inapotajwa itamhakikishia mtu kuwa ni wao ndio Roho Mtakatifu anaonyesha kwa ajili ya uponyaji huo.

Imani Kuachiliwa

Wakati Roho Mtakatifu huthihirisha kupitia neno la ufahamu kuwa Yeye ataponya ugonjwa fulani au mtu fulani, imani huachiliwa. Wakati mwingine ni kipawa cha imani. Mara nyingi neno la ufahamu pia huachilia kipawa cha nguvu cha uponyaji.

Kile Mungu hutufunulia, Yeye huponya!!

UPONYAJI NA NENO LA HEKIMA

Kipawa cha hekima ni kuwepo kwa hekima ya Mungu isiyo kawaida ambayo hudhihirisha jinsi tunavyoweza kuendelea katika njia ya utenda kazi ambapo tutahudumia bora katika hali fulani. Hii hutupatia hekima kujua kile tunatakiwa kufanya kuhusu ufahamu juu ya mtu tuliopokea kwa kawaida au kwa njia isiyo kawaida. Hudhihirisha jinsi tunatakiwa kuhudumia mahitaji kulingana na mpango wa Mungu na kusudi Lake.

Ni muhimu kuwa tupate muda kusikia na kuona mapenzi ya Baba ili tujue kama, nani, lini, wapi, na jinsi Yeye anatutaka kuhudumia mahitaji fulani.

Yohana 8:28 Kisha Yesu akawaambia, mtakapomwinua Mwana wa Adamu, hapo mtajua kuwa Mimi ndiye, na kuwa sifanyi chochote; bali kama alivyonifunza Baba Yangu, nayanena mambo haya."

Yohana 14:10 Je, hamwamini kuwa mimi niko ndani ya Baba, naye Baba yu ndani yangu? Kazi ninayonena kwenu sineni kwa mamlaka yangu mwenyewe; bali Baba aishiye ndani yangu hufanya kazi hizo.

Kupitia neno lahekima, Yesu aliongozwa kwa mtu fulani katika dimbwi la Bethesda, na kuhudumu uponyaji kwa njia tofauti. Aliwaponya watu wengi katika njia tofauti tofauti. Aliwawekelea mikono, aliweka kidole chake kwenye masikio yao, alitema mate na kuguza ulimi wao, aliwatolea pepo wachafu, pia hata aliwaponya kwa kunena tu.

Katika Huduma ya Uponyaji ya Paulo

Paulo pia alihudumu uponyaji katika njia nyingi tofauti tofauti kwa kuwa aliongozwa kufanya hivyo kwa utenda kazi wa neno la ufahamu. Paulo alihudumu uponyaji kupitia kuwekelea mikono na kupitia vitambaa na mavazi yaliyokuwa mikononi mwake na kuwekelewa wagonjwa. Paulo alimwinua kijana, Utikasi, kutoka kwa wafu kwa kumwangukia na kumukumbatia.

Kabla Paulo kumhudumia babaye Publio, aliomba kwanza, (ili kupokea neno la hekima juu ya jinsi ya kuhudumu uponyaji mtu huyo) na kisha akawekelea mikono yake na kumponya.

Matendo 28:8 Na ikafanyika kuwa baba ya Pablio alikuwa mgonjwa kitandani akiwa anaumwa homa na kuhara damu. Paulo akaingia ndani ili kumwona na baada ya maombi, akaweka mikono juu yake na kumponya

Kwa neno la hekima tunaweza kujiona tukihudumu uponyaji juu ya mtu kwa njia isiyotarajiwa. Wakati hii inafanyika, mara nyingi kipawa cha imani huanza kutenda kazi nasi tunafanya tu kile Mungu ametuonyesha. Wakati hii hufanyika, ubainifu wa uponyaji kila mara hutokea.

UPONYAJI NA KUBAINISHA KATI YA ROHO

Roho Wachafu

Kutofautisha kati ya roho ni ufahamu wa ndani usio kawaida katika ulimwengu war oho. Huonyesha roho, aliye nyuma ya hali, kitendo au ujumbe.

Mara nyingi roho wa mapepo wachafu ndiyo huleta magonjwa, au maradhi. Kwa mfano, hii ni roho wa saratani, kifua kikuu, kukataliwa, na chuki.

Kwa kubainisha kati ya roho, Roho Mtakatifu atatufunulia, au kuweka kidole chake juu ya chanzo hasa cha shida na mtu anaweza kukombolewa na kuponywa.

Luka 11:20 Lakini nikiwatoa pepo kwa kidole cha Mungu, basi kwa kweli ufalme wa Mungu umekuja juu yenu.

Jinsi Vipawa Hufanya Kazi

Wakati mtu anaongozwa na Roho wa Mungu, ubainifu wa kipawa cha kutofautisha kati ya roho itakuja kupitia hisia, wazo, ambalo hudhihirisha jina la pepo mchafu ambaye ni chanzo cha shida.

Litoe pepo katika jina la Yesu na mtu huyo ataponywa.

Matayo 9:32,33 Walipotoka, tazama, wakamleta Kwake mtu, bubu na mwenye pepo. Na pepo alipotolewa, bubu akaongea. Na umati ukashangaa, wakisema, "Hapajaonekana haya Israeli!"

UPONYAJI – KIPAWA CHA IMANI – KUTENDA MIUJIZA

Kipawa cha Imani

➢ *Huja kwa Njia Isiyo Kawaida*

Kipawa cha imani ni imani isiyo kawaida kwa muda na kusudi fulani. Ni kipawa cha nguvu ili kutimiza kazi fulani katika hali yoyote unayojikuta ndani wakati fulani.

Wakati mwingine, tunapogumbana na mahitaji yamwujiza wa kujenga au kumhudumia mtu ambaye mahitaji yake ya uponyaji inataka imani ya hali ya juu kuliko mahali imani yetu imefika, Mungu atatupa kwa njia isiyo kawaida imani maalumu, ili hata ikiwa vigumu kiasi gani kwetu tunajua bila shaka kuwa kutakuwepo ubainifu wa uponyaji.

Wakati mwingine, watu huja kwetu wakikosa sehemu fulani mwilini mwao kupitia ulemavu, upasuaji, au ajali. Labda imani yetu haijafikia mahali ambapo tunaweza kumwamini Mungu kwa ajili ya mwujiza. Lakini, kupitia neno la hekima, tunaweza kuwa na maono na kujiona tukihudumu kwa ujasiri katika hali fulani kwa miujiza ya kujenga ikifanyika kabla itendeke.

Tunapopokea neno hili la hekima kupitia maono, kipawa cha imani huachiliwa nasi tunajua bila shaka kuwa mwujiza utafanyika tunapohudumu hata jinsi tulivyoona ikifanyika katika roho.

➢ *Kipawa cha Imani kwa Vitendo*

Petro na Yohana walipokea kipawa cha imani siku walipoona kilema kando ya lango la hekalu.

Matendo 3:6 ... Fedha na dhahabu sina, lakini nilicho nacho nakupa wewe: katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti, inuka na utembee.

Kutenda Miujiza

Maneno ya ufahamu na hekima huachilia utenda kazi wa miujiza. Baada ya kupokea neno la ufahamu, tumeona katika roho kwa maono au hisia – mwujiza ukitendeka kabla ya kuanza kuhudumu uponyaji kwa mtu aliye na mahitaji ya mwujiza wa uponyaji.

Wakati huo, tulipokea kipawa cha imani. Sio tena tatizo katika kuamini. Tunajua bila shaka kuwa tunapohudumu uponyaji jinsi tulivyoona ikifanyika, mwujiza utatokea. Tunatenda kwa ujasiri katika kipawa cha kutenda miujiza.

Mariko 3:3,5b Kisha akamwambia mtu aliyekuwa na mkono uliodhoofika, "njoo mbele." Akamwambia yule mtu, "Nyosha mkono wako." Naye akaunyosha, na mkono wake ukawa sawa kama ule mwingine.

VIPAWA HUFANYA KAZI PAMOJA

Kama tulivyogundua, ni vigumu kusema kuwa hii au ile hali iliyoandikwa katika Maandiko ilitendeka kwa ajili ya kipawa hiki au kipawa kile.

Sababu ni rahisi.

Vipawa vya Roho Mtakatifu ni ubainifu wa Roho Mtakatifu. Vinashikamana sana hata ikawa vigumu kuvitenganisha.

Wakati mwongine vipawa hufanyika pamoja katika mtu, au viwili, au wakati mwingine kwa kundi lote. Hakikisho tulilopata ni kuwa kipawa chochote tunachoitaji kipo kwa ajili yetu!

Tunavyoenenda kwa ujasiri kile Mungu ametuonyesha, uponyaji mara nyingi hubainika.

JE, MTU MMOJA ANA KIPAWA KIMOJA?

La!

Je, mtu mmoja na kipawa cha imani, mwingine kipawa cha miujiza, na mwingine vipawa vya uponyaji?

Mtu, au watu, wanaohitaji kupokea faida za huduma ndio wanaopokea kipawa kutoka kwa Mungu kupitia utenda kazi wa vipawa vya Roho Mtakatifu. Badala ya kusema, "Ninacho kipawa hiki au kile!" ni bora kuelewa vipawa vya Roho Mtakatifu na kuwa tayari kuwahudumia wengine wakati wowote kwa moja au vipawa vyote tisa vya Roho Mtakatifu.

Undeni "Misuli ya Imani"

Mtu akibatizwa katika Roho Mtakatifu, yeye amepata vipawa vyote vya Roho. Lakini kupitia mafunzo ya uongo au dhambi maishani mwetu, anaweza kuwa alikoma au kuzuia mtiririko wa Roho Mtakatifu ndani yake.

Anapoanza kutekeleza majukumu yake ya kutenda katika ubainifu wa Roho Mtakatifu, itakua maishani mwake.

Wakati mwingine tunasema, "Mtu huyo kwa kweli anatembea katika kipawa cha uponyaji." Na kisha tunaanza kufikiria, "Wana kipawa cha uponyaji." (Kwa wazo la kinyume kuwa "Mimi sila kipawa hicho.") "Nitauliza waniombee."

Ukweli ni kuwa wametembea katika imani yao na kuenda katika kipawa hicho zaidi yako na kuwa "misuli yao ya kiroho" imeimarishwa katika sehemu hiyo.

Mbele ya Watu

Mwili wa Yesu unapokuja pamoja na vipawa vya Roho vinaruhusiwa kufanya kazi, mmoja atapewa kipawa cha ndimi na mwingine tafsiri yake, au mmoja atapewa unabii na mwingine kipawa cha ufunuo.

Mungu atagawa vipawa kati ya mwili ili wote watembee pamoja. Lakini mtu aliyeonyesha imani yake katika sehemu ya kutoa unabii labda taendelea katika unabii haraka. Nasi tena tunaanza kufikiri, "Aha, yeye ana kipawa cha unabii. (Mimi sina kipawa cha unabii.)"

Kumbuka, vipawa vyote vya Roho Mtakatifu vinaweza na vitatenda kazi katika kila mwamini aliyebatizwa katika Roho Mtakatifu na atakayeruhusu Roho Kuhudumu.

Kwa Kumalizia

2 Timotheo 1:6 Kwa hivyo nawakumbusha kuchochea kipawa cha Mungu kilicho ndani yako kupitia kukuwekelea mikono yangu.

Kila mara kuna kuwekea au kuachiliwa, utenda kazi wa vipawa vya Roho Mtakatifu kwa kuwekelea mikono. Mpate mhudumu mwingine, au mwamini, aendaye katika vipawa vya Roho Mtakatifu. Waulize waiweke mikono yao juu yako na kuachilia vipawa vitumike maishani na huduma.
Paulo aliandika,

Warumi 1:11 Kwa kuwa natamani kuwaona, ili niweze kuwawekea ndani yenu vipawa vya kiroho, ili muweze kuimarishwa.

Vipawa vya Roho Mtakatifu ni sanaa muhimu ya huduma ili kujenga mwili wote wa Kristo na kwa uinjilisti.

- ➢ Endelea "kuchochea" vipawa hivi.
- ➢ Usiviachilie vikuponyoke.
- ➢ Tarajia vifanye kazi maishani mwako.
- ➢ Viachilie, kila siku, kwa imani kamilifu na ubainifu kimakini.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, nini vipawa vya uponyaji? Kwa nini imeitwa "vipawa," wingi, wakati vipawa vingine vyote ni umoja?
2. Je, vipi kipawa cha neno la ufahamu hutenda kazi pamoja na vipawa vya uponyaji?
3. Ni kipawa gani cha Roho ambaco Mungu amekuchagulia? Jibu ni vyote! Sasa, andika orodha ya vipawa vyote vya Roho ambavyo umehudumu hata mara moja.
4. Je, ni vipawa gani vya Roho Mtakatifu ambavyo unaitaji "kuchochea" maishani mwako?